ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaybah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini – Tarehe 5 Julai, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nashukuru kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa asubuhi ya leo, mimi kwa kweli sina mchango mkubwa sana nataka niseme machache sana katika hotuba hii kwa sababu wasemaji wazuri, wachumi watu wa biashara wameshamaliza kazi. Kwa hivyo, sisi wengine itabidi tuseme machache tu ili kutoa baraka zetu.

Mhe. Spika, la kwanza nililokuwa nataka niseme bahati nzuri Mhe. Ahmed Nassor Mazrui aliniwahi ni kuhusu suala la ajira 50,000 za wazalendo, ambao Mhe. Mazrui alizungumza lakini kwa *interest* nyengine na mimi nazungumza kwa *interest* nyengine. Mimi *interest* yangu hasa nikitaka kujua katika hawa elfu hamsini mimi najaalia kwamba wapo na takwimu zipo sahihi nachukuliwa hivyo. Je, mchanganuo unaonesha katika wafanyakazi hawa elfu hamsini wamegawanyika vipi na katika sekta gani, wangapi wapo katika sekta gani, hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili tunaambiwa kwamba ni wazalendo, sasa unaposema wazalendo inajumuisha Wazanzibari na wenzetu kutoka Bara wote ni wazalendo. Vile vile naomba mchanganuo katika hawa elfu hamsini tuseme Wazanzibari kiasi inakadiriwa na wenzetu kutoka upande wa pili kama ni wangapi. Hilo ndio nataka kujua.

Mhe. Spika, nataka nipongeze juhudi zilizofanywa za ujenzi wa jengo jipya la Pemba ni juhudi njema, lakini pia mna adhma ya kujenga ofisi ya jengo la wizara. Mhe. Spika, hili ndio nataka nilizungumze kidogo kwa kweli wizara zetu nyingi Zanzibar hazina haiba za kuitwa makao makuu ya wizara. Miongoni mwa majengo ambayo hayana haiba kuwa wizara ni hili la Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji halifanani hasa kwamba hii ndilo jengo ambalo lina waziri ndani yake, mna Katibu Mkuu mna wizara nzima kwa kweli

halifanani hata kidogo. Mhe. Spika, wakifuatiwa na jengo la Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi yale yanafanana kuwa kama majumba ya kumbukumbu hayafanani kuwa ni majengo ya ofisi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naiomba serikali imsaidie waziri kumpatia fedha kujenga jengo jipya lenye hadhi ya wizara. Mhe. Spika, sasa hivi mtu yeyote akenda Wizara ya Elimu unajua kwamba hapa naingia pahala pa utawala, ukenda Afisi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo unajihisi unaingia katika jengo la utawala, ukenda Afisi ya Wanawaka na Watoto haidhuru hawajamaliza hiyo hiyo *ground floor* lakini unajihisi kwamba umo katika ofisi ya serikali. Lakini kwa kweli mengine yanapunguza ile haiba na hata kuja mgeni kutoa nchi za nje akatuona vile atasema watu hawa wakoje jamani. Kwa kweli mimi naiomba serikali imuwezeshe waziri ajenge jengo la kisasa.

Mhe. Spika, mimi nataka niulize suala kuhusu katika hizi jumuiya za maendeleo za kikanda. Unajua Tanzania bahati nzuri katika kila jumuiya tumo, kwenye *East African Community* tumo, kwenye *SADC* tumo na mote humu mna mambo ambayo ni *common*, ile mitengamano yote utakwenda kuta ndio yale yale. Huku katika Afrika Mashariki kuna Soko la Umoja wa Forodha, kuna hili Soko la Pamoja ambalo tumeingia juzi tarehe 1 Julai, halafu tunakwenda katika sarafu moja, tunakwenda katika *Political Confederation* ambapo wingi wana wasi wasi hapo ndio inakuwa Zanzibar haitwaji tena.

Vile vile kwa upande wa pili kwenye *SADC* kuna mambo haya haya kwamba kuna Umoja wa Forodha ambao umepangiwa, kuna Soko la Pamoja ambalo lategemewa 2015, kuna Sarafu Moja 2018. Mhe. Spika, suala langu ni kwamba mambo haya utekelezaji wake tutakuwa vipi au tunajiunga kama ile Jumuiya ya Afrika Mashariki nzima na *SADC* yote inaungana inakuwa pamoja, maana yake hapa mimi kidogo pananibabaisha. Mhe. Spika, ikiwa nchi zote za *SADC* pamoja na *East African Community* zinaungana wanafanya kitu kipya hapo nitakuwa sibabaiki, lakini ubabaufu wangu unakuja je, huku kuna mitengamano hii na huku kuna mitengamano hii sasa wale wanachama watakuwa katika hali gani kwa yule mwanachama aliyekuwa yuko katika pande zote mbili. Mhe. Spika, hapa namuomba Mhe. Waziri aje anifafanulie vizuri.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka anisaidie Mhe. Waziri ni hili kwamba jana nilikuwa nasoma gazeti moja la Kenya nikaona taarifa ya Waziri wa Mambo ya Ndani wa Kenya anasema kwamba kutokana na huu mtengamano wa Soko la Pamoja ambao tumeingia juzi sasa hivi watalii wakiingia katika nchi moja itakuwa hawana haja ya visa tena kuingia katika nchi nyengine. Mhe. Spika, hofu yangu mimi ni kwamba kutokana na mashirika mengi ya ndege kwamba yanapitia Nairobi na kwa sababu *Airport* yao ni nzuri kuliko yetu, na historia nyuma inaonesha wakati wa Afrika Mashariki iliyovunjika watalii wengi

walikuwa wanateremka Kenya halafu wanaingia Tanzania ikawa mapato yote ya visa yanapatikana Nairobi. Hii ndio katika Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika hali ilivyokuwa.

Mhe. Spika, suala langu je, hii taarifa kwanza aliyosema huyu Waziri wa Mambo ya Ndani wa Kenya ni kweli kwamba kuanzia sasa watalii wakiingia katika nchi moja itakuwa wakiingia nchi nyengine hawalipi tena visa. Kwa maana hiyo je, tumeshaiona hatari iliyotukabili kwamba watalii wengi watakuwa kutokana na *infrustructure* ya Kenya ilivyo kwamba wengi watateremkia Nairobi na Mombasa huku waingie tu mara moja halafu warudi. Mhe. Spika, ni kwamba tuone kuwa jambo hili linaweza likaathiri sekta ya utalii au tumejiandaa vipi kukabiliana na tatizo hili. Hilo Mhe. Spika, ni jambo jengine ambalo nilikuwa nataka nielimishwe zaidi.

Mhe. Spika nije katika suala la uwekezaji. Mhe. Spika, katika suala hili wenzangu wamezungumza sana, lakini kitu kinachonitia mashaka ni hizi fursa za wawekezaji kwa wazalendo. Mhe. Spika, wazalendo wapo wachache Zanzibar waliowekeza, tumeyaona mahoteli yao mengine yapo makubwa, lakini sio ya viwango kama vile vya wageni. Mhe. Spika, ukichukua hii Sekta ya Utalii hasa kwa wawekezaji wa nje ni wengi zaidi kuliko wa ndani, na kwa nini ukijiuliza wazalendo wanashindwa kuekeza.

Mhe. Spika, kwanza elimu tunakosa elimu katika mambo haya ya biashara, la pili ni mabenki kwamba riba zinakuwa kubwa sana, halafu hapajakuwa na benki mahsusi za rasilimali kwa ajili ya kuwasaidia wazalendo. Mhe. Spika, wenzetu Bara nasikia wanataka kuanzisha Benki ya Kilimo ili kuihamasisha hasa ile sera yao ya Kilimo Kwanza. Mhe. Spika, benki kama hii wenzetu wakianzisha kweli Kilimo Kwanza kitapata kasi, kwa Zanzibar mimi naona wawekezaji wazalendo bado utaendelea kuwa mgumu kama hatujafikiria kuanzisha mabenki au taratibu hata mabenki yaliyopo sasa yakaweza kuwasaidia wazalendo kuekeza. Mhe. Spika, licha ya mabenki hata sera zetu za uwekezaji pia kama hatujaziandaa vizuri ikawa zina masharti ya kuwashirikisha wazalendo katika uwekezaji nalo hilo ni tatizo.

Mhe. Spika, mimi bahati nzuri ni mwalimu na napenda kudadisi, unajua siku moja niko katika kutembea tembea Saudia nilipita maduka mengi sijamkuta hata Msaudia mmoja kuuza duka, kila ninayemuuliza mimi natoka Yemen, nilikuwa Dar es Salaam, Nairobi lakini kumbe yale maduka wakenda kuekeza wana *conditions* hawakupi leseni lazima umpate mzalendo mshirikiane hata kama hana mtaji lakini ule uzalendo wake ndio mtaji wake. Kwa hivyo, wale wazalendo wao wanawabeba hawa wawekezaji ndio wanapata leseni. Kwa hivyo, wanakuwa wanapata malipo ya afadhali kutokana na ule uzalendo wao,

na hawawezi hawa wawekezaji kuwachezea rafu hawa kwa sababu ukimchezea rafu hukumlipa basi nae anakugeuka unanyanganywa leseni.

Mhe. Spika, ndio nasema mara nyengine wawekezaji hata huwezi kuwapa pesa wakawekeza lakini unaweka masharti kwa wale wawekezaji wanaokuja wale wazalendo nao wakafaidika. Hili na mimi nataka niungane na wenzangu kwamba uwekezaji kwa wazalendo kwetu kidogo una matatizo itakuwa tunabakia na ule ule uwekezaji mdogo mdogo tu.

Mhe. Spika, jengine nataka niulize nimeona kitu kidogo katika vile viambatisho nafikiri Nam. 6 kuna kitu kinaitwa tunuku ya David Living Stone kumeanzishwa hii tunuku ya Dr. Living Stone ili kuwa kivutio kwa hawa wenzetu wanaofanya biashara za utalii. Mhe. Spika, kwa nini tunuku hii tukaipa jina la Dr. David Living Stone na tusitafute kiongozi wetu maarufu mmoja nchini badala ya huyu David Living Stone, labda kuna sababu ipi ya kuifanya hivyo. Mimi nilikuwa nafikiria labda kama tungeipa jina la kiongozi wetu mashuhuri katika Tanzania au Afrika nadhani ingekuwa ni jambo jema zaidi kuliko kurejea kule kule katika ukoloni mambo leo kuipa jina la Dr. David Living Stone, kama kuna sababu za kibiashara pengine tungeita jina la Mandela au Nyerere au Karume pengine ingeharibu, hapo naweza nikaridhika.

Mhe. Spika, mwisho nataka nimalizie katika suala la changamoto. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 25 Mhe. Waziri ametaja changamoto zinazokabili suala la utalii, na changamoto aliyoitaja kwanza ni kutolewa kwa huduma zisizoridhisha watalii, wageni, wazalendo katika Uwanja wa Ndege na Bandari. Halafu ametaja mazingira yasiyoridhisha ya uchafu katika Mji Mkongwe, halafu ukosefu wa vyombo vya usafiri kwa ufuatiliaji wa shughuli za kitalii la mwisho kuna moja inasema vikwazo vya njiani na usumbufu wa Jeshi la Polisi kudai hongo kwa magari ya kitalii.

Mhe. Spika, mimi nataka nimalizie hapo tu kwamba huu utalii inaonesha wazi wazi kwamba ni Sekta MTAMBUKA unahitaji mashirikiano na sekta nyengine. Je, Mhe. Waziri kashirikiana vipi na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuondoa hii kero ya Uwanja wa Ndege na Bandarini? Pia Mhe. Waziri kashirikiana vipi na Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kuondoa kero ya uchafu katika huu Mji Mkongwe? Mhe. Waziri kashirikiana vipi na Afisi ya Waziri Kiongozi ambayo hapa ndio inayohusika na Polisi kuondoa hii aibu ya askari kuomba omba watalii wanaotembea katika magari. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi asubuhi hii kuwa mtu wa pili ili niweze kuzungumza angalau machache.

Mhe. Spika, mengi na mazuri yameshatangulizwa, lakini kwa namna nyengine kuna umuhimu wa kuyakokoteza.

Mhe. Spika, hapa tunazungumzia Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, biashara jana tumepata darasa, lakini mimi nataka niseme machache juu ya hilo. Mhe. Spika, bado nina imani kwamba zao la karafuu ni muhimili wa uchumi wa visiwa vyetu. Mhe. Spika, ni kawaida duniani kote biashara ni kupanda na kushuka hata haya mafuta ambayo yanaongoza duniani kwa umuhimu wake kuna wakati bei inashuka na kuna wakati bei inapanda. Namna ya zao hili linavyotusaidia kwa uchumi wetu tumelidharau kiasi kwamba sasa tunasema hata maharage ni bora inawezekana lakini ni ukweli wa hili naona bado.

Mhe. Spika, mwenzangu jana alisema kuongeza kwa miche ya mikarafuu si ufumbuzi wa kuongeza mazao, miche hii inatolewa, inapandwa lakini ni nani anahakikisha tunapanda miche mia moja na inabaki mingapi, mingapi inakufa na mingapi inaendelea, hilo halifanyiki. Sasa kama tutaendelea kila siku kupanda lakini kinachobaki mashambani hatukijui matokeo yake tunayaona kwenye mazao yenyewe uzalishaji unashuka ilhali miche mwaka hadi mwaka tunaendelea kupanda. Nadhani hapa kunahitajika namna ya wizara hii ama serikali kukaa chini kutafuta kuna nini.

Mhe. Spika, tunaisema Zanzibar bado ni *Spice Island* kwa namna ninavyoifahamu hali halisi tuliyonayo tunatumia hili jina lakini ukweli huo haupo, haupo juzi tulipokuwa tunazungumzia Wizara ya Kilimo tuliliona hili, miti ya matunda, miti ya viungo hakuna chochote kilichoko kwenye vituo vyetu vya kilimo. Mhe. Spika, tumebaki na ile miti ya pale Kizimbani ndio hiyo tunayoringia lakini *spice* sasa hivi zinatoka India zinakuja hapa, huo ni mtihani. Mhe. Spika, ni kwamba hatujaweza kuzitumia rasilimali zetu kwa maslahi ya watu wetu, bado iko haja ya kukaa chini kulifikiria hili *Spice Island* iwe ni kweli atakapokuja mgeni aondoke na hiyo sifa.

Mhe. Spika, hili nakwenda sambamba na dhana nzima ya utalii, utalii hatujafaidika sana kama ambavyo ingepaswa tufaidike. Mhe. Spika, hili litasemwa kwa sababu hatuna ndege katika shirika letu la kuwachukua hawa na kuwaleta, hilo nalikubali hatujafikia hapo. Lakini kuna rasilimali nyengine ambazo hizo ni mali yetu na zipo hapa hapa gharama ni ndogo tunaohitaji kugharimika ili tuweze kuzitumia rasilimali hizo kwa faida kubwa.

Mhe. Spika, kilimo chetu bado hatujajipanga ili chende sambamba na utalii tunaohitaji, tunaagiza vyakula vingi kutoka nje ya Zanzibar ilihali vyakula hivyo tunaweza kuvizalisha hapa kwetu. Lakini sasa ili wakulima wetu waweze kufaidika na soko la kitalii ni kwamba mahoteli haya tuliyonayo tujipangeni

kwenye kilimo. Mhe. Spika, haitapendeza kwamba kila siku tusimame tukiimba nyimbo hii lakini angalau tumeanza wapi katika hili, hapana.

Mhe. Spika, jengine katika hili hili la utalii juzi juzi hapa tuna Chuo cha Utalii wenzetu wametusaidia mambo yetu tunayajua wenyewe lakini tumeshasaidia vyombo tumepata kwa hiyo kule jikoni kwetu mambo ni mazuri angalau lakini pakuviweka vyombo hivi hatuna. Mhe. Spika, ikinyesha mvua vyombo hivi vinaharibika kwa mvua, jua likiwaka linapiga hapo Mhe. Spika, hata wale waliotusaidia kwamba wenyewe sisi wametusikia kelele zetu kwama Sekta ya Utalii sasa tunaitegemea wakaja wakaiona hali ile hapa namuomba Mhe. Waziri atusaidie ni lini hasa mtaweza angalau kutanua pale mahali tukapata mahali pazuri pakuweka vitu vyetu.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kwamba tuna tatizo gumu linalotusibu upande wa uwekezaji *ZIPA* kwenye kitabu amesema Mhe. Waziri kuna huduma kwa wawekezaji hutolewa kwa mashirikiano na taasisi nyengine nyingi za serikali. Mhe. Spika, taasisi hizi ni Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi nyengine ni za Serikali ya Muungano.

Mhe. Spika, dhana hii tulisema ili mafanikio yapatikane ni kuwa na *one stop centre* hiyo imekuwa ni ndoto. Mhe. Spika, nina barua hapa za Kamishna Jenerali Migration, nina barua ya Meneja wetu. Mhe. Spika, kuna mtaalamu ni shemeji yetu ameomba kibali aishi hapa atusaidie pale Amani kwenye viwanda vyetu ndugu yetu huyu wa Uhamiaji hataki kumpa *permit.* Mhe. Spika, huyu ni mtaalamu ingetusaidia kwa wafanyakazi wengine wazalendo pale kuwepo kwake tungepata mawili au matatu kwa wakati mmoja, pia ana utaalamu tunauhitaji.

Mhe. Spika, huyu mtu wa Uhamiaji jibu sitaki maana yake nini, na kweli baada ya sitaki imekuwa ni basi. Mimi hapa nashindwa kufahamu hivi yeye akishasema ndio kasema Mhe. Waziri hebu naomba utusaidie na hili ni hatua zipi za ziada kama Serikali ya Zanzibar huyu mtu anatukorofisha tena kwa makusudi, mimi sijaridhika na majibu haya humu sijui Mhe. Waziri mwenyewe kwa sababu ndio wako naye huko pengine ana la ziada kuliambia Baraza hili.

Mhe. Spika, hali kama hii inadhoofisha mtu mmoja kudhoofisha mtiririko mzima wa ile dhana inakuwa inauma. Mhe. Spika, wenzetu wengine mara unapoolewa katika nchi nyengine wewe tayari umeshakuwa ni raia wa nchi hiyo. Mhe. Spika, wale wazungu wanaitizama thamani tu ama wamepata mkwe ama wamepata shemeji basi wanakupa uraia. Mhe. Spika, hivi kwa nini kwetu sisi liwe gumu kiasi gani na faida ni tatu kwa pahali pamoja. Mhe. Spika, hapa kuna namna sio bure.

Mhe. Spika, jengine ni Maeneo Huru dhana hii ni ya miaka sasa tunakwenda Maeneo Huru angalau tungeanza tukasema miundombinu ya barabara na miundombinu hii si ya Waziri tu wa Biashara hawezi tumeseme ni lazima taasisi zote zishiriki katika jambo hili ni vita vya uchumi. Barabara ingekuwa nambari moja katika hili angalau wale tunaowaita waje wawekeze wangeona kuna kitu hapa na watu wameelekea huku, tukasema tuanze na moja katika haya matano.

Tokea tulitangaze hili leo tungekuwa tumefika mahali, lakini matokeo yake pa kutembea wewe kwa miguu Mhe. Spika, ukiterereka uko ndani ya shimo, barabara yenyewe ile ya kwendea huko maeneo huru, gari hazipishani. Lakini cha ajabu haya yote yanatendeka Halmashauri zipo, Serikali za Wilaya zipo, hii kazi inakuwa ni ngumu. Kwa sababu kama tutaendelea kumuachia mwenyewe Mhe. Waziri peke yake na ende, arudi, tutaendelea kumlaumu hakai, lakini hata akikaa atafanya nini, pesa anazopewa ndio hizi, wengine tunashuhudia tu ni mashahidi.

Mhe. Spika, nadhani tungejipanga, katika hicho hicho kidogo akaambiwa mtu wa mawasiliano ngwe yako wewe ni hii mpaka hapa, mtu wa ardhi na yeye akapewa yake, na wa umeme na mambo mengine. Lakini hivi tulivyo tutaendelea na nyimbo mpaka *christmas* zote zitakuja zikimalizika sisi hatufiki.

Jengine katika suala la uchumi Mhe. Spika. Uchumi leo duniani ni mtihani na sisi rasilimali yetu kuu ambayo haya kwenye utalii ni bahari hii tuliyonayo Mwenyezi Mungu katupa sisi, ni vipi tunaitumia katika maslahi ya nchi yetu hii? Tusiwe na kigugumizi. Mhe. Spika, mimi nashangaa sana na kuona kwamba hata suala la uvuvi wa bahari kuu, sawa tumekubali kwamba kuna mamlaka ya pamoja na wenzetu.

Ukizitizama asilimia zilivyogawiwa inakuja kwamba tunajikaza Zanzibar mara hii tuna asilimia 40, *a reality* sio 40, asilimia 50 zinaendesha mamlaka hesabu takatifu naikubali zimebaki 50, haya zijaaliwe hivyo zinavyojaaliwa kwamba ni mia moja, sitini zinaambiwa za Tanganyika imezaliwa lini na hii haipo? Arubaini ndio tunabaki nazo. Hivi kukiwa na maslahi huzuka akasimama anadai ziwa, hakuna anajitia ndani ya tumbo la mama yake Muungano, huu ni mtihani Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Abdalla Tamim: Ahsante Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima. Pili nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji. Tatu nampongeza Mhe. Waziri pamoja na wafanyakazi wote kwa juhudi zao wanazochukua katika wizara yake.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu kwanza naipongeza hotuba hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, mchango wangu nianzie kwenye utalii. Mhe. Spika, utalii Mwenyezi Mungu katika kitabu chake kitukufu cha Quran ameutaja, lakini nafikiri hatujui ameutaja vipi. Kwa sababu Mwenyezi Mungu kasema katika Quran kwamba, someni na nendeni hadi Uchina, yaani tutafute elimu mpaka Uchina, ile ina maana mimi ninavyoona. Nafikiri ile someni mpaka Uchina hakukusudia kama hakuna nchi nyengine ya kutafuta elimu, mimi naona hapa katumia hekima zake tu, kwamba tutoke yaani tutembee, tutembeleane tuone mambo na tushirikiane.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niseme kwamba, nilibahatika kwenda nje kidogo kutoa tongo za macho. Kikwetu tunasema kutoa tongo za macho, nisije nikasema nimekwenda kutembea nikaambiwa najisifu.

Mhe. Spika, kuna siku nilikwenda China pamoja na wenzangu, kusema kweli nilishangaa. Kwa sababu kule China asilimia kubwa ya watu wa kule sio Waisilamu. Lakini nilishangaa tulipokuwa tunatafuta sehemu ya kula tukaambiwa kuna hoteli ile pale ya Waarabu na chakula chao cha Kiarabu.

Mhe. Spika, tulipoingia ndani ya hoteli ile tulishangaa, tulikuta wafanyakazi wake wanawake wamejistiri tena Wachina sio Warabu. Sasa mimi pale nikaanza kutafuta umbea, nikasema tumeambiwa China asilimia kubwa ya watu wao sio Waisilamu, lakini tukaambiwa hoteli ile inaendeshwa Kiisilamu kuanzia chakula na kila kitu. Sasa nikawa najiuliza kwa nini tusiweze kuiga mambo kama yale.

Kwa sababu sisi Zanzibar tukitaka tusitake asilimia kubwa ni Waisilamu, kweli serikali haina dini, lakini watu wake wana dini na dini yenyewe ni ya Kiisilamu. Sasa kwa nini tusiweze sisi kufanya mambo kama wanayofanya wenzetu ambapo wao hawana ule Uisilamu mkubwa ni asilimia chache tu? Lakini wameweza kujistiri katika baadhi ya mahoteli, nadhani hata mambo ya pombe itakuwa hamna mle, sina hakika lakini.

Sasa Mhe. Waziri wewe unatembelea nchi nyingi mwenzetu, naomba kukuuliza kwamba, katika hizi nchi zetu za Kiarabu naona kuna utalii, wenzetu wanauendesha vipi utalii huu? Naomba nipatiwe majibu. Kwa sababu naona wenzetu serikali yao wanaendesha kidini, lakini nina imani kuna mambo mengine hawaendeshi kidini. Kwa sababu kuna nchi nyengine za Kiarabu lakini mbona hakuna hukumu za kuuwa. Nina imani kuwa si mambo yote kuwa wanafuata dini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa nini na sisi tusisome kwa wenzetu hasa nchi za Kiislamu tukafuata ule utalii wao.

Kwa mfano, hapa watalii wakija si lazima kuwa wajistiri mwili mzima kuanzia juu mpaka chini, lakini angalau wajisitiri kidogo tu japokuwa kichwani. Kwa sababu hatujaweka sheria hiyo. Hakuna sheria katika nchi yetu ya kumtaka mtu lazima ajistiri, lakini angalau kuwe na heshima iondokane na zana kuwa kazi za mahotelini ni za kihuni.

Mhe. Spika, sisemi uongo, mimi mwenyewe binafsi nilifikiri hii kazi ya hoteli kwa wanawake ni ya kihuni na nina imani kuna silimia kubwa ya wazazi hapa Zanzibar wana imani kama yangu mimi. Ndio maana hapa tunasema ajira jamani zinakwenda kwa watu wa nje, sijui Wakenya, Tanzania Bara, si kweli. Sisi wenyewe wazazi hatuwaruhusu watoto wetu kwenda kufanya kazi za mahoteli tunahofia kuwa kuna kazi za kihuni, unahisi mwanao pengine akienda kule atashawishika na wageni atafanya vitendo visivyokuwa vya maana.

Lakini tukifanya utaratibu kama huu wa wenzetu itakuwa vizuri. Kwani binadamu tumeambiwa kuiga mambo mazuri si dhambi, ila kuiga mambo mabaya ndio dhambi. Sasa namuomba Mhe. Waziri anieleze kuwa utalii wenzetu wa nchi za Kiarabu wanauendesha vipi?

Nikiendelea nije katika uwekezaji. Mhe. Spika, Mheshimiwa aliyekaa sasa hivi wa Upande wa Upinzani amesema kuwa tunashindwa sisi wazalendo kuwekeza hapa kwetu. Mimi nakataa, nasema kwamba serikali bado haijawa tayari kuwasaidia wazalendo kuwekeza hapa katika kisiwa chetu. Naamini serikali itapokuwa tayari kuwasaidia wazalendo na kuwapunguzia masharti magumu wanaweza kuwekeza.

Mhe. Spika, tunakwenda katika *super market* huko tunaona choyo, kila matunda yanahifadhiwa mpaka madoriani, *juice* za machungwa, za ndimu kwa sababu matunda mengi yanahifadhiwa ndani ya ma-*packet*. Nashangaa unakwensa *super market* unakuta mahindi katika nyama, mambo madogo madogo wewe unadharau, lakini wenzetu wanafanyia kazi. Sasa Mhe. Waziri nilikuwa naomba tuwasaidie hawa wafanyabiashara wazalendo kwa kuwapunguzia masharti magumu.

Halafu pia naomba wafanyabiashara wetu wa ndani tusijaribu kuiga biashara, ukimuona mwenzako kafanya hili na wewe unafanya hili, kwa nini hatubadiliki. Kama mwenzako kajenga skuli wewe jenga hospitali, mwenzako kajenga hospitali wewe jenga kituo cha kuuzia mafuta, mwenzako kajenga kituo cha mafuta wewe unafanya mambo mengine. Lakini sasa tuna utamaduni ukiona mwenzako kafanya hili basi na wewe unafanya hilo hilo. Kweli tunatakiwa tuwe na choyo cha maendeleo, lakini sio maendeleo kama haya, ukiona mwenzako kafanya hili wewe wekeza katika viwanda.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hebu tuwasaidie hawa wafanyabiashara wetu, tuwaombe na tuwasaidie. Kwa sababu kuwaomba kwenyewe na kuwasaidia kibenki, wawekeze katika viwanda vidogo vidogo kama hivi kufanya *juice* za matunda kwenye makopo.

Mhe. Spika, juzi nimekwenda sokoni kuanzia pale mlango tu uwanja mzima machungwa yamejaa kama uchafu, yamejaa tele. Machungwa yale sijui kama yote yanaliwa, najua mengine yanaoza. Sasa Mhe. Waziri tungekuwa na viwanda vyetu vidogo vidogo hawa wakulima wangefaidika na watoto wetu wangepata ajira. Kwa hilo Mhe. Waziri nakuomba muwasaidie wawekezaji wazalendo wa hapa kwetu.

Mhe. Spika, jengine naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kule Bara wenzetu nimewahi kuwasikia wajasiriamali wanawake wanawezeshwa. Kwa mfano, kama kuna mikutano mikubwa nje ya nchi huko wanakwenda kufanya biashara kubwa kubwa huko kama kuuza vitenge, kanga, mabatiki. Wao wenyewe wanao mfuko wao lakini pia wanawezeshwa na serikali, tena utakuta wafanyabiashara wa kule wa hivi vitenge lakini matajiri. Sasa Mhe. Waziri nataka kuuliza, kwani na sisi wanawake au wanaume lakini sana nasema wanawake, wenzetu wanawezeshwa na serikali kwa kwendwa nje kukiwa na mikutano mikubwa mikubwa na kupeleka biashara, sasa kwa nini na sisi tusiwasaidie wanawake wenzetu wa hapa.

Mhe. Spika, kwa mchango wangu huu sina zaidi, ila naipongeza tena hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia machache tu katika hotuba hii ya Mhe. Waziri. Awali ya yote nami nataka nimsifie kwa hotuba ambayo ni fupi lakini kwa kadiri ninavyojua si mambo mengi aliyoyaweka humu. Sasa kwa sababu hiyo, mimi naona niende moja kwa moja kwa yale ambayo hayamo katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, jana asubuhi nilikutana na vijana wanaoitwa wasambazaji vyakula mahotelini, wakaniuliza Hotuba ya Wizara ya Biashara tayari? Nikawaambia bado inategemewa kuwa leo ili jana. Kwani kuna nini? Wakanipa huo mkasa. Kuna vijana wengi tu ambao ni wajasiriamali wamejiajiri wenyewe na wanasambaza vyakula ikiwemo samaki, mboga mboga kwenye mahoteli haya makubwa ya kitalii. Lakini kuna mahoteli mengine wanakwenda vizuri, wanapeleka baada ya mwezi wanalipwa, lakini kuna hoteli hii ambayo waliiandikia barua inaitwa *Venta Club* ilioko Kiwengwa.

Mhe. Spika, kwa sababu nakla ya barua walinipa na barua hii ilinakiliwa ilikuwa inakwenda kwa Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja lakini imenakiliwa kwa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, Mkuu wa Mkoa Idara ya Usalama, Kamisheni ya Utalii, Waziri Kiongozi, Idara ya Uhamiaji, Kitengo cha Uwekezaji *ZIPA.* Vijana hawa kwa mujibu wa barua hii wanasema, wanaidai Hoteli ya *Venta Club* zaidi ya shilingi milioni mia tatu, ndivyo ilivyoandikwa humu. Na wasi wasi zaidi ni kwamba meneja ameondoka sasa ni miezi miwili imekwishapita ambaye ndiye mwenye kuidhinisha sisi kulipwa na kuna ripoti kwamba, huenda kampuni ya *Venta Club* ikawa imefilisika kwa kuuza hoteli zao zote duniani na kubaki ya Zanzibar. Kwa hviyo, tunaomba msaada wenu hawa viongozi walionakiliwa.

Sasa Mhe. Spika, hawa ni vijana wetu ambao wamejiajiri wenyewe ni katika juhudi za MKUZA, milioni mia tatu na zaidi ni pesa nyingi sana hasa ukiangalia watu wenyewe ni wa biashara za mikononi. Kwa sababu Waziri wa Biashara kanakiliwa mimi naomba atapokuja hapa atueleze kama taarifa hii anayo. Kama anayo amechukua hatua gani, kama hana basi vijana hawa awaite hii nakla ya barua kama hana mimi nitamtolea nimpe ili upatikane ufumbuzi. Kwa sababu kama mwekezaji ana tabia hii kwamba vijana hawa wanaodundukiza dundukiza pesa mbili tatu, deni linafika mpaka zaidi ya shilingi milioni mia tatu hii ni balaa. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili nilipokuwa nasoma kitabu hiki katika ukurasa wa 71 hapa kuna jadweli kiambatisho Nam. 2, hiyo *table* kubwa lakini kuna nambari yaani *serial number,* kuna malengo ya 2009/2010, kuna utekelezaji, kuna na maelezo. Sasa ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano huku mbele naona hakuna nambari lakini nafikiri itakuwa ya saba, ya nane, ya tisa, ya kumi na moja, inaeleza hivi. Katika malengo kuendeleza kutafuta wabia kwa ajili ya kushirikiana nao katika uwekezaji wa maeneo ya Kuji na Vitongoji Kisiwani Pemba.

Kwenye utekelezaji kuna juhudi za kutafuta wabia kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya Vitongoji na Kuji kisiwani Pemba zinaendelea lakini bado hazikafanikiwa.

Mwaka jana kama mtakumbuka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ni kwamba kuna eneo la Kuji lilizungumzwa hapa, lakini jawabu la waziri likawa kwamba, eneo lile na lilikuja tu kwamba kuna mwekezaji ikaelezwa hadithi fupi kdigo lakini ilieleweka. Kuna mwekezaji mzalendo anataka kuwekeza pale lakini kumetokea mambo kiasi ambacho mwekezaji yule mzalendo baada ya kwishapewa barua kwamba anaweza kuwekeza, lakini akazuwiwa kwa mdomo na kwama eneo lile labda kumegunduliwa mafuta. Sasa suala langu liko hapa. Kama sasa hivi katika hotuba ya mwaka huu mambo ni haya, masuala yangu ni

machache tu, kwa nini tusirudi kwa yule mwekezaji mzalendo ambaye ni muhimu zaidi kuliko mwekezaji mgeni.

Kwa sababu hizi ni katika juhudi ya sisi wenyewe hapa kuwekeza, kwa hivyo manufaa na uajiri na mambo mengine yote yanabaki hapa. Sasa ilivyokuwa mwekezaji mwenyewe alishatoa hata mambo yote yale ya mikataba na hivi na hivi alishakamilisha. Sasa Mhe. Spika, kwa idhini yako waziri atapokuja hapa vile vile atuelekeze. Ni kwa nini au juhudi hizi tayari wameshaonana na huyu mwekezaji mzalendo wa awali? Au atueleze hasa ni juhudi zipi zimefikiwa. Kama hawajampata basi wamtafute ili kama atashindwa yeye basi hao wengine ndio waanze kutafutwa. Lakini vyenginevyo kama *decision* imeshatoka kwamba eneo la Kuji na Vitongoji kuwe na uwekezaji basi mimi nafikiri *priority* ya kwanza angepewa huyu mzalendo.

Lakini si hayo tu, kuna taarifa vile vile ambayo sina hakika nayo lakini waziri anaweza akatuhakikishia hapa. Hivyo ni kweli kwamba uwekezaji kwenye visiwa umezuiliwa na serikali. Kwa sababu hii Kuji ni kisiwa hiki, lakini huku kuna taarifa ambayo nasema waziri atakuja kututhibitishia, uwekezaji kwenye visiwa kama Bawe, Kuji, na kwengineko umezuiliwa na serikali?

Mhe. Spika, katika kimbatisho Nam. 1 waziri ametueleza au atueleze hapa kuna utekelezaji wa malengo ya 2009/2010 Idara ya Mipango ya Sera hii iko nambari 2, usimamizi wa ujenzi wa jengo jipya la wizara Pemba, hiyo ni malengo. Lakini utekelezaji ni kwamba wizara imewasilisha taarifa zote muhimu Wizara ya Fedha na Uchumi kuhusu eneo na mahitaji ya fedha za awali ili ujenzi huo uweze kuendelea. Lakini maelezo ni kwamba, mchakato wa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi unaendelea.

Mimi hapa sijaelewa vizuri, hii ni bajeti ya mwaka 2010/2011, hii inayozungumza ni bajeti iliyopita. Sasa naona kama sijaelewa vizuri au kuna *contradiction as a statement*. Mimi kama mjenzi unaposema unaanza *process* ya mchakato wa zabuni maana yake ni kwamba *you have already some money*, lakini huyu katwambia kwamba taarifa ziko Wizara ya Fedha ili kupatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi. Sasa sijui ipi inakuja kwamba na ipi inafuata.

Kama ni bajeti hii ambayo iliishia juzi wamepata kiasi gani. Na huyo *contractor* ambaye anatafutwa saa hizi au mchakato umefika wapi. Kwa ufupi tu waziri angekuja kutueleza katika kadhia hii ya usimamizi wa jengo jipya la wizara hii huko Pemba na mahali ambapo wamefikia.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 57 ambapo kifungu hicho kimeendelea mpaka 58 lakini nasoma kuanzia 57. Huduma kwa wawekezaji zimeendelea kutolewa kwa mashirikiano na taasisi nyengine za serikali kama vile Uhamiaji,

Kamisheni ya Kazi na Idara ya Ardhi na Usajili. Hata hivyo, bado dhana ya kituo kimoja cha uwekezaji (*one stop facilitation centre)* hakijaweza kutekelezwa kwa ukamilifu, jambo ambalo wizara inalifanyia kazi. Sasa hakijaweza kutekelezwa kwa ukamilifu maana yake ni kwamba kuna sehemu tayari imefikiwa, basi waziri aje atueleze. Hii *one stop facilitation centre* tumefikia hatua gani. Na kukamilika kwake hasa ni kupi.

Lakini ukiendelea mbele katika mwaka 2009/2010 jumla ya maombi 310 ya vibali vya kazi na ukaazi yalipokelewa. Kati ya hayo, maombi 207 ni mapya, 103 ni ya kuongeza muda. Maombi 45 ya kuongeza muda yamekataliwa na vibali vyake kufutwa kutokana na sababu ya kumalizika kwa makubaliano ya muda wa ajira ya wageni katika nafasi zilizoombwa. Suala langu kwa Mhe. Waziri Mhe. Spika, ni kwamba hawa wanajua kwama muda wao unamalizika, bilashaka wanajua kwa sababu kuna mikataba, hivyo vibali vimeandikwa ati. Lakini kwa nini wakaomba tena?

Bila shaka ziko sababu pengine kuna vivutio vizuri. Waziri atueleze ni sababu zipi anaziona yeye au zilizoelezwa za kuomba tena hawa ambao wamekataliwa. Kama ni sababu nzuri tu au ni mbaya, labda atueleze ni vigezo gani ili mtu aweze kuomba tena kibali chake kikimalizika kuwe na *criterion* gani aweze kukubaliwa.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kwamba mchango wangu si mkubwa lakini nilitaka niyaeleze haya kwa idhini yako na kwa heshimia na taadhima nakushukuru sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuchangia kidogo bajeti ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutuweka hai, tukawa wazima na tukaweza kupata sauti ya kuzungumza. Pia namshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa usomaji wake wa bajeti na bajeti yenyewe ilivyo.

Lakini Mhe. Spika, nikianza kama ambavyo nasema katika bajeti nyingi ni kwamba bajeti hii ya wizara ni ndogo sana ukilinganisha na malengo na majukumu yake. Sasa asilimia pengine zisingesaidia sana. Kwa sababu asilimia 50 ya shilingi mia mbili ni shilingi mia, lakini asilimia 50 ya shilingi laki mbili ni shilingi laki moja. Kwa hivyo, asilimia isingekuwa ni kigezo kizuri sana kwa sasa cha kuangalia. Kigezo kizuri ingekuwa ni ile keki yenyewe kuiangalia je, imechomwa katika kisufuria cha kibaba, au ni keki iliyochomwa katika *tray* inayochukua chumba kizima.

Kwa hivyo, hii ni wizara iliyokumbatia mambo ya uchumi. Wizara ya Fedha ni wizara inayochukua zile fedha. Ukitazama kama utalii ni sekta kiongozi Mhe. Spika, utaona wizara hii ndio inayotia lile pato la utalii. Biashara tunazoagiza kutoka nje na tunazosafirisha zinatozwa ushuru hapo bandarini unachukuliwa na Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, biashara inachangia katika mapato ya nchi.

Mhe. Spika, ukichukulia ya mwisho uwekezaji, wawekezaji wakija wanataka leseni, wanalipa ushuru katika vitega uchumi vyao. Kwa hivyo, hii ni wizara chumi, sasa wizara chumi hii ikitaka ijipange upya kwa sababu keki ya Zanzibar ni ndogo hatuna cha kugawana ndio tunakuja kupiga kelele nyingi hapa. Mhe. Spika, ukimuuliza hata Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi anakwambia tutakwenda lakini ndio hivyo, tutatazama kidogo kidogo mambo. Ni kwa sababu keki yake ndogo.

Sasa ilivyokuwa keki ndogo tuamini kwamba keki ni ndogo, sio tukae kitako keki ndogo tu, tuangalie vyanzo vipya vya mapato. Sisi tumekaa chini ya mti Mhe. Spika, lakini tunafaidi kivuli tu matunda hatuyafaidi tunawaachia popo wanakuja wakichukua. Mhe. Spika, umepata kusikia maneno hayo, watu waliokaa chini ya mti wakafaidi kivuli cha mti, lakini matunda yanachukuliwa na popo. Mhe. Spika, mti wenyewe una matawi mawili, moja liko mashariki na moja liko magharibi. Upande wa magharibi kuna bahari kubwa ambayo hatofaidi chochote na matunda yake zaidi ya samaki wawili waliowatoa kwenye kishazi. Kwa hivyo, tuko chini ya mti lakini matunda yake hatuyapati.

Mhe. Spika, upande wa mashariki kuna dudu moja linaitwa Muungano, hili linafaidi matunda lakini sisi tuna kazi kubwa. Mhe. Spika, ninao ushahidi wa kusema hayo. Hapa katika mjadala huu huu tuliokuwanao Mhe. Waziri kalitaja moja kwamba Jeshi la Polisi. La pili linatokana na *ZIPA* kwamba Idara ya Uhamiaji inapiga *full stop* kwa wale wataalam ambao wanaomba kupata ajira na kuvisaidia vile viwanda vianzilishi.

Sasa Mhe. Spika, ikiwa hatukuweza kuutazama vizuri kero za Muungano, haya mambo ya biashara na utalii mimi naona ni ndoto. Hapa chanzo chake kikuu hasa Mhe. Spika, ni sisi tulipopoteza Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano akawa ni Rais wa Zanzibar. Kwa sababu ukiwauliza hata wale maprofesa waliokuwa wamebobea kwa mfano Profesa Shivji, atakwambia Zanzibar haina *partner* katika Muungano. Hata akenda Mhe. Shamsi Vuai Nahodha anakwenda tu kwa kuwa kaitwa lakini hana nguvu ya kuzungumza kwa sababu hayumo katika katiba. Tulipokuwa Rais wa Zanzibar ni Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano linapotokezea jambo lolote la kero yeye ana uwezo wa kuzungumza kama ni Rais wa Zanzibar ndani ya Muungano. Mnayataka yachukueni, hamyataki niachie mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi natoa *challenge* akaulizwe Profesa Shivji sasa hivi ndio mwenye katiba hii ya Muungano ameandika kitabu chake kile. Je, Zanzibar ina *partner*? Ndio maana ikawa sisi tumeshalipitisha jambo hapa ukasikia linapelekwa Bungeni kwa sababu Zanzibar bado kutokana na katiba haijawa na *partner* katika Muungano.

Mhe. Spika, kwa mfano mimi nitasema kwamba haya hilo Jeshi la Polisi mmoja hapa alichangia apelekewe Mhe. Waziri Kiongozi. Katika katiba wachilia mbali ya kienyeji enyeji polisi wanawajibika kwa nani? Waziri wa Mambo ya Ndani. Waziri wa Mambo ya Ndani hawajibiki kwa Mhe. Waziri Kiongozi hapa, anawajibika kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hata tukimpelekea Waziri Kiongozi kwamba Jeshi la Polisi linatutalia nini yetu, yeye watazungumza kienyeji tu, lakini hana nguvu za kikatiba za kulizungumza hili jambo. Sasa kama tunataka kweli kuimarisha biashara, kuimarisha utalii na kuimarisha sekta yote ya uwekezaji, tutatue matatizo yaliyomo ndani ya Muungano. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, la pili kama nilivyosema kwamba tutazame tawi la magharibi, tawi la magharibi ni bahari kuu ambayo sisi hatujachuma chochote. Sasa ukitazama uwekezaji wote unaofanywa ni kwenye fukwe, ni lile lile jivuli. Mhe. Spika, utawekezaje kwenye fukwe na bahari inakutazama hapo. Kwa nini kwa muda wa miaka kumi na tano na zaidi sasa hivi tokea ianzishwe haya mambo ya uwekezaji, lakini *ZIPA* haijapata mwekezaji hata mmoja wa bahari kuu na tukaona kwamba angalau tija yake iko hivi. Sasa lazima tubadilishe mwelekeo.

Mhe. Spika, jambo la tatu katika uimarishaji wa sekta ya viwanda suala zima la sera ya nishati lazima wizara hii ishiriki kabisa kabisa katika kutazama sera ya nishati. Kwa sababu hivi sasa kabla ya huo mgogoro ambao juzi ulizungumzwa humu baina ya *ZECO* na *TANESCO*, hivi sasa wenye viwanda katika Afrika Mashariki wanapiga kelele kwamba wanalipa umeme ghali. Hakuna *package* za viwanda, umeme wanalipa kama wanavyolipa watu wengine. Kwa hivyo, bidhaa zetu zinakuwa ni ghali zikizalishwa viwandani.

Mhe. Spika, wawekezaji wakitazama *energy price* ya kuja kuwekeza hapa watakataa hakuna *package*. Sasa lazima hilo liende sambamba na mambo ya uwekezaji. Kwa hivyo, tukisema kwamba papatikane nishati mbadala ni lazima na wizara hii ishiriki kwa sababu inataka kukaribisha wawekezaji, inataka kukaribisha uwekezaji katika viwanda.

Mhe. Spika, jana usiku nilikuwa nikitazama *news*, Morocco wameingia katika upepo *megawatt* 125 *project* moja tu ya upepo. Leo sisi waya wetu wote huo mzima unaotoka huko ni *megawatt* 100, wao mradi mmoja tu wa upepo

megawatt 125. Sasa Mhe. Spika, lazima wizara hii iingie katika mchakato kama ilivyosema kwamba ni wizara mtambuka. Kwa hivyo, lazima iingie pamoja na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, ili kuweza kupata nishati mbadala na kuweza kuwekeza katika viwanda viwe na umeme uliokuwa wa bei nafuu.

Mhe. Spika, matumizi ya ardhi. Moja katika jambo ambalo Zanzibar lina ukosefu ni matumizi ya ardhi. Hata ukenda kwenye Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira sasa hivi ukiwauliza nyinyi ardhi yenu ya kulima iko wapi. Hawakwambii, ooo maana yake tunafanya, sijui vipi. Ndio maana mwengine akachukua muda mrefu. Hivi sasa kuna viwanda viwili kule Pemba vimesita kabisa kwa sababu hawajapewa hatimiliki ya ardhi. Kwa sababu hakujapangwa yale matumizi ya ardhi, inachukua miaka miwili pengine kupata au mitatu zaidi.

Kwa hivyo, wizara hii vile vile ingekaa pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira pamoja na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wakalishughulikia suala la matumizi ya ardhi na hivyo ndio wakaweza kupewa maeneo yao. Wakishapewa maeneo yao hakuna haja tena ya kusema kwamba *One Stop Centre* haitofaa kwa sababu maeneo yao wameshakabidhiwa. Lakini kwa sababu hakuna mpango wa ardhi unakaa *One Stop Centre* haifanyi kazi, anayepelekwa pale katika mjadala hana maamuzi ya ardhi kwa hivyo mambo yote yanasita.

Mhe. Spika, jengine ni suala la utalii na namna linavyotononesha Zanzibar. Si kweli kwamba utalii unaitononesha Zanzibar mimi na-*challenge* kwa sababu hatuna cha kuwapa watalii. Mhe. Spika, ingelikuwa sisi tuna kiwanda cha magodoro, magodoro yote wanayolalia watalii ni yetu sisi, ma-*bed sheet* ni yetu sisi, vikombe, lakini kila kitu kinaagizwa mpaka figili na kabeji. Mhe. Spika, lazima tubadilishe msimamo.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa *strategic grain reserve*. Mhe. Spika, toka siku iliyotajwa hii na kuna mheshimiwa mmoja hapa alikuwa *champion* wa kuitaja, lakini toka siku aliyopewa uwaziri hajaitaja tena. Kwa hivyo, mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri, tumefikia wapi katika ile akiba ya nafaka kwa ajili ya siku za dhiki. Wakati wowote mchele unaweza ukashtuka duniani, lakini tumejisahau madhali uko mwingi hakuna ule mpango wa kuweka akiba ya nafaka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawaomba wale ambao wanapata uwaziri wakiingia ndani yale mambo ambayo tulikuwa tunazungumza hapa wayakumbushe huko katika *cabinet*. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa nimeshughulika kuandika sijui kumeingia kitu kipya gani hapa. Lakini nadhani ni utaratibu wa kawaida wa kupongeza hotuba na mengineyo.

Kwanza kabla ya kumkaribisha Mhe. Ame Ussi Juma, tumezungumza na Mhe. Waziri kwamba atakuwa yuko tayari kuweza kufanya majumuisho hivi asubuhi. Ukiangalia michango tayari inaanza kujirudia na wachangiaji hawa nilionao hapa nafikiri wanatosha ambao tunaweza tukamalizia kwenye saa tano na nusu na baada ya hapo basi Mhe. Waziri aweze kufanya majumuisho. Kwa hiyo, sasa tuendelee kwa kusikia michango, lakini wakati huo huo leo Waheshimiwa Wajumbe walioko nje basi waanze kujitayarisha kuingia ndani ya ukumbi.

Mhe. Ame Ussi Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa asubuhi ya leo na mimi kupata fursa hii ya kuweza kuzungumza. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, pili nakushukuru wewe binafsi. Lakini Mhe. Spika, kilichoingia ni kwamba anakumbusha George Saitoti apeleke hizo taarifa za mchele ambao hakuna. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kuanzia Katibu Mkuu kwenda chini, kwa juhudi zao ambazo wamezifanya katika kukaa na kutafakari masuala ya wizara yao nzima.

Mhe. Spika, kitabu hichi kwa kweli mimi sitakuwa na mengi ya kueleza kama ulivyosema kwamba kuna wengi wamezungumza na yanaweza kujirejea rejea. Lakini mimi nilitaka nizungumze tu na mimi kidogo ili nitoe yangu niliyonayo.

Mhe. Spika, kitabu hichi kimeeleza malengo ya mwaka 2010/2011. Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo. “Katika mwaka wa fedha 2010/2011 idara imejipangia kufanya mapitio ya sera ya viwanda na sera ya biashara”.

Mhe. Spika, hizo ni taratibu nzuri ambazo tayari wizara imejiwekea. Lakini na mimi kwanza nilikuwa na ya kuzungumza kidogo kwa upande mwengine ili kusaidia zaidi ya wale wafanyabiashara wetu wadogo wadogo kwa ajili ya kupata ufanisi zaidi wa kipato. Hili nalo lingeangaliwa zaidi kwa kina kwa gharama nafuu wakapata wale wafanyabiashara ambao wanawekeza.

Mhe. Spika, jengine ni kuwashajiisha hawa wafanyakazi wa sekta binafsi kushirikiana na kuendeleza zaidi zile biashara zao. Mhe. Spika, lakini pia hoja yangu iko hapa. Je, serikali itasimamia vizuri kwa kipindi hichi kijacho cha 2010/2011 hasa ukizingatia kwamba sekta binafsi zilete mafanikio.

Mhe. Spika, ikileta mafanikio kwa sekta binafsi nafikiri ndio tutakuwa tunapiga hatua sana katika serikali yetu na kuwakomboa wale ambao kipato chao ni cha chini kwenye biashara. Kwa sababu Mhe. Spika, biashara si ya matunda tu, kuna biashara chungu nzima ambazo zinaweza zikamletea tija mfanyabiashara au mwananchi kuweza kujiinua kimaisha.

Mhe. Spika, jengine sekta ya viwanda. Tuliambiwa kwamba viwanda vidogo vidogo tunavyo lakini uzalishaji wake pia nao ni mdogo. Sasa Mhe. Spika, nafikiri wizara ingejipanga zaidi ikaona kwamba inatumia njia gani za kuwezesha hivi viwanda ambavyo vinazalisha kidogo kidogo vikaweza kuzalisha kwa wingi pia vikapata maelekezo ya kutosha kutoka serikalini. Kwa sababu wengine wanavyo viwanda lakini mawazo wanajua kwamba ni kuzalisha tu kesho kimesimama.

Mhe. Spika, mtu utasikia ana kiwanda cha sabuni matokeo yake kiwanda kile hakifiki kipindi kimekufa kwa sababu hakina malighafi. Kwa hivyo, hivi navyo ingeonekana kwamba suala hili ipo haja ya kuongeza ufanisi zaidi na kuelezwa hawa wajasiri amali kuweza kuviendesha. Pia wakapewa mitaji kwa kusaidiwa, wameshazungumza wenzangu hapa kwa hivyo na mimi nitataka niongezee tu kwa hilo.

Mhe. Spika, jengine imezungumzwa kwamba kuna utekelezaji halisia ambao serikali yenyewe imejipanga kama inavyoonesha kwenye kitabu hichi namba 6.36 Utekelezaji Halisia naomba kunukuu: Inasema “Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:” Sasa nafikiri kuna mambo kama kumi na moja hapa ambayo yametajwa, lakini kati ya hayo kuna manne ambayo zaidi ndio yamefanikiwa. Mhe. Spika, ningeona na haya ambayo hayakufanikiwa vizuri kiutekelezaji basi nafikiri kuna haja yakapewa msisitizo kwa kusimamiwa vizuri ili kufanikisha yale malengo ambayo serikali imejipangia.

Mhe. Spika, hili nafikiri kwa wizara linawezekana kwa sababu kuna watendaji kamili, kuna watu ambao wenye fani zao, waziri mwenyewe ana uwezo huo ameshazunguka sana kuona zile nchi nyengine ambazo zinaweza zikazalisha kwa kupitia mitaji hii. Mhe. Spika, kwa sababu wanasema mwanamke akiwezeshwa anaweza, Mhe. Waziri ameshawezeshwa alikuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kaja Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kapewa sasa kazi sio kuwezeshwa tena, kapewa ile kazi ambayo sasa aifanye. Yeye amepewa na timu yake nyuma wakae wajipange waone sasa vipi tunajikwamua katika serikali yetu. Mhe. Spika, ingekuwa hivyo basi nategemea kasoro ndogo ndogo hizi zingekuwa zimeondoka.

Mhe. Spika, niseme pia katika biashara wizara inatafuta wanaoweza wakawekeza kwenye mahoteli na biashara nyengine. Lakini Mhe. Spika, kuna tatizo watu wetu bado watazunguka kwamba hawana ajira. Labda wawekezaji wale na wao wangekuwa wanawekewa mikakati kama nchi nyengine ambazo zinafanya. Kwa sababu mwekezaji akija nchini kunakuwa na taratibu ambazo anaambiwa utafuata moja, mbili, tatu.

Mhe. Spika, kuna nchi ambazo zina wawekezaji kama hawa wanasema hata kwanza unawekeza taratibu zetu watu wetu wote na kama huna chuo basi uanze kusomesha wewe wakimaliza wengine wanapata ajira pale pale na wengine watakuwa wapo katika kusubiri wale ambao wawekezaji wengine labda watakuja. Nafikiri hii nayo itazamwe kuliko vile kuja kuambiwa kwamba mwekezaji anakaa anatoka na mtu Kenya au Uganda anakuja kufanya kazi hapa, wakati kwetu na sisi watu wanataka ajira vile vile. Sasa hili nalo lionekane kama ni jambo muhimu na la kutiliwa maanani.

Mhe. Spika, kitu chengine Mhe. Hamad Masoud Hamad kakizungumza kuhusu huyu mfanyabiashara au mzabuni mwenye kudai mapesa, itabidi nayo lazima nizungumze. Hata jana ametoa taarifa zake kwenye Zenj FM sijui nini anahojiwa, akaeleza kwamba yeye barua alikwenda mpaka kwa Mkuu wa Wilaya jawabu aliyopewa anaambiwa kwamba mimi suala hili siliwezi. Lakini bado mamilioni ya pesa anayadai sasa anasema afanye nini. Mhe. Spika, mimi nasema Mhe. Waziri amsaidie huyu kijana kwa sababu najua kuna orodha za wafanyabiashara wanafahamika na wanalipa vile vile kwa hivyo asaidiwe ili apate chake. Kwa sababu huu ni mwezi wa tatu au zaidi yeye anakwenda tu hana anachokijua.

Mhe. Spika, baada ya hayo, mimi binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Nungwi naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri asilimia mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru Mwenyezi Mungu kukujaalia na mimi ukanipa nafasi ya kuchangia mawili matatu katika bajeti ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Spika, mimi sina mengi sana ni mambo ya jumla jumla tu. Lakini kwanza nianze na karafuu. Tunaambiwa sekta kiongozi ni sekta ya utalii, lakini nathubutu kusema sekta mama ni mkarafuu na karafuu zake. Utalii ni kiongozi lakini karafuu ndio mama. Kwa sababu kwa kawaida binadamu haui mama yake, hata akiua mama yake basi watu hujiuliza mara kumi kumi labda huyo kakosa radhi au labda kapungukiwa na akili. Basi na mimi naamini kwamba Serikali ya Zanzibar kwa sababu karafuu ndio mama yake aliyemzaa toka asili na jadi, ndio mama yake hasa aliyemchukulia mimba akamzaa hatoua mkarafuu.

Lakini kutokuua kwake mkarafuu ni kumuachia mwananchi mwenyewe mwanawe aliyemzaa akashughulika nae. Kwa sababu serikali inaonekana kama kwake ni mzigo tena kubeba kushughulikia hili zao la karafuu. Ndio maana karafuu zinapungua mwaka hadi mwaka. Sisi sote ni mashahidi karafuu zilipopandishwa bei basi wananchi wote wa Pemba pamoja na hapa Unguja wale wenye mikarafuu walikuwa wanaishughulikia katika kiwango cha juu kabisa kwa sababu karafuu zimeongezwa bei. Kwa hivyo, huu mti ulikuwa unashughulikiwa ukapata mazao mazuri.

Lakini Mhe. Spika, kwa ghafla ilipoanguka bei ya karafuu basi na wananchi nao wameiacha. Nafikiri viungo vyengine vyote basi ni ghali kuliko hata karafuu. Kwa sababu tangawizi wakati mwengine ukenda sokoni hapo Darajani kilo moja shilingi 4,000/=, siku moja moja ndio utapata kilo moja shilingi 3,000/= au shilingi3,500/= lakini hasa ni kilo moja shilingi 4,000/= tena ni tangawizi mbichi hiyo ndio utapata kilo Shs.4,000/=. Sasa kwa sababu hiyo mimi ningeiomba serikali ile nia yake nzuri iliyonayo ya kwamba karafuu wawaachie wenyewe wananchi na serikali ishughulikie kutazama wananchi kwamba hawanyang'anywi haki zao zile au kutizama bei, na serikali ikapata pato la kodi yake. kwa hivyo, kila mtu achiwe karafuu kushughulikia mwenyewe na aiuze atakapo.

Mhe. Spika, labda tu hii mikarafuu ingeshughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi ingeweza kupata pesa nyingi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa, kwa sababu wangepata kodi kutokana na hao watu watakaouza karafuu. Watu wasingefanya tena magendo, magendo yangehama na KMKM badala ya kushughulikia magendo ya karafuu basi wangeshughulikia magendo ya kuvua samaki katika bahari yetu kubwa huko na magendo mengine ya watu labda kununua mafuta wakayaingiza nchini bila ya kodi na mambo mengine pia wangeshughulikia ulinzi wa nchi yetu Zanzibar, lakini wasingeshughulika tena na watu wa karafuu.

Mhe. Spika, sasa hivi kwa sababu karafuu iko serikalini, basi KMKM hawana wanalolishughulikia isipokuwa karafuu. Kwa nini iwe karafuu tu ndio lizibitiwe namna hiyo, sasa wakulima wa karafuu wanaona choyo kwa ndugu zao au kaka zao wanaowapenda hapo Tanzania Bara. Korosho zao wenyewe, pamba zao wenyewe na kila kitu chao wenyewe. Kwa nini sisi tukandamizwe na karafuu. Sasa mimi naiomba serikali ile nia yake nzuri waitie basi katika mchakato waendelee nayo ili waone ni namna gani karafuu watawaachia wenyewe wananchi wazishughulikie na wao pato lao serikali watalipata namna gani.

Mhe. Spika, nikitoka hapo Mhe. Spika, niingie kwenye biashara. Wanawake na biashara. Mimi naiomba wizara hii kwa sababu Zanzibar ni visiwa na visiwa tunategemea sana biashara, hatuna ardhi ya kutosha, mkombozi wetu ni biashara pamoja na bahari na mambo mengine madogo madogo. Wanawake wengi sasa hivi wanaonekana wameingia katika biashara, lakini wanafanya biashara kwa kubahatisha, hawajui biashara ni kitu gani. Ni mtu kuwa na pesa zake hapa akazivunjisha akapata dola akaondoka akenda India, akaondoka akenda Dubai na akaondoka kwenda Thailand, akaondoka kwenda China na akaenda Turkey na kwenda nchi mbali mbali. Lakini hajua hasa biashara inavyofanywa, anajua kununua, kule kanunua kwa shilingi ngapi na huku aje auze shilingi ngapi.

Kwa hivyo, wanawake hawa pamoja na vijana wa kiume ambao wanaingia sasa katika biashara wafunzwe, wafanyiwe semina nyingi, wapewa maarifa ya kibiashara na wasaidiwe kiutaalamu. Kwa sababu wizara ya biashara wanao wataalamu na wawasaidiwe kitaalamu hawa, ni namna gani ya kufanya biashara na namna gani ya kuchagua vitu vilivyokuwa vizuri na kuvileta hapa nyumbani, wasichukuwe tu mwadabwada wakatuletea hapa nyumbani.

Kwa mfano sasa hivi ukikuta biashara ya China madukani unaogopa kidogo. Kwa sababu wafanyabiashara wengi wanaonekana wanapokwenda China, wanachukua biashara ile ya *low quality*. Wakati kule China ukitaka hata ya *quality* gani basi utafanyiwa, lakini wao wanachukua biashara za *low quality*. Kwa hivyo, kidogo wafanyabiashara wetu hasa wanawake, waelimishwe ni namna gani ya kufanya biashara bora ili waweze kunyanyuka kibiashara.

Suala jengine Mhe. Spika, ni usafi na mazingira ya hoteli yetu ya Bwawani. Mimi Mhe. Spika, nachukizwa sana nikiliona lile bwawa la maji machafu pale mbele ya hoteli ya Bwawani, kwa hakika nachukizwa sana. Ningeiomba wizara hii kwa kushirikiana na labda Baraza la Manispaa na wengine wanaohusika na kazi hii, sehemu ile ikawekwa katika sehemu ya usafi, kwa sababu sio vizuri watalii wageni kuingia pale kisha wakitizama tu hivi mbele yao wanakuta bwawa la maji machafu. Bwawa lile huzalisha mbu na nzi wengi, pengine wakati mwengine wadudu wabaya. Kwa hivyo, pangefanyiwa utaratibu ili pale pakafanywa kuwa pasafi ili hoteli izidi kuvutia. Kwa sababu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatuna hoteli nyengine mikononi mwetu isipokuwa hoteli ya Bwawani. Kwa hivyo, ile ni kumbukumbu tuliowachiwa na madamu tumeachiwa kitu urathi ni lazima tukitunze na tukienzi ili kiweze kutusaidia sisi na vizazi vijavyo.

Jambo jengine Mhe. Spika, pale hoteli ya Bwawani tuna hili *hall* la salama au Salama *Hall*. Wakati serikali ilipolijenga, ilione ni *hall* kubwa sana kwa wakati ule, lakini hivi sasa *hall* hili limeshakuwa dogo. Hata tukifanya harusi zetu tu

za kawaida ikiwa mtu anataka kwenda Salama, basi kama atalipanga vizuri na ataalika watu kidogo basi hili *hall* linakuwa ni dogo. Wakati mwengine linafanyiwa mikutano ya kimataifa lile *hall*, vile vile linakuwa ni dogo.

Kwa hivyo, naiomba wizara hii kama kuna uwezekano au kama kuna nafasi pale Bwawani basi lile *hall* livutwe kwa urefu na upana ili lizidishwe. Kwa hivyo, kupatikane pesa hapa za kulizidisha lile *hall* na lifanywe liwe zuri na liwe la kimataifa ili hata mikutano yetu ya kimataifa iweze kufanyika pale, kila mtu awe na kipaza sauti chake mbele kama hivi tulivyo na kisikilizio chake na kila kitu chake. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba hili *hall* liwe la kimataifa na mikutano mingine ya kimataifa badala ya kufanyika Arusha basi iweze kufanyika hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 25 kuna suala jengine ambalo limeandikwa hapa kuwa mazingira yasiyoridhisha ya uchafu katika Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni kivutio kikubwa cha watalii, pamoja na kero za mapapasi wanaosumbua wageni wanaotembelea mji wetu. Hii ni kweli. Mimi wakati mwengine ninakuwepo sana Mji Mkongwe, kwa sababu nasema tena, nimekulia huko na niko huko huko mpaka leo Mji Mkongwe. Kweli Mji Mkongwe ni mchafu.

Mhe. Spika, kuna wakati mmoja nilitoa rahi hapa kwamba kwa sababu Mji Mkongwe unajichumia wenyewe kwa sababu wanaingia watalii, basi zile pesa ambazo kidogo zinapatikana labda wapewe makusudi watu wa Manispaa kwa ajili ya kusafiri Mji Mkongwe. Au pafanywe vyenginevyo labda au sijui itakuwa ni kuingilia kazi za watu, kwa sababu kuna wizara mbali mbali. Au watu wa mambo haya ya biashara na utalii basi wawe na watu wao wenyewe wa kuusafisha huu mji, wenye mahoteli, wenye vioski Mji Mkongwe basi wachangie ili wawe na watu wao wa kuweza kuusafisha huu Mji Mkongwe. Watu wa Manispaa waingie pale wakati makaro yanapofufurika kwa sababu hawa wengine watakuwa hawana utaalamu wala hawana zana.

Lakini Mhe. Spika, ni kweli Mji Mkongwe haufyagiwi na hapo hiyo siku unapofyagiwa basi utacheka wewe, mtu anafyagia fyaa fyaa, vikaratasi vya juu, wanaweza kuviona taka pale basi *Wallah Laadhim* anazipita. Kwa hivyo utakuta siku zote Mji Mkongwe ni mchafu.

Mhe. Spika, mimi naomba Mhe. Waziri ashirikiane na watu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, ili waweelimishe tena wakaazi wa Mji Mkongwe turejeshe mila za Mzazibari jamani kila siku nasema. Mzanzibari mila yake akiamka kwanza mbali ya kufyagia ndani lakini lazima afyagie uwanja. Sasa kila mmoja Mji Mkongwe ana mazingira yake ya uwanja hata mbele ya nyumba yake. tunapotoa taka usiku basi wanaziangusha, basi hata pale mbele ya mlango wake

mtu anashindwa kuzoa taka akazitia ndani ya debe, zinaachwa vile vile zilivyoangushwa na paka usiku. Sasa hii ni kuleta sura mbaya katika mji wetu na wageni wetu wanatuona labda sisi ni wachafu, ilhali sio mila zetu. Hizi mila za uchafu zinatokea wapi hasa kwa Wazanzibari.

Vile vile wale wahamizi waliohamia Mji Mkongwe waelimishwe mazingira ya kukaa na Mji Mkongwe, Mji Mkongwe utamaduni wake ni usafi, utamaduni wake ni kunukia sio kunuka. Sasa mimi naomba Mhe. Spika, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ishirikiane na Manispaa pamoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe, ili tuone kwamba Mji Mkongwe unavutia na ni kivutio kitakachotia pesa katika mji wetu.

Halafu jambo jengine ni kuhusu wafanyabiashara wa ndani,

Mhe. Spika: Dakika mbili zimebaki.

Mhe. Najama Khalfan Juma: *Inshaallah*. Waelimishwe vya kutosha ili waweze kuekeza katika viwanda. Vile vile Kiwanda cha Makonyo. Kiwanda cha Makonyo Pemba kinatoa mafuta ya makonyo pamoja na mafuta ya viungo vyengine kama mchaichai, mdalasini, mkaratusi na mengine. Lakini bado hayajatoka kwa wingi mafuta haya. Mimi ningeiomba wizara iwashirikishe na wananchi katika kutoa mafuta haya na baadae wauze kiwandani, au wauze zile *row material* wapeleke pale kiwandani, ili wao waweze kupata pesa lakini na kiwanda kiweze kupata hizi *row material* za kutosha.

Mhe Spika, kuna uhaba wa madarasa huko kwenye Chuo cha Utalii. Mhe. Spika, inasikitisha kuona kwamba watu hawa wanasoma pale *restaurant*. Kwa kweli kuna *hall* pale lilikuwa linataka kujengwa, kwa nini halijengwi basi hili *hall* ili hawa nao wakapata kukaa kwa uzuri na kusoma kwa vizuri katika hilo *hall* litakalojengwa.

Jengine Mhe. Spika, mbio mbio ni kuendelea kutafuta wabia kwa nia ya kushirikiana nao katika uwekezaji wa maeneo ya shirika huko Kuji na Vitongoji kisiwani Pemba. Mnakumbuka lakini kama mlituletea ramani hapa, ya kutuambia kwamba Kuji haitolewi kuna mafuta sijui kuna nini, leo ilikuaje tunaona tena Kuji na Vitongoji. Vitongoji haya tunajua kwamba kuna Mbuyu mkavu na kuna maeneo mengine yatatafutiwa wawekezaji. Lakini hii Kuji mliotuambia haitoki hii kwa sababu kuna mafuta, tena itakuaje mafuta yameshakauka au atapewa tu mwekezaji hivyo hivyo ajenge juu ya mafuta halafu joto limuakie, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo tu mheshimiwa. Namshukuru

Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah mwenye kutuwezesha tukaweza kufika hapa kwa salama. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tunyamaze salama.

Mhe. Spika, kwanza nawapongeza watendaji wote kuanzia waziri, katibu, wakurugenzi na watu wa mashirika pamoja na watendaji wake wote kwa kitabu kizuri na bajeti yao nzuri iliyopangika.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi nitazungumza kidogo tu. Kwanza nitakuja kwenye mikarafuu, lakini Mhe. Spika, nitagusia mambo mbali mbali maana Mhe. Mjumbe aliyemaliza amenifilisi kidogo.

Mhe. Spika, unajua zao la karafuu ni zao ambalo ni uti wa mgogo kwa watu wa Zanzibar. Kwa tunavyolifahamu tokea tunakotokea mpaka tukafika hapa. Mhe. Spika, ilikuwa karafuu ni zao ambalo lilikuwa ni kipaumbele sana.

Mhe. Spika: Tunaotoka nje tusisahau kurudi ili tuje kumaliza kazi zetu.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Halafu Mhe. Spika, watu walikuwa wanachuma karafuu na mapato yakipatikana kwa grade. *Grade* ya kwanza ilikuwa na bei yake, *grade* ya pili ilikuwa na bei yake na hata sisi watoto tulikuwa tukiokota karafuu zile kwa ufanisi na tukaweza kujipatia mapato. Badala ya kwenda juu zao hili basi tunaona kidogo limedidimia hatujui tumekwama wapi.

Mhe. Spika, tunaomba tupate ufanisi mzuri sisi wazalishaji kwa sababu watu wa Pemba wote ndio tuliokuwa tunamiliki mashamba haya ya mikarafuu, lakini bado mikarafuu inatutoka na mazao tunayopata bado ni madogo.

Halafu Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika viwanda vidogo vidogo na vya kati. Mhe. Spika, viwanda vidogo vidogo na vya kati vinataka vishajihishwe ili viweze kufanya kazi zake, bila ya elimu basi watu wanaweza kufanyakazi zao na viwanda vikawa vinaanguka kwa kukosa soko. Wazalishaji hawa pengine katika kuuza mazao yao, je mazao yapi yanayohitajika na yakakidhi haja katika viwanda vile. Pengine mananasi mtu anataka akafanye jam, labda hataki lile nanasi kubwa anataka nanasi dogo. Je, watu wanashajihishwa katika vilimo hivi na kuweza kupata vitu kama vile na kuweza kusindika matunda katika viwanda vyetu.

Mhe. Spika, vile vile kuna kiwanda kidogo kilichofunguliwa kwetu Pemba bado hakikidhi haja kwa mazao ya kwetu, kwa sababu ikiwa ni embe hakiwezi kiwanda kile kikasindika embe iliyoko Pemba kwa juisi, ni lazima litaharibika. Kwa hivyo tunakosa mapato ya taifa na sisi wazalishaji bado moyo wetu

kidogo unatuanguka, kwa sababu kila siku viwanda tuna vihitaji vya kuweza kutengeneza vitu na tupate viwanda ambavyo vitakidhi, tuna mananasi, tuna tungule, maembe na ndimu.

Mhe. Spika, msimu huu ni wa ndimu basi kwa kila mmoja ambaye analo shamba la ndimu, basi Mhe. Spika, madimu yamezagaa hayana vya kufanywa. Kwa hivyo, tunaomba wenye viwanda vidogo vidogo waweze kushajihishwa jinsi ya kuzitumia ndimu kukamua na kupata achari ili kuweza kuuza katika masoko na kuweza kujipatia mahitaji.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije kwenye hizi biashara ndogo ndogo za wanawake. Mhe. Spika, biashara za wanawake wa vijijini ni biashara ndogo ndogo za kilimo. Kwa mfano, watu wanapanda mboga mboga pamoja na vitu vingine, lakini bado soko la kujikwamua wanawake katika shughuli hizi hawana. Utamkuta mama kapanda mchicha wake, lakini hajui akauzie wapi, yule kapanda na mimi nimepanda, mimi nakula wangu lakini wake hana pakuupeleka. Mazao mengine halikadhalika kama tungule na mabilingani na mambo mengine. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Spika, waziri aweze kufanya juhudi ya kutoa semina ili kuweza kushajihisha vikundi na mambo mbali mbali ili wanawake hawa kuweza kujikwamua kwenye uchumi na kupata mahitajio yao ya kila siku.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa ilikuwa nataka niseme kidogo ili kumuunga mkono waziri wangu. Mhe. Spika, na mimi naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia pamoja na wanawake wenzangu. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika. Kama nilivyokuomba sijui hata kama hizo dakika tano zitafika. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa Zanzibar ni nchi ndogo yenye visiwa viwili vya Unguja na Pemba. Nchi hii yenye ongezeko kubwa la idadi ya watu na sehemu ndogo ya ardhi inayoweza kutumika kwa kilimo.

Mhe. Spika, njia pekee ya kujinasua kiuchumi ni kuimarisha na kusafirisha nje ya nchi, na kuzalisha bidhaa mbali mbali za viwanda zenye mahitaji ya lazima na yasiyokuwa ya lazima. Uagizishaji kutoka nje inawezekana ili lengo hili likatuondolea umaskini.

Mhe. Spika, na mimi nije kwenye zao la karafuu kama walivyozungumza wenzangu. Mhe. Spika, serikali iwe makini kuhusu zao la karafuu. Kwa sababu Mhe. Spika, zao la karafuu ambalo ndio zao la asili lakini sasa hivi linatukimbia kwa hali zote. Mikarafuu mingi inatoweka, mingi inakufa na hata

hao wachumaji wanarudi nyuma kuhusu zao hili kutokana na hivyo lilivyoanguka.

Mhe. Spika, nije kwenye viwanda. Tunakumbuka tulikuwa na viwanda vingi hapa Zanzibar. Tulikuwa na kiwanda cha viatu, viwanda vya ngozi, viwanda vya mafuta ya nazi Mwanakwerekwe, kiwanda cha sabuni Mwanakwerekwe na tulikuwa na kiwanda cha sigara. Viwanda vyote hivi sasa havipo wala hatuvioni vimeshatukimbia Mhe. Spika. Kama viwanda hivi tungekuwa navyo mpaka sasa hivi si vingetuongezea mapato zaidi Zanzibar.

Mhe. Spika, nije kwenye uwekezaji. Jana Mhe. Kaimu Waziri Kivuli aligusia kuhusu suala la mwekezaji alioko Kisiwa Panza Chokocho, mwekezaji huyu anaitwa Calous. Mhe. Spika, mwekezaji huyu yupo kwa siku nyingi sana na kwa kweli hatujui kazi yake anayoifanya, yupo tu pale. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atueleze mzungu huyu anafanyakazi gani au anafanya mradi gani. Pia atueleze mapato anayoingiza, yaani ni kiasi gani cha mapato anachoingiza serikalini, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ni kweli hazikutimia dakika tano.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii. Pili nimshukuru Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka niingie katika ukurasa wa 15. Mhe. Spika, inawezekana ukurasa huu umeshachangiwa, lakini na mimi nachangia kwa aina yake. Mhe. Spika, utalii unategemea sana utulivu pamoja na vivutio katika nchi.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa hivi utulivu upo na utalii upo na hakuna sababu au visingizio kwamba utalii umerudi. Lakini Mhe. Spika, utalii siku hizi umekuwa na hila. Naomba hili nachangia ili waziri pamoja na watendaji wake wafuatilie. Mimi ningependa mawaziri wengi wakawa kama Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Mhe. Tafana Kassim Mzee.

Mhe. Spika, Mhe. Tafana Kassim Mzee ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi akisikia kitu basi anakwenda. Kwa sababu ndani ya nchi wako watu wetu, lakini kama sio wetu.

Kwa mfano hivi karibuni kuna tatizo la kwamba kuna mameneja wameondoka na mapesa wamekimbia *supply* hawana pesa, wao wanadai na wao wanadaiwa. Siku zote tunaiambia serikali, ukienda kwa Mkuu wa Wilaya anakuambia

nenda kwa utalii, ukenda utalii anakuambia nenda kwa Mkuu wa Mkoa, ukenda kwa Mkuu wa Mkoa hujulikani uende wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sichangii namna ya utalii wala athari ya utalii, isipokuwa nalichangia hili liko ndani ya eneo letu, kwamba watalii wameondoka na mapesa mengi na sisi tumekaribisha watalii ili wananchi wetu watononoke. Hivyo kuna sababu kwamba kuna mtafaruku wa pesa huko duniani, sasa ndio wawaibie wanyonge. Mhe. Waziri kwa hili uje unipe maelezo na nitakuja kukuambia ni hoteli gani na hoteli gani. lakini suala hili lifuatiliwe mapema sana. Maana yake sasa hivi hawa wawekezaji hawana huruma.

Mhe. Spika, kuna kijana mmoja anaitwa Tela mlemavu wa mguu kakatwa kwa sukari, kajikusuru kusuru akatafuta mfuko wa kujiendeshea maisha yake, basi huyo ndio kabisa kadhulumiwa zaidi ya milioni 12, pesa zake hazipati kwa zaidi ya miezi minane na wako wengine. Kwa hivyo, utalii huuu tunaupenda, tunautaka na tumepewa maeneo kwa madhumuni kwamba wananchi wetu watononoke, sio serikali peke yake. Mhe. Waziri suala hili uje unipe maelezo vizuri. Pia uwasiliane na Wilaya ya Kaskazini ili wakupe maelezo kuwa wamefuatilia kwa kiasi gani suala hili.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka jengine ambalo nataka kulizungumza, limezungumzwa sana, ni kuhusu sekta ya viwanda katika ukurasa wa 48. Mhe. Spika, bado hatuna viwanda, tufanyeni viwanda ili wananchi waondokane na matatizo ya ajira. Kukiwa na viwanda viwili tu, kimoja Unguja na kimoja Pemba basi tatizo la ajira litapungua. Tusiwe na maneno ya kujikanyaga na kupinda pinda, jamani tuwakaribishe wawekezaji wakubwa ili tuwe na viwanda.

Mhe. Spika, kuna siku moja nilikuwa na mjumbe wa kamati ya Fedha na Uchumi, tukenda Dar es Salaam tukaambiwa nyinyi mnakagua nini, tukawaambia tunakagua shughuli za fedha humu nchini. Tukaambiwa nyinyi hamtaki pesa. Kule kwenu kwa nini tukitaja kiwanda mnahangaika sana, huyu anasema sijui ina muhusu huyu na huyu ina muhusu huyu. Tukachukuliwa tukaangalie namna viwanda vinavyokwenda, tukenda kwanza kwenye kiwanda cha kibiriti.

Mhe. Spika, tumeona namna ya kiwanda kinavyotengeneza kibiriti na jinsi kinavyobeba ajira basi wewe mwenyewe utacheka. Watu wamevaa vizuri, roho zao zimetulia na wala hawana shaka maana wanajua kuwa mwisho wa mwezi anapata mshahara wake. Lakini sisi hapa hatuna viwanda, hapa tuna vitu tunajifundisha fundisha tu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukaribisheni viwanda ili tuondokane na tatizo la ajira. Mhe. Spika, ajira serikalini ina masharti makubwa na wala haipatikani. Ukitaka mtoto wako awe askari basi utapata tabu kweli, maana utaambiwa kazidi miaka 23 na akiwa hajafika basi utaambiwa bado kidogo na hata awe ametimia basi utaambiwa nafasi zinatoka kwa Mkuu wa Mkoa, ukenda kwa Mkuu wa Mkoa anakuambia wenyewe ni polisi. Basi inakuwa hakuna ajira, sasa tunarudi nyuma tu, hatuna ajira wala hatuna chochote tupo tu. Mwisho tutafika pahala wenzetu wasituelewe hawa, maana yake sisi tunawategemea wenzetu vijana. Lakini vijana wengi wamekuwa ni wazururaji tu kwa sababu mipango yetu haiendi vizuri. Tunatoa maeneo kwa madhumuni ya uwekezaji, akishapokea eneo mwekezaji basi hakuna chochote.

Mhe. Spika, natoa mfano wa Kiwanda cha Sukari Mahonda. Tokea tulikuwa tunakwenda kukagua na kupata maelezo mpaka tumeingia uvivu hatuendi. Hakuzalishwi tena sukari, utaona moshi hakuna kinachofanywa wala hujui wanachoma nini au wanatengeneza nini. Hebu Waheshimiwa Wajumbe tukiona mkataba unakaribia kwisha basi mwekezaji tumwite, tumwambie unaweza au huwezi ili tutafute wengine, kwa sababu ile mali ni ya Wazanzibari. Kiwanda cha Wazanzibari na ardhi ya miwa ni ya Wazanzibari. Kwa hivyo, lazima tunapoweka mikataba tuone kwamba tunaweka mikataba yenye uhakika.

Mhe. Spika, tumfuate mtu kwao na kujua ile kumbukumbu yale ya biashara anaweza vipi, mtaji anao na anakopa benki gani. Lakini sisi akija na maneno mazuri basi tayari anapewa. Kwa hivyo, naona kwamba bado sekta ya viwanda tunaitania, hatujaweza kuishughulikia haswa. Mhe. Spika, naomba sana tuwakaribishe wawekezaji wakubwa ili tuondokane na matatizo.

Hivi sasa tunaambiwa tunaingia kwenye soko la pamoja. Mhe. Spika, kwa mtizamo wa haraka kama hatutopeleka mwani basi hatuna cha kupeleka katika soko la Afrika ya Mashariki. Sisi hatunusuriki, kwa sababu hatuzalishi na hatuzalishi sio kwamba wale rasilimali watu hatuna tunayo kubwa, elimu wanayo na ujuzi wa wastani wanao, lakini mipango yetu kama serikali hatujaiweka sawa.

Mhe Spika, sina madhumuni ya kwamba naponda kama anavyotumia Mhe. Rashid Seif Suleiman. Eeh! Na yeye huwa anachangia tu. Lakini lazima tuone tunabadilika tusiwe kule kule tuliko na bado hapa tuliko tuko vile vile na tunako kwenda tuwe vile vile. Ni lazima tubadilike.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kuchangia ni kwenye ukurasa wa 36 katika sekta ya biashara. Mhe. Spika, ZSTC ina sifa zana na ina sifa kwa sababu viongozi na watendaji wao wana akili sana. Mhe. Spika, mashirika mengi

yamekufa, lakini bado ZSTC na Shirika la Bandari yanafanya kazi vizuri ni lazima tuyasifu na yanafanyakazi kwa moyo.

Unajua Mhe. Spika, kinachotuumiza hapa Wazanzibari wengi sio waaminifu. Kama sio waaminifu katika shirika basi kazi yoyote haiendi. Kwa hivyo, hawa inavyoonekana ni waaminifu sana. Wanafanyakazi katika afisi zao na kazi zao vizuri na halafu wana ubunifu, maana kujenga majengo wakakodisha na wakawa wanaleta kiwango cha fedha kama kilivyoainishwa basi ni watu wa kupewa sifa sana.

Pia naishukuru serikali kuwa imetambua sasa, nafikiri haiwakopi na ikiwakopa inawalipa. Kwa sababu kipindi cha kati iliteteruka sana ZSTC, mpaka ikapelekea kwamba walitaka kushindwa kununua karafuu. Lakini baahati nzuri sasa hivi wanaweza sijasikia malalamiko. Kwa hivyo, kama wanaweza bado tusimamie kwamba kubinafsisha zao la karafuu bado kwanza liwe kwenye mazungumzo tu, isiwe kwa vitendo. Kwa sababu ni shirika ambalo linaweza kutusaidia sana hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, naona Mhe. Najma Khalfan ananiangalia sana, lakini ni lazima tuseme, tuangalie huku na huko. Kubinafsisha shirika Mhe. Spika, ni hatari kubwa. Yako mashirika ya biashara yaliyobinafsishwa sasa hivi hayaendi na yanapokwama unakuwa ni mzigo kwa serikali. Kwa hivyo, nasisitiza sana huo ubinafsishaji tuufikirie sana.

Jengine ninalotaka kuchangia Mhe. Spika, ni kuhusu sekta ya uwekezaji. Mhe. Spika, sekta ya uwekezaji ipo na ilitaka kufanywa, maana ilifanywa lakini haijawahi vizuri. Ilitaka kufanywa kwamba ni kituo kimoja tu, mwekezaji asipate tabu wala asihangaike, lakini bado dosari ipo na inaonekana kwamba hawakai pamoja. Kama hawakai pamoja na wala hawana maamuzi ya pamoja, basi wanawapeleka mbio wawekezaji.

Mhe. Spika, chengine ambacho kinanishughulisha ni kwamba wanapotoa ardhi kwa mwekezaji, bado hawafuatilii hatua ambazo mwekezaji anakwenda nazo. Nitatoa mfano Mhe. Spika, uko mradi mkubwa kule Muyuni Matemwe, lakini bado mpaka leo hupati taarifa, hakujengwi wala hakuendelezwi ni pori tu. Kwa bahati mbaya sana kuanzia karibu ya Nungwi mpaka Kijini yenyewe Muyuni wamepewa wawekezaji, lakini hakufanywi chochote. Wananchi walitegemea sana ajira hapo kwa huyo mwekezaji, kwa sababu mwananchi ni lazima ategemee ajira, kuanzia ujenzi, kufyeka fyeka na ikishafika ajira kubwa najua sio yao ni ya hao wengine wanaotoka nje. Lakini hata ile ambayo waliitegemea haipo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho naomba anipatie ufafanuzi kupitia watendaji wake kuhusu Mradi wa Muyuni hivi sasa ni mwaka wa ngapi na umefikia hatua gani.

Mhe. Spika, kama bado hatua haijaonesha mwelekeo basi ninapenda sana mwekezaji japokuwa rafiki pia ni ndugu yetu, lakini mradi ule uangaliwe kama hauwezi ni vyema ardhi kurudi serikali, kwanza ardhi yenyewe ilikuwa na mzozo kwa muda mrefu. Kwa hivyo, hakuna sababu kwamba ardhi ile isiwe ya serikali, nadhani ardhi irudi serikali ili wananchi waweze kuitumia kwa mapana ardhi yao.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Mhe. Spika, eneo hili ni kubwa sana ambalo ni zuri na kuna haja sisi sote tukisaidie chuo kiweze kupiga hatua. Hivi sasa vijana wetu wengi wanashindwa kuomba kazi mahotelini, kwa sababu bado hawajataka au hajawaamua kwenda kusoma kwanza na baadaye ndio kuomba kazi.

Kwa hiyo, naomba chuo kiwe na utaratibu wa kuwasomesha wanafunzi, ili maeneo ya mahoteli zaidi watendaji wake wanatoka hapa Zanzibar. Mhe. Spika, tunashukuru kwa wale ambao wamekwenda na kujiunga na chuo, hivi sasa wengi wanafanyakazi vizuri.

Lakini jambo lililonifurahisha kwamba hivi sasa kimeandaa mitaala ambayo itawafanya waweze kuwasomesha vizuri wanafunzi.

Vile vile suala jengine ambalo limenifurahisha zaidi kwamba sasa wanasomesha, hivi sasa kama inavyoonekana kwenye kitabu wanao walimu karibu watano ambao wenye sifa. Kwa kweli ni jambo la kupigiwa mfano sana chuo hiki. Mhe. Spika, sijaitizama bajeti yao mara hii imeomba kiasi gani, lakini naomba kwenye bajeti yao Katibu Mkuu awasimamie vizuri, ili wapate hilo fungu kwa ajili ya kufanyia kazi zao.

Mhe. Spika, tunao utaratibu kwamba Katibu Mkuu akiona jambo hili halina umuhimu sana, yaani ikimjia tu na serikali nzima na wala sikusudii Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, basi hashughulikii zile fedha za kufanyia kazi mbali mbali na kupatikana kwa haraka.

Kwa hiyo, naomba ajitahidi sana na ionekane kwamba kuna mabadiliko makubwa. Kwa kweli tukizingatia hivi sasa inaonesha chuo hiki kinajiunga na *NACTE* na kitatambulika kitaifa na kimataifa. Kwa maana hiyo, inawezekana tukawa na upungufu mkubwa wa nafasi za kusomesha, kwa sababu Watanganyika, Waganda pamoja na sehemu nyengine watakuja kusoma. Mhe.

Spika, nadhani tujitahidi sana kushughulikia sisi wenyewe watoto wetu wasome.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la mwani. Mhe. Spika, mwani ni biashara na zao hili linalimwa kimya kimya zaidi kuliko hata hiyo karafuu yenyewe ambayo inapigiwa kelele. Kwa kweli wakulima wengi wanalima mwani na wanazalisha kwa wingi, lakini bado hakuna taarifa zozote kutoka serikali, kwa sababu inaonekana zao hili wenyewe ni wanawake tu na wala hivyo sivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakumbuka mwaka juzi watu walipiga kelele sana kuhusu bei na Mhe. Waziri Kiongozi kwa umahiri wake alijitahidi sana kuwaweka wale wanunuzi wa mwani, Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na sisi Wawakilishi kwa lengo la kujadili bei. Kwa hivyo, tuliona kwa kiasi gani au wakulima wa mwani wanaweza kufaidika, nadhani iliongezeka kama shilingi mia 200 au 300.

Lakini tokea siku zile Mhe. Spika, hatupati taarifa za soko ziko vipi na bado wanunuzi wa mwani wananunua vile wanavyotaka wenyewe, yaani siku akitaka ananunua na siku nyengine hanunui. Kutokana na hali hiyo, lazima tupate maelezo huko kwenye soko kuna nini hawautaki au kuna tatizo gani, kwa sababu kitu chochote unatakiwa uwe unapata taarifa kwa ajili ya kuwambia wahusika, ili waone wanafanya vipi.

Mhe. Spika, nafikiri ni vyema tukaelezwa kuhusu Soko la Mwani na hivi sasa bei iko vipi pamoja na wanunuzi wako katika hali gani, kwa sababu hawa wakiona kazi hii wanawaniana kidogo basi wanajitokeza kuongeza bei, lakini wakiona mmoja ametafuta shughuli nyengine na wao wanasimama kibei. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, tujitahidi sana kwa hili. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo nataka kulisema kuhusu wale wahusika, yaani wanunuzi waendelee kuwapa vifaa wale wakulima. Mhe. Spika, pamoja na hayo, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupitia Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini inajitahidi sana kuwapa vitendeakazi, lakini kwa upande wa wanunuzi wajitahidi sana.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, mimi mwenyewe baada ya kupata maelezo ya wawekezaji wa mahoteli wale wanaondoka na fedha za watu, Hoteli zenyewe ni *Going* na nyengine *Venta Club*, nitaunga mkono kwa kiasi ambacho kinahitajika kuungwa mkono. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi sina mchango mkubwa sana, isipokuwa nataka kutoa baraka zangu kwenye Wizara hii ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwenye Sekta ya Uwekezaji Mamlaka ya Uwekezaji *ZIPA*. Katika miaka ya 1996/1997 eneo la jimbo langu na mimi nilibahatika kupata miradi ya uwekezaji.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naendelea kuhimiza tu wale tunaopata dharura basi tukitoka nje turudi kwa ajili ya kumaliza kazi katika Wizara hii ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninachotaka kujua ni masuala kwa Mhe. Waziri, kwa sababu mwaka 1997 wananchi wa Shamiani waliingia mkataba na Kampuni ya *Pemba Resort Limited* kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa Hoteli ya Kitalii. Katika mkataba huo ambao ninao na nimeuona wananchi wa eneo lile walikubaliana kutoa sehemu yao ya shamba kwa madhumuni ya shughuli hiyo, mategemeo wao watalipwa dola mia 300 kwa mwaka kama ukodishaji wa eneo lao.

Kwa hivyo, kwenye mkataba huo ambao walikubaliana walipane kila baada ya mwaka, lakini kutokana na maelezo ambayo wananchi wa Shamiani wanayotoa, basi mkataba huo haukutekelezwa. Pamoja na hayo, ujenzi wa hoteli ya *Kiwani Resort* uliendelea mpaka pale ambapo mwekezaji amefilisika.

Mhe. Spika, wananchi wale waliendelea na hatua za kudai, lakini kila ngazi waliyokuwa wakifuatilia zaidi walikuwa wakipata vitisho na walifikia hatua ya kuambiwa kwamba wanaweza kuwekwa ndani badala ya kupewa ufafanuzi wa hoja yao.

Kwa hivyo, mimi kama mwakilishi wao nilipoona sasa hatua imekuwa kubwa, basi nilikwenda moja kwa moja *ZIPA* mwezi wa Aprili, kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa ziada kuhusiana na suala hili. Kutokana na kwamba nilikwenda bila ya barua basi watu wa *ZIPA* walinielekeza kuwa niandike barua na niweke hoja yangu pamoja na kuambatanisha na mkataba wenyewe.

Mhe. Spika, mwezi wa Aprili nilifanya hivyo na barua niliipeleka *ZIPA* pamoja na mkataba wenyewe, pia niliomba kupata majibu kuhusiana na ufafanuzi wa lile suala. Lakini mpaka nazungumza hapa sina majibu yoyote niliyoyapata.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kwamba wananchi wangu walipata vitisho na mimi kama mwakilishi niliandika barua, kwa ajili ya kupata ufafanuzi na hadi hii leo sijapata jawabu lolote. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa hisani yake naomba anipe ufafanuzi mzuri, kwa sababu nahitaji kupeleka majibu kwa wale ambao wamenituma, ili sote kwa pamoja tupate ufafanuzi wa suala hili.

Sambamba na hilo wakati yanafanyika haya mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani, vile vile niseme ninabahati kwamba Katibu Mkuu wa Wizara hii ni mtu kutoka Jimbo la Kiwani. Kwa hiyo, nisingependa kabisa kuona kwamba wananchi hawa hawapati taarifa kwa uwazi kuhusiana na suala hili, kwa sababu mimi mwakilishi nipo na Katibu Mkuu ni mtu wa Kiwani. Hivyo tunahitaji ufafanuzi wa hali ya juu, ili wananchi wa Mwambe/Shamiani wapate kujua nini hatima ya suala lao.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kujua kwa ufupi ah! Kwa kweli nimeshangazwa sana na maelezo ya kitabu hiki, kwa sababu mwaka jana kwenye bajeti ya wizara hii ni mimi ambaye nilihoji uwekezaji eneo la Kuji. Lakini Mhe. Waziri alinijibu kwa ufanisi mkubwa kwamba eneo lile limesita kuwekezwa kwa sababu kuna mafuta ndani yake.

Hata hivyo, kwenye kitabu hiki kinasema juhudi zinaendelea kutafutwa. Sasa sifahamu juhudi zipi za uchimbaji mafuta au uwekezaji wa masuala ya utalii.

Mhe. Spika, niliwahi kusema kwamba mimi niliiona mikataba, yaani niliziona barua za Kamisheni ya Utalii pamoja na *ZIPA*, lakini kwa wakati ule nilishindwa kupata majibu, kwa sababu Mhe. Waziri alitupeleka moja kwa moja kwenye suala la mafuta. Kwa kweli Baraza hili watu ukiwatajia suala la mafuta kwa sababu ndio hamu yetu, basi tulikuwa hakuna haja tena. Nadhani mafuta yamekaa na hivi sasa wanaendelea na juhudi za kumtafuta mwekezaji.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika anipe ufafanuzi, hatua hizi suala la mafuta limekufa na hivi sasa mnataka kujenga hoteli ya aina gani, kwa hivi sasa nani amejitokeza kuomba. Mhe. Spika, nilikuwa nikipata tabu kwa sababu Mhe. Said Ali Mbarouk huniambia kwamba Katibu Mkuu wa wizara hii walisoma pamoja na asili yao ni watu wa Ole.

Sasa naomba kupata ufafanuzi, kwa majibu haya tunababaishana au ndio udhati wa hali ilivyo, kwa sababu haya ni majibu yale ya Kiole ya kuuziana maua basi mimi siyapendi. Mhe. Spika, kama mwaka jana aliniambia Mhe. Waziri eneo lile lina mafuta na leo ukiniambia kwamba mnaendelea kutafuta mwekezaji. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika anifafanulie ni mwekezaji wa aina gani.

Mhe. Spika, ninavyoamini na kwa sababu nimesikia kesho kutwa anakwenda Bungeni, basi naamini akiondoka humu Barazani hapa patajengwa hoteli. Lakini kumekuwa na usiri mkubwa na wala hataki kutueleza hili eneo nani mwenye kuliomba. Kwa kweli ninahakika baada ya uchaguzi huu Mwenyezi Mungu akimjaalia kuwa Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, basi akiondoka hapa patajengwa hoteli ya kitalii na hakuna mafuta wala dhahabu.

Mhe. Spika, nimenyanyuka kwa sababu hiyo. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitika kwako Mhe. Spika, kuhusu suala la Mwambe/Shamiani pamoja na Kuji nipate ufafanuzi mzuri, kesho kutwa atakapoondoka tukijaaliwa *hansard* ioneshe majibu ya waziri aliyeondoka.

Mhe. Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja lakini mpaka nipate majibu. Naomba kukaa.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuichangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na kutoa maelekezo pale palipohitaji maelekezo na kuuliza kwa ajili ya ufafanuzi pale palipotakiwa kuulizwa.

Mhe. Spika, waliotoa mchango katika mjadala wa bajeti hii ni Waheshimiwa Wajumbe 20 waliopata nafasi ya kuchangia kwa kutumia vipaza sauti na wajumbe wa tatu wametoa mchango wao kwa maandishi.

Naomba sana niwataje wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia kwa kutumia vipaza sauti ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi);
2. Muhyddin Moh'd Muhyddin (Waziri Kivuli wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji);
3. Mhe. Ali Suleiman Ali;
4. Mhe. Omar Ali Jadi;
5. Mhe. Omar Ali Shehe;
6. Mhe. Said Ali Mbarouk;
7. Mhe. Ali Denge Makame;
8. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui;
9. Mhe. Asha Moh'd Hilal;
10. Mhe. Haji Faki Shaali;
11. Mhe. Assaa Othman Hamad;
12. Mhe. Fatma Abdalla Tamim;
13. Mhe. Hamad Masoud Hamad;

14. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
15. Mhe. Ame Ussi Juma;
16. Mhe. Najma Khalfan Juma;
17. Mhe. Raya Suleiman Hamad;
18. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi;
19. Mhe. Ame Mati Wadi na
20. Mhe. Hija Hassan Hija

Mhe. Spika, waliotoa michango kwa maandishi ni Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Suleiman Hemed Khamis na Mhe. Ashura Abeid Faraji. Mhe. Spika, narudia tena kuwashukuru wote kwa michango yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sasa niseme yafuatayo kabla sijaingia kwenye hoja moja moja. Kwa kweli kama ilivyobainika kwamba wizara hii na sekta inazozifanyiakazi Utalii, Biashara na Uwekezaji, sekta hizi zinagusa maeneo mengi, yaani zinagusa mpaka maeneo ya kisiasa. Kwa mfano tumemsikia Mhe. Rashid Seif Suleiman alivyojimwaga na kweli aliyoyasema ni *concern* yetu sote, yaani sote tunaguswa na hilo.

Lakini niseme kwamba wizara hii inagusa sehemu nyingi. Kwa mfano, kuna matatizo ya masuala ya karafuu na kilimo chake pia jinsi zinavyozeeka na wala hazichumwi, kwa kweli si matatizo moja kwa moja ya wizarani kwangu. Vile vile kuna matatizo ya ujenzi wa barabara, upelekaji umeme pamoja na matatizo ya ardhi na miundombinu hayagusi moja kwa moja wizarani kwangu.

Hata hivyo, nataka nimshukuru sana Mhe. Mjumbe mmoja aliyesema jamani muisaidie wizara, kwa sababu mambo haya ni shughuli za kiuchumi ambayo inagusa kila sekta. Kwa hivyo, sekta zote zifanyekazi kwa pamoja, ili wizara hii iweze kufanyakazi zake kwa uzuri zaidi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, mengi yamezungumzwa, lakini yalitoka nje ya wizara. Kwa hivyo, nami nishirikiane na Mhe. Mjumbe aliyetoa ombi hilo kuomba sekta nyengine wasaidie nguvu zao, ili tuweze kwenda vizuri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa niingie kwenye hoja moja moja zilizozungumzwa, kwa ajili ya kuzitolea ufafanuzi pale itakapowezekana. Sasa pale nitaposhindwa kutoa ufafanuzi basi nitawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba sikupata muda wa kutoka nje na kwenda kutafuta ufafanuzi unaotakiwa, kwa sababu nimetakiwa kujibu wakati huu.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la *TCFB* ambalo liliulizwa kwa nini bajeti ya mwaka jana liliondoshwa kufanyiwa kazi. Kwa kweli tumeamua kuiondosha ripoti *TCFB*, ili kwanza tushughulike na marekebisho ya Sheria pamoja na Sera

za Biashara. Kwa maana hiyo, tuliripoti kwamba tumefanya marekebisho, yaani tumefanya marekebisho ya Sheria nne za Biashara na tumeacha kuifanyiakazi ripoti ya *TCFB*.

Katika ripoti ya *TCFB* kilichokuwa kikizungumzwa mule ni kupanda kwa gharama za biashara hapa Zanzibar, kutokana na huduma hafifu za bandarini. Sasa tumeona kwamba kwa kuwa bandari imeshatengenezwa na huduma zimekuzwa, kwa hiyo hakuna tena sababu ya kushughulikia ripoti ile, kwa sababu bandari inatoa huduma zinazotakiwa hivi sasa.

Mhe. Spika, kwa kweli bandari yetu inatoa huduma nzuri zaidi hata kuliko Bandari ya Dar-es-Salaam. Kwa hivyo, tukasema ripoti ile tuiweke pembeni na tushughulikie kuimarisha mazingira ya biashara. *(Makofi)*

Vile vile kulikuwa na suala la kujirudia kwa malengo ya mwaka jana na huu. Mhe. Spika, kuna malengo ambayo mwaka jana tulianza kuyafanyiakazi na mwaka huu yanakamilishwa. Kwa mfano, ukipitia hotuba ya bajeti kwenye kitabu inasema kabisa, mwaka jana tulisema kufanya marekebisho ya sheria, lakini mwaka huu tunasema kukamilisha kwa sheria.

Ni kweli kwamba rasimu za mwanzo za marekebisho ya sheria zile yako tayari. Lakini bado mchakato unaendelea, kwa sababu tunatakiwa kuziwasilisha katika Kamati Tendaji ya Wizara wapitishe, twende kwa Makatibu Wakuu, Baraza la Mawaziri na baadaye tulete hapa, ndio maana tukasema kukamilisha hatua za kufanya marekebisho ya sheria zile. Kwa hivyo, hakuna kujirudia kwa hayo malengo.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Kwa kweli mwaka jana tuliomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo wakati tunajitayarisha kufanya hivyo tukakumbana na tatizo la uhalali wa matumizi ya ardhi ile. Sasa kama tulivyosema kwenye kitabu chetu kwamba ardhi ile ilikuwa inamilikiwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Kwa hivyo, tulifanyakazi ya kuomba eneo lile litumike kama chuo kubadilisha Waraka au Hati ya Matumizi ya Ardhi ipewe chuo. Sasa baada ya kupata Hati ya Matumizi ya Ardhi ndipo tulipoanza shughuli za kupima eneo lile na kulipangia matumizi mazuri. Kwa kweli hatukutaka kuharibu uzuri wa eneo lile, yaani ile minazi, bustani pamoja na mambo mengine tumetaka vibakie.

Kutokana na hali hiyo, tukachukua wataalamu kutoka Idara ya Ardhi na Upimaji kutupangia jinsi ya kutumia eneo lile, ndio maana kuna msingi ambao umeanza, lakini haujaendelezwa tukawa tunasubiri michoro mipya, ili tuweze kutumia na michoro hivi sasa iko tayari.

Kwa hivyo, kuanzia mwaka wa fedha ujao chuo kitajengwa nafasi za madarasa zitapatikana na hivyo vyombo vilivyonunuliwa vitapata sehemu ya kuwekwa. Kwa maana hiyo, suala la chuo tumelishughulikia kwa kiasi hicho, mategemeo yetu ni kwamba huko tunakokwenda mwaka huu wa fedha chuo kitajengwa na matatizo madogo madogo yatakuwa yameondoka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala la vitendeakazi katika Idara ya Kumlinda Kutumiaji. Kwa kweli nataka nikiri katika changamoto zetu tumeandika kwamba bado tunakabiliwa na tatizo la vitendeakazi pamoja na utaalamu. Kwa hivyo, hilo tunakiri na tunalijua na tunalifanyiakazi.

Vile vile kulikuwa na suala la *Investment Forum* ngapi zimefanywa na *ZIPA*. Mhe. Spika, katika kitabu chetu sehemu ya uwekezaji tumekiri kwamba *ZIPA* kwa kutumia fedha zake haikuwahi kufanya *Investment Forum*. Lakini tumetumia Mtandao wa *East Africa* kushiriki katika *Investment Forum* zilizotayarishwa kupitia mitandao ya Ushirikiano wa Kikanda.

Mhe. Spika, kuhusu suala la karafuu. Kwanza naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba karafuu ni uti wa mgogo wa uchumi wetu. Lakini kwa vipimo vya kiuchumi katika miaka ya karibuni Sekta ya Utalii imejitokeza kuwa iko juu yaani inaongoza.

Hata hivyo, ni kweli kabisa karafuu ndio uti wa mgogo wa nchi yetu hapa Zanzibar, kwa sababu Sekta ya Utalii chochote kikitokea ulimwenguni au hapa ndani inatetereka, lakini mikarafuu kwa muda mrefu imekuwa ikituchumia na wala haijatetereka.

Mhe. Spika, nadhani imetetereka hivi sasa kwa sababu imezeeka na mikarafuu mipya jitihada zinafanywa za kuipanda, lakini mkarafuu ukeshakuupanda leo. Kwa mfano, tuseme ile iliyopandwa mwaka 2005 wakati tunaingia leo bado hatujaanza kuchuma na mikarafuu ile inaendelea kukua na inahitaji huduma na mipya mingine inahitaji kupandwa, kwani mingi imezeeka. *(Makofi)*

Kwa kweli kupungua kwa karafuu kunategemea mambo mawili moja kuzeeka kwa mikarafuu na jengine ni hali ya hewa kwa kipindi fulani au mwaka wenyewe. Kwa hivyo, karafuu zinapungua kwelli, kwa sababu mikarafuu michanga. Lakini tukiingia kwenye mashamba ya mikarafuu na hasa Pemba na hata hapa Unguja iko mikarafuu michanga ambayo inakuja juu na tatizo ni kwamba kipindi cha kuchumwa bado.

Mhe. Spika, nafikiri baada ya miaka mitano au kumi ijayo karafuu itarudi hali yake, kwa sababu ile inayopandwa hivi sasa itakuwa imeshakua na tayari imezaa karafuu.

Pamoja na hayo, nataka nisisitize umuhimu wa Mabwana na Mabibi Shamba kwenda kuikagua ile mikarafuu mipya inayopandwa. Mhe. Spika, ni kweli serikali inapoteza fedha nyingi. Kwa mfano, sisi kupitia Shirika la *ZSTC* tunatoa shilingi 80 milioni kila mwaka, kwa ajili ya kushughulikia mikarafuu, lakini kazi ya kuhakikisha mikarafuu inao afya au haina ama umekula haukula ni kazi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Spika, naomba niungane na waliosema kwamba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira nayo ijitahidi, kuhakikisha kwamba mikarafuu ambayo inapandwa hivi sasa baada ya miaka kumi imekua na imeanza kutoa matunda.

Vile vile kuna suala zima la viwanda. Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, kwa kweli ameieleza vizuri Sekta ya Viwanda. Pamoja na ukweli kwamba Sekta ya Viwanda imeanguka kwa sababu tofauti. Kwa mfano, kulikuwa na viwanda vya nyumba ambavyo vilikuwa vikiendeshwa na serikali, kwa sababu za kiutawala pamoja na mambo mengine viwanda vile vimeanguka na cha serikali ndio cha serikali.

Mhe. Spika, serikali imejitahidi kubinafsisha viwanda vile kwa bahati mbaya havijaanza kazi na vilivyoanza vimeanza kwa kasi ndogo. Lakini Sera yetu ya Viwanda inasema, ili tuweze kukuza uchumi wa kati, yaani *Middle Class Economy*. Sasa hawa *Middle Class Economy* ni wazalishaji wadogo ambao ndio wenye kuchangia uchumi kukua.

Kwa hivyo, tulichokifanya kama tulivyosema mwaka jana na huu ni kuanzisha *Database* ya hawa wenye viwanda vidogo vidogo na vile vilivyokuwepo ambavyo vimekufa, vile vitashughulikiwa mlango mwengine, yaani vile vitashughulikiwa na Kitengo cha Mitaji ya Umma kwa sababu ni mali ya serikali kwa kushirikiana na sisi.

Kwa mfano, amekuja mwekezaji anataka kiwanda hiki, basi tunapeleka Kitengo cha Mitaji ya Umma tunakubaliana na tunawapa, kama tulivyofanya kwa Kiwanda cha Viatu na kile cha Maziwa.

Lakini hivi vidogo vidogo ni jukumu la Idara ya Viwanda kuvikuza. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwamba viwanda vile vinahitaji kukuzwa, ndicho tunachokifanya hivi sasa kwa kupitia mafunzo pamoja na kuwatayarishia mtaji, ili waweze kuwa na mitaji kwa ajili ya

kununua mashine za kisasa ambazo ni bora na kuweza kukuza viwanda vyao. Kwa kweli viwanda vile si vya kudharau. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu suala la biashara ya Comoro imeanguka, kwa sababu miongoni mwa bidhaa ambazo walikuwa wakichukua wafanyabiashara wa Comoro kutoka Zanzibar ni tambi, tena walikuwa wakichukua kwenye mapolo.

Lakini kutokana na kutokuwa na usafiri wa uhakika, wakati ule meli zetu zikienda mpaka Comoro, yaani Wangazija wa kule wanaingia na kuja huku wanabeba wanakwenda zao, Wangazija wa hapa wakati wanapokwenda kwao wanabeba na kwenda zao pamoja na mambo mengine mbali mbali.

Kwa kweli kuporomoka kwa usafiri imekuwa ni vigumu sasa kwa watu wa kawaida Comoro na Zanzibar kwenda katika sehemu hizo mbili na kuweza kufanya biashra, isipokuwa usafiri ambao upo ni ndege yenye kuongeza gharama ya kufanya biashara.

Mhe. Spika, nirudi tena kwenye viwanda kama tutavikuza viwanda vile na kuvielekeza ipasavyo, basi viwanda hivi vinaweza kuzalisha vizuri, vikafanya *packaging* inayotakiwa, tumesema tunaweka suala la viwango, yote lengo ni kukuza viwanda hivi. Vile vile kuangalia viwango wanavyovizalisha na kuweza kupenya kwenye masoko hata ya hapa kwenye kanda yetu na wala sio lazima Masoko ya Ulaya, yaani Masoko katika Kanda yetu.

Kwa hivyo, kama tulivyosema hapa kwamba Jumuia ya Afrika ya Mashariki imeanza Soko la Pamoja, tusipozalisha Zanzibar hatutaweza kutumia soko hilo. Sasa katika kujitayarisha kuzalisha ni kukuza Viwanda hivi Vidogo Vidogo.

Mhe. Spika, nini tumefanya katika viwanda hivi. Kwanza tumekuja na Mbinu au Mkakati wa Usafirishaji Zanzibar, ambapo juzi wakati nilipokuwa nikijibu swali nilisema kwamba ndani ya mkakati ule kuna mambo matatu makubwa ambayo yanataka kufanyika.

Kwanza ni mafunzo kwa wenye viwanda, pili nalo tumelizungumza kwenye Baraza la Biashara kwamba *PBZ* iwe na tawi maalum kwa ajili ya mikopo ya wafanyabiashara, ambao wizara itawa-*recommend* na wala sio mikopo ambayo ilitoka wakati ule na watu wakachukua fedha na kuziponda na kuondoka nje ya nchi.

Mikopo hii itakuwa mfanyabiashara anakuwa *recommended* na wizara anakwenda *PBZ* sehemu maalum na kuweza kupata mkopo na wizara inamsaidia kumlea na wala si wizara peke yake. Kwa kweli suala hili

linafanywa pamoja na Jumuia ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima.

Mhe. Spika, niseme kwamba tunalo tatizo la viwanda vikubwa, lakini kuna umuhimu mkubwa sana wa kukuza viwanda vidogo vidogo na wala hatupaswi kuzibeza.

Vile vile kulikuwa na suala la daladala kuingia mjini, lakini hili Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi atalichukua na kuweza kulifanyiakazi hasa kesho, ambapo ataingia na bajeti yake.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala mahoteli pamoja na walinzi wanaoajiriwa hotelini. Kwa kweli suala la ulinzi na usalama wa watalii ni wetu sote na wala sio wa wizara peke yake. Kwa maana hiyo, baadhi ya vijiji vyenye mahoteli ya kitalii walichofanya, hapa nataka nichukue nafasi hii kutoa mfano kijiji cha Uroa na niwasifu sana. Kijiji cha Uroa baada ya kuona kwamba kuna hayo matatizo wanaowajiriwa wao wenyewe hawawaamini kama walinzi, matatizo yakitokea na majambazi yakiingia wanakuwa wanaathirika mpaka wao wana kijiji, walichofanya wana kijiji wote wameunda mtandao wa ulinzi katika kijiji chao, wanashirikiana na wanajeshi wastaafu na jeshi la polisi kufundishwa mambo ya ulinzi lakini wenyewe pia wametafuta walimu kusoma mambo ya utalii, lakini pia wanasoma mila na desturi za Kizanzibar.

Madhumuni ya kujiunda namna hii ni kwamba kazi zote zitakazotokea katika kijiji chao waweze kuzifanya wenyewe na hili pia wamewashirikisha wawekezaji wa eneo lile, kazi zote katika maeneo yale wazifanye wenyewe kama ni ulinzi, kama usafishaji, kama bustani kila kitu wafanye wenyewe, kwa maana hiyo watazuia wageni kuingia pale na kufanya mambo yasiyo maana katika eneo lile. Kwa hivyo niseme tu kwamba shughuli ya ulinzi na usalama wa utalii na nchi yetu ni letu sote, jeshi la Polisi, Wizara hii lakini pamoja na wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, nikiacha niliyoyazungumza sasa hivi naomba niendelee kuliulizwa swali na Mhe. Omar Ali Jadi suala la ushuru kwa wafanya biashara wadogo wadogo, alisema kwamba nyinyi mnakuza wafanya biashara wadogo wadogo lakini mbona wanapata usumbufu wakifika Dar es Salaam. Mhe. Spika, kuna mambo mawili kuna wafanyabiashara wanaopeleka bidhaa Dar es Salaam na kupeleka nje zaidi, wafanyabiashara wale wanakwenda na nyaraka zao zote bandari *TRA, ZRB* na kila kitu wakifika pale wanatoa mizigo yao wanaweka kwenye matreki wanakwenda. Haya tumeyazungumza na usumbufu haupo usumbufu unatokea pale ambapo mtu amekwenda na *TV* zake tatu nne hata kama kazinunua mitumba lakini ziwe na risiti, kuna watu wanakamatwa pale na

TV tatu au nne hazina risiti, kwa hivyo unapokwenda na *dogment* zako kamili usumbufu huu haupo.

Kuna kesi ilikuja kwetu mtu kenda na TV tano na vitu vyangine vyengine lakini risiti alizokuwa nazo hana risiti halisi za kupita Bandari, *ZRB* na *TRA* kenda tu na kirisiti cha mkono kwa hivyo pale wamemzuia, huenda mali ile ikawa ya wizi sio mali ya halali. Kwa hivyo kama utakwenda na risiti zako kamili usumbufu siku hizi umepungua kwa kiasi kikubwa wanachozuia pia kutoka na mali ya wizi Zanzibar na kwenda nayo kule. Kwa hivyo mimi ningewaomba tu wafanya biashara wanapokwenda waende na makaratasi yaliyotimia kama kodi imelipwa vizurim, kama kuna nyaraka ambazo zitoke taasisi tofauti wote wawe nazo na wakifika pale watapita na hatukukuwa na usumbufu.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la vyakula kumalizika muda kazi hii sasa kwa sababu ukitizama hotuba za bajeti za nyuma wakati kazi hii inafanywa na wizara yangu peke yake nilikuwa naonyesha kabisa kwamba katika mwaka huu bidhaa ambazo tumezitembelea na kukuta zimemalizika muda wake ni kiasi kadha, za thamani kadhaa na tumezitupa pwani au tumezichoma au tumezifanya jee, lakini kwa kipindi hiki tokea tumepitisha sheria ya vyakula vipodozi na madawa kazi hii inafanywa pamoja na vyakula na vipodizi na madawa. Kwa hivyo pamoja na kwamba kitengo changu cha kumlinda mtumiaji kinashiriki lakini kinashirikiana na bodi na bodi ndio inayopaswa kutoa taarifa ya mambo haya. Lakini hata hivyo niseme nalichukua kwa upande wa kitengo changu na tutaengeza jitihada katika kulifanyia kazi.

Mhe. Spika kulikuwa kuna maswali kwamba safari ya kumaliza umasikini ni kubwa kwanza kwa sababu ya bajeti ambayo wizara inapewa, lakini pili kutokana na urari mkubwa wa biashara ambao huwa tunauripoti kila mwaka. Mhe. Spika, nataka nikubaliane nae kwamba safari hii sio fupi ni ndefu na tutaweza kupunguza urari wa biashara pale Zanzibar itakapoweza kuzalisha na tutaweza kuzalisha kama tutakuza viwanda vyetu vidogo viweze kuwa vikubwa.

Kuna na suala la Elimu na suala la uwezeshaji lakini kama nilivyosema tumelizungumza kwenye baraza la biashara za Zanzibar na kwamba katika baraza lile makubaliano ni kwamba PBZ iwe na *wing* maalum ambao utaweza kutoa mitaji kwa wafanya biashara wadogo wadogo, wale ambao watakuwa tayari. Lakini jengine tunalolifanya kupitia jumuiya ya wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima kuna aina ya mafunzo ya aina mbili yanatoka pale.

Moja wanaita BDS mafunzo haya ni kwamba *Tanzania Private Sector Foundation* wamepewa pesa na *World Bank* pesa zile zimegaiwa kwa Tanzania

Bara na Zanzibar, tunachokifanya ni kuchukua wafanya biashara wanaoomba tunawaweka katika mafunzo miezi mitatu baadae tunamtaka mfanya biashara aandike mchakato utakaomuwezesha kupata fedha kwa biashara yake ambayo ameitayarisha. Baada ya kupokea mchakato tunafanya ukaguzi wa biashara yake na kama ameandika vizuri kuna mtaji unatoka kwa kiasi ambacho mfanya biashara ameomba, kwa sababu ni wafanya biashara wadogo wadogo basi nadhani *limit* ya juu kabisa ni milioni thalathini, lakini kwa hapa kwetu mfanya biashara aliyepata kubwa kwa mwaka jana ilikuwa ni kwa milioni ishirini na tatu.

Kwa hivyo kazi hii tunaifanya na kuna *capital* mpaka ya milioni moja zinatoka kwa hivyo kwa mwaka jana si chini ya wafanya biashara tisa kama sikosei walifaulu kupata pesa hizi, lakini vile vile mwaka huu mafunzo yale yanaendelea na kwa mwaka huu jumuiya wameongeza fursa nyengine zaidi, wenyewe wanaiita fursa ndio hii kuza mtaji wako na wanakwenda katika maeneo yale yale, kufundisha wafanya biashara kwa miezi mitatu na baadae wafanya biashara watapewa mitaji ya kuweza kujiendeleza katika biashara zao.

Hii fursa ya pili Jumuiya ya wafanya biashara wenye viwanda na wakulima wameshirikiana na *MACEMP* na *MACEMP* ndio wamekubali kutoa pesa hizo, kwa hivyo jitihada zinafanywa katika pande zote kwenye *private sector* na ndani ya serikali, ili kupunguza urafu wa hiyo safari yetu ya kupunguza umasikini.

Kulikuwa na suali la *Economic Diplomacy* tunawatumiaje mabalozi wake ukweli ni kwamba kama tunatoa taarifa za uwekezaji katika balozi husika, taarifa zile zinapewa au ubalozi unazisambaza katika maeneo tofauti tumeweza kufanya hivyo katika maeneo mbali mbali lakini ni kweli pia kuna maeneo ambayo taarifa hizi hazijafika na tunafanya kazi za kuzifikisha. Kwa hivyo tunatumia balozi zetu na sisi katika kukuza uchumi wetu hapa.

Vile vile kulikuwa na suala la soko la *East Africa* Zanzibar watalitumiaje kama nilivyosema tukizalisha tunaweza kulitumia vizuri hatukuzalisha tutalitumia kwa kununua tu kuleta kwetu na kuwafaidisha wengine, lakini niunganishe na hili katika suala la soko la *East Africa* kulikuwa na suala ambalo aliuliza Mhe. Haji Faki Shaali kama sikosei, alisema yale ambayo tunayazungumza kwenye *East Africa* pia yanazungumzwa *SADC* sasa sisi kama Tanzania tunakwenda wapi wakati tuko huku na huku. Kama mwezi wa tatu mwaka huu kulikuwa na kikao kikubwa baada ya kuwa na vikao vidogo vidogo huko nyuma baina ya *East Africa Community na SADC* kuzungumza jinsi ya kuziendeleza hizi soko mbili ya *SADC na East Africa Community* waweze kutumia viwango vimoja soko moja, *currency* itakuwa ni matatizo hawajafikia huko, lakini mpaka sasa hivi wamezungumzia maeneo ya *Customs Union* na soko moja.

Kwa hivyo mazungumza bado yanaendelea ya kuweza kuwa na masoko mawili kwenye *Customs Union* na soko moja la uchumi, kwa hivyo ni matumaini yetu kwamba wataweza kufikia makubaliano na mambo yatakwenda vizuri, lakini kama tukishindwa kuelewana hizo soko mbili basi Tanzania itabidi ichague aidha ikae *SADC au East Africa* wataangalia uzito wao uko wapi, kwa sababu *SADC ni mtoto wao na East Afrikai* ndiko kwao. Kwa hivyo wataangalia uzito uko wapi.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala linalosema bidhaa zipi zilisafirisha kwa mwaka huu uliopita, bidhaa zilizosafirishwa ni bidhaa ambazo zinatoka katika viwanda na hasa *Industry Park* ya Amani pale tunazalisha *casset*, tunazalisha nguo, tunazalisha bidhaa za plastic kuna vitu vingi karibuni *item* tano zinazalishwa pale. Lakini chengine katika usafirishaji ni hizi biashara za *Transit trade* biashara ambazo zinakuja Zanzibar halafu zinatoka yakiwemo ma. TV, mabaskeli pamoja na vitu vyengine, lakini pia likiwemo eneo huru la Maruhubi pale kuna biashara za aina kama nne ambazo makampuni yanaleta Zanzibar baadae wanatoa nje.

Pamoja na hayo bidhaa zetu maarufu kama karafuu na mwani nazo pia zinasafirishwa na ndio maana mwaka huu tumesema usafirishaji umeanguka kwa asilimia moja point nne nadhani na hii imetokana na upungufu wa usafirishaji wa karafuu na mwani, lakini maeneo mengine yamekwenda vuziri, nadhani wote mnashuhudia meli zinapoingia mabaskeli yanavyokuwa mengi nchini mpaka watu wanasema uchafu huu umeshashuka tena lakini baada ya muda uchafu haupo, tunaona ma TV yameshazongwa kwenye maplastic hayo yanasafirishwa yanaondoka. Kwa hivyo hizo ndio biashara ambazo tunafanya.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la Shirika la Magari na suala la Utalii kwa nini halipo katika muundo wa Wizara. Mhe. Spika, mwaka jana niliahidi kwamba tutakaposoma bajeti ya mwaka huu Shirika la Magari na Shirika la Utalii yatakuwa sio mashirika kwa sababu yamepunguza sifa za kuwa Shirika, taasisi hizi zitakuwa ni vitengo ndani ya Idara za Wizara kwa maana hiyo Shirika la Utalii limeingia katika sekta ya utalii ikiwemo na Hoteli ya Bwawani na Kamisheni na taasisi kama hizi na Shirika la Magari limeingia ndani ya Idara ya Biashara kwa hivyo tumelifiti humu humu.

Bado katika hotuba zatu za bajeti tumeendelea kusema Shirika la Magari na Shirika la Utalii kwa sababu muundo ule tumemaliza sisi Wizara tumeshaupitisha, tumeupeleka kwa Makatibu Wakuu ili uendelee na safari ya kuthibitishwa au kukubaliwa na serikali, kwa hivyo mpaka tulipofika sasa hivi hatuwezi kubadilisha jina la mashirika yale bali tunaendelea kuyaita hivyo

mpaka muundo ule utakapokubaliwa na serikali basi mashirika yale yataacha kuwa mashirika na yatakuwa ni vitengo ndani ya Idara za Wizara.

Mhe. Spika, kulikuwa suala ambalo nimesahau kuliunganisha mwanzo ni kwamba wizara imejipa jukumu la kusimamia mambo ya *East Africa* tueleze sasa itakapokuwa *Federation* Zanzibar itakuwa kwenye taasisi gani, nataka nitoe ufafanuzi kwamba Wizara hatujajipa jukumu la kusimamia mambo ya *East Africa*, mambo ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa yanashughulikiwa ndani ya Afisi ya Rais katika ushirikiano maalum wa ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kina katibu Mkuu wake.

Wizara huwa inajaribu kuripoti yanayoweza kutokea ndani ya kanda yanahusiana na biashara na uwekezaji na mambo kama hayo, masuala ya masoko ya pamoja, masuala ya *Customs Union* ni *consign* ya Wizara ya Biashara na Utalii kwa hivyo huwa tunatoa taarifa hizi ili wajumbe na wananchi kwa jumla wajue katika maeneo hayo Wizara inasimamia vipi. Kwa hivyo si jukumu letu kubeba *East Africa* lakini pia niseme tu kwamba tulipofika sasa hivi soko la pamoja jumuiya sasa hivi inajikita katika mazungumzo ya sarafu moja ambayo hatujui itakuwa muda gani katika kulikamilisha hilo, baada ya hapo ndipo tutazungumza *Political Federation* ya *East Africa*.

Lakini nisema kwamba tunapokuwa katika mikutano ile sisi Wazanzibari huwa tunajua nchi yetu, tunajua saizi yetu tunajua siasa zetu kwa maana hiyo tunakuwa makini sana katika mijadala ile.

Kuhusu suala la ajira sisi Zanzibar tumeweza kufunga na tumefunga ajira nyingi tu kuzifungua kwa wageni na tumefungua zile ajira ambazo tunahisi kweli tuna upungufu na hatuko makini katika hayo, lakini ajira nyengine zote za chini tumezifunga hatutoi kwa wageni na hatukufunga ajira tu lakini pia matumizi ya ardhi, matumizi ya uhamiaji na mambo kama hayo Zanzibar tumezuia tumesema sisi wenzenu hali yetu ni hii kwa hivyo tunazuia. Mambo mengi huwa tunaanza sisi kuyauliza halafu wenzetu Tanzania kwa ujumla tunayazungumza kama Tanzania, lakini mengi huwa yanaanza na sisi kwa kujua saizi yetu.

Kwa hivyo niwahakikishie tu tunapokwenda kule huwa tunakuwa makini sana upatanishi na kuna wataalam wa aina mbili, kuna wataalam ambao sisi tumewapendekeza wanalipwa *East Africa Community* ni Wazanzibar wanaingia kwenye upatanishi, lakini kuna wataalam tumewatoa humu ndani wa Mawizara yetu tunahisi huyu akienda yuko *Competent* na kwa upande wangu na Mkurugenzi wa Biashara Ndugu Rashid Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba asimame aonekane. Ndugu Rashid yeye ndio amesema vya kutosha

kwenye *East Africa* kupitia kwenye wizara yetu na kwa kweli baada ya kukamilisha mazungumzo ya soko la pamoja ndugu Rashid alikabidhiwa cheti kwamba ni mpatanishi mzuri mzuri katika *East Africa* au bora. *(Makofi)*Kwa hivyo tuko makini na haki zote za nchi yetu hatutokuwa tayari kutoa milki kwa nchi nyengine kwa sababu tunaingia kwenye *Coporation.*

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la ajira za hamsini elfu katika sekta ya utalii, kilichoonekana katika bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi tunasema *Survey* zilizofanywa na serikali katika makampuni binafsi yamesema na wamejaza fomu kwamba mimi nimeajiri watu kadhaa katika viwango kadhaa, jumla ameipata hiyo lakini takwimu zinazoonekana hapa ni za *former sekta na informer sekta*. Katika utalii kuna mambo chungu nzima kuna wasuka kili na mikoba, kuna wanaouza bidhaa za viungo, kuna wanaofanya biashara za chakula, kuna wanaofanya *Tower Operation,* kuna watembeza watalii kuna mambo chungu nzima.

Kwa hivyo sisi tumechukua wale wote na tukaona kwamba nap engine hii inaweza kuwa ndogo kidogo kwa sababu sekta ya utalii ina mikono mingi sana na imetoa ajira mbali mbali lakini ajira zile ni *informer* ambazo haziwezi kuonekana katika takwimu rasmi za kiuchumi za serikali. Kwa hivyo ni kweli kwamba hii inatofautiana na Waziri wa fedha lakini sababu ni hiyo sisi tumechukua *Formally Inclement na Informally and Prominent* na tukaja na figa hii hapa.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna pendekezo la Mhe. Nassor Ahmend Mazrui kwamba tutakapoanza kuendeleza maeneo huru ya uchumi basi tutengeneze shirika au mamlaka, pendekezo tunalichukua na tutafanya hivyo.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala la viza za *East Africa* na kwamba sasa mtalii akiingia nchi moja hatopaswa kutoa viza katika eneo jengine, hili kweli tulilizungumza ndani ya *East Africa* lakini hatukulifikisha mwisho tulizunguza na kukawa kuna mambo chungu nzima yaliyotolewa, kwa upande wetu Tanzania tulisema sawa kuna na visa moja lakini utaratibu gani tutatumia kugawa mapato ya viza na sisi mtalii akishaingia nchi moja tutajuaje mtaliki kalipa kiasi gani. Hasa kwa sababu viwango vya viza viko tofauti sasa hivi, kwa hivyo hili limezungumzwa lipo na linazungumzwa lakini halijafikia mwisho maamuzi yetu sisi mpaka tuwe na utaratibu wa kugawana mapato unaoaminika na tutakaoukubali ndio tutaweza kuingia katika hili. Lakini kwa sasa hivi hata bado halijakubaliwa kwenye jumuiya bado.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la Dk. Livingston kwa nini tumeanzisha tunzo ya Dk. Livingston. Tuna jengo la Dk. Livingstone ambalo shirika la Utalii ndio makao makuu yake tumesema tuanzishe tunzo hii kwamba katikati hapa

kutakuwa na mambo mengi, kutakuwa na *compition*, tutaweza ku- *raise fund* na kufanya nini, tukasema jengo lile ni *pride* ya Waingereza kwa sababu Dk. Livingston ni Muingereza katika *ctivitis* tulizozipanga ilikuwa ni ku-*rase fund* kulitengeneza jengo lile. Kwa hivyo atakayechangia kwa kiasi kikubwa na pia tulisema tutafanya *compition* ya maskuli kuhusu utalii, mwanafunzi atakayejibu vizuri kuhusu utalii ndio watakaopata tunzo hii ya Dk. Livingstone.

Kwa hivyo lengo letu ilikuwa ni kulitafutia pesa za kukarabati lile jengo na kuliweka katika hali nzuri, tumetumia jina hili kwa sababu ni jina la lile jengo lakini tumetumia jina hili lengo letu ilikuwa kupitia kwenye makampuni ya Kiingereza ku-*rease fund* na kulitengeneza jengo lile sababu ni hiyo tu hakuna sababu nyengine yoyote.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna suala la *link* ya kilimo na Utalii ambalo Mhe. Assa Othman Hamad alilizungumza nataka nikubaliane nae na nimwambie kwamba hiyo ndio mipango ya serikali hasa katika hii awamu ya pili tunayoendelea nayo, ku-*link* sekta ya utalii na sekta ya kilimo pamoja na sekta nyengine ambazo zitafanya utalii ukuwe. Hili lipo lakini mambo hayaji kwa mwaka mmoja mwaka huu mnapanga nnaanza kutekeleza matokeo yake tutayaona kwa miaka mitatu au minne lakini hili lipo.

Suala la maeneo huru kama kawaida majibu ni yale yale ambayo huwa nayatoa kwenyd maswali na majibu hapa asubuhi kwamba sisi tungependa maeneo huru yasimame kesho, lakini kutokana na kutokuwepo miundo mbinu mizuri inayofanya wawezezaji kufika kule basi bado, juhudi tulizozifanya ni zile zile kushirikiana na makampini ya watu wa nnje hasa *private* sekta ili tusaidiane kwa ubia katika kuendeleza hilo, hiyo ndio uamuzi tuliokuja nao sasa hivi na nilisema hapa kwamba tumefanya mazungumzao na mamlaka ya Jebelali ya maeneo huru ya Dubai, lakini pia jimbo la Buodong la China tumefanya nalo mazungumzo na wote wameonyesha mwelekeo wa kuja na kusaidiana nasi katika hilo.

Mhe. Spika, jengine uendeshaji wa hoteli kwa njia za kiisalam Mhe. Fatma Abdalla Tamim amesema je kwani hapa kwetu hatuwezi kuendesha hoteli kwa njia ya kiislam, namwambia inawezekana na zipo zinazokwenda kwa njia hizo. Kuna hoteli Zanzibar na Tanzania ukienda kwanza kwa mwanamke na mwaname uonyeshe cheti cha ndoa vyenginevyo hawakuingizi ndani na hamna ulevi mle wala nini, kuna hoteli Miraji ya Dar es Salaam pale ambayo mmiliki ni Mzanzibari, pale ukifika mwezi wa Ramadhani utafikiri uko nyumbani kuna futari nzuri kuna daku zuri, kuna kila kitu. Mpaka dira ya kibla na miswala ndani inakuwepo. Kwa hivyo uendeshaji wa hoteli unategemea nani mmiliki wa hoteli ile hata huko china alikofika kama alivyosema mwenyewe

mwendeshaji wa hotali ile ni mwarabu ambae ana maadili ya kiislam ndio ameaamua kuendesha hoteli.

Lakini jengine pia ni soko kama watu wote wanaendesha hoteli za mchanganyiko wewe ukiweka yako *specific* ina maana mwenye mahitaji yale atakufuata ulipo, kwa hivyo uendeshaji wa hotali unategemea uvutaji wa biashara silka na mila za mmiliki wa hotali na mazingira yaliyokuwepo.

Mhe. Spika, madai ya wananchi wa Pweni Mchangani au Kiwengwa ya milioni mia tatu nataka niwathibitishie waheshimiwa kwamba nakala ya barua nimeipata na *ZIPA* wameipata, baada ya kupata nakala ya barua suala hili tulilifanyia kazi. Suala la kwanza tulilojiuliza kama Wizara itakuwaje *suplayer* anadai hotel milioni mia tatu na sio suala la mara moja ni suala la kuendelea nab ado anaendelea ku- *supply* mpaka mwenye hoteli ameondoka imekuwaje.
Lakini pia tukataka kuona mkataba wa mwenye hoteli na hao *suplayer* wamekubaliana nini hakuna kitu ambacho kidhibiti unaweza kukamata, hata hivyo t umechukua hatua za kumuandikia mwenye hoteli kule aliko na kuna barua kwa sababu nimesimama sasa hivi sitokuwa na kopi hiyo ya barua, kuna barua ambayo mwenye hoteli amethibitisha kwamba hajakimbia alifunga kwa sababu ya *seezon* na alikiri kudaiwa kiwango hiki cha pesa. Lakini kwa kushirikiana na Mwanasheria wetu wa *ZIPA* na wao wa kampuni wanalifanyia kazi suala hili, kwa hivyo hili suala sasa hivi linafanyiwa kazi, lakini niseme kesi kama hizi tunazipata nyingi nyingi kuna zile ambazo wanakuja na mikataba waliyotiliana nayo na tukaweza kumbana muwekezaji na akalipa.

Lakini kuna wale ambao wanafanya hawana mikataba na wawekezaji wengine mnawajua kwa hivyo hawa na muwekezaji na hasa Venta Club anaweza kupokea kweli na kwa vile ana *good will* anapewa pesa kidogo kidogo lakini anaweka hesabu yake, sasa inafika wakati anamrusha kwa sababu hana nae mikataba. Kwa hivyo tuwaombe ndugu zetu wanapofanya kazi hizi waje serikalini na wende *ZIPA* wasaidiwe kuingiliana mikataba na hawa wenye mahoteli, ni kweli wanarushwa kwa sababu hawana mikataba ya maana.

Kuna wengine walikuja na mashtaka wamechonga fanicha ma mahotali wamefanya kazi hoteli milioni thamanini mwenye hotali hataki kuwalipa, nikawaambia nileteeni mkataba wenu nione tuweze kumkamata mkataba walioniletea ni kwamba mwenye hotali ameingia mkataba na mtu mwengine, wachongaji nao wameingia kwa mkataba ule ule wa kampuni hii. Kwa hivyo mwenye hoteli anasema muulizeni huyu mliyeingia nae mkataba mimi namlipa yeye, wakati huyu hajalipwa na hawa hawajalipwa inafika hapali sisi hatuwezi kuzishughulikia kesi kama hizo.

Kwa hivyo tunachoaambia jamani nendeni kwenye Mahakama zitaamua lakini kweli huko tuliko tuwasaidia watu wetu sisi tutajitahidi kutoa elimu kupitia *ZIPA* lakini na sisi tuwasaidie watu wetu wasifanye biashara Kizanzibari, ule moyo wa Kizanzibari wa ukarimu sasa hivi haupo maana yake wageni wapo wengi na kila mgeni anyekuja ana sifa zake. Kwa hivyo matatizo kweli yapo tunayafanyia kazi lakini na nyinyi tunaomba mtusaidie.

Suala la Kuji Mhe. Spika naomba nikiri kwamba labda watu wangu walifanya *catel past* katika kuandika hili lakini msimamo ni ule ule, katika ramani iliyotolewa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ni kwamba Kuji wana wasi wasi ni eneo la nishati na ramani inaonyesha kabisa, kwa hivyo Kuji ni kweli tumeacha kama kulivyo hatujagusa visiwa mpaka Wizara ituelekeze vyenginevyo, kwa hivyo kilichofanyika hapa ni *catel past* kwa hivyo naomba radhi kwa niaba ya wafanyakazi wangu.

Mhe. Spika, suala la *One stop centre* kama mlivyoona kwenye hotuba yetu na sisi pia tulililia kwa hivyo ukinambia hapa mimi niseme lini litakamilika na liko hatua gani, hatua tuliyonayo ni hiyo tunafanya nao kazi vizuri, lakini yanapokuja maamuzi ya mwisho wale tunaofanya nao kazi hawana maamuzi ya mwisho na sisi tunalililia hilo hilo. Lakini niseme tu labda kupitia Baraza la Biashara *issue* hizi zitazungumzwa kwa sababu kama mlivyoona kulikuwa na mambo mengi yanazungumzwa ndani ya baraza na yanapatiwa ufumbuzi, kwa hivyo kupitia baraza la biashara hili nalo tutalishughulikia.

Mhe. Spika, naona saa moja iliyotolewa kujibu kwa Mawaziri imekwisha lakini bado hoja ninazo nyingi, lakini nyingi ya hoja hizo nilishazichanganya katika kujibu jumla jumla, labda kuna suala moja tu la wanawake kupewa kipaumbele kwa kufanya biashara. Niseme kwamba kupitia *program* nilizozisema wanawake hawabaguliwi wamo na ndio wengi kuliko wanaume katika program hizo ambazo nimezitaja.

Kuhusu ukumbi wa Bwawani sisi pia haliturudhishi, lakini niseme tu kwamba kuna kampuni ya Kichina imeni- *approach* kwamba wangependa kupewa eneo lile ili walifanyie kazi. Nilichowajibu ni kwamba wakafanye *proposal* yao wanataka kufanya nini, kwa gharama zipi, aina gani, eneo gani wanahitaji halafu tutakuja kujibu hapo mbele tukapomalizana na hawa.

Masuala ya uchafu wa Mji Mkongwe na mambo mengine tutayafanyia kazi. Suala la Kalos wa Chokocho hayupo ameondoka na pale sasa hivi hakuna *activities* inayoendelea lile boti lipo tu pale na ZIPA wanaufanyia kazi mradi huu aidha kuufuta au kumpa muwekezaji mwengine.

Lakini pia kulikuwa kuna suala la Muyuni ya Matemwe. Muyuni ya Matemwe alipewa muwekezaji wa Dubai anaitwa Would Tourism lakini pamoja na IFA. Muwekezaji huyu alikuwa tayari kufanya kazi, kwa bahati mbaya mwaka juzi wakakubwa na suala la *prices* ya fedha na Dubai ilikuwa CVLI *damaged* wakatuandikia barua wakaomba *recession* ya mwaka mmoja kwamba waji-*recover* halafu waje tena kujiandikia.

Mwaka mmoja umepita 2009 hatukuwaona na muda walioomba umekwisha, juzi tu ZIPA wamewaandikia barua *copy* imekuja kwangu kutakiwa kueleza je, bado wana niya ya kuwekeza au eneo tumpe mtu mwengine. Kwa hivyo hilo nalo tunalijua na tunalifanyia kazi.

Mhe. Spika, naona yale makubwa makubwa nimejitahidi kuyajibu. Kulikuwa kuna suala la Kiweni Resourt la Mhe. Hija ambalo amesema amelifikisha kwa ZIPA lakini bado hawajampa jawabu. Mhe. Hija naomba aniachie mimi nitalifatia kwa ZIPA na utapata jawabu rasmin aidha wataendelea kulipwa au vyenginevyo.

Mhe. Spika, naomba nimalizie na suala la Shirika la Magari kwa nini hawalipi fedha za Mkaguzi. Ni kweli kulikuwa na tatizo hilo na Shirika la Magari waliacha kulipa kwa sababu wao wenyewe walikuwa wanaidai hiyo Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu milioni 9.7 waliingiana kazi huko Shirika likalipa lakini Idara ya Mkaguzi hawakuweza kurudisha.

Lakini hata hivyo inaelekea Shirika la Magari lilishindwa kwa hoja wamelipa deni lote isipokuwa kuna deni kipindi cha 2008/2009 tu ndilo halijalipwa. Lakini tutahakikisha na hili tunalilipa.

Mhe. Spika, nashukuru naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji basi waheshimiwa wajumbe wale wanaokubaliana na hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Utalii Biashara na Uwekezaji wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utalii, Biashara na

Uwekezaji. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara hii.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 21 WIZARA YA BIASHARA UTALII NA UWEKEZAJI

Kifungu 06	Idara ya Biashara
	23,525,000
Jumla ya Fungu	
	23,525,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 31 KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 02 Utawala Unguja

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, sina niya ya kuharibu wala kutia dowa kwa sababu maelezo niliyoyapata kwa Mhe. Waziri ni mazuri mno. Alisema kwamba atajitahidi kufatilia lakini kidogo tu nilitaka kusisitiza.

Kwa kuwa wananchi wetu hawajui kwamba *supplier* na hawa wanaweke mikataba kwa sababu *supplier* wenyewe wa kuokotea okotea. Ningeomba tu Mhe. Waziri akanihakikishia atawasaidia vipi kwa muda mdogo ili waone masikini kama wale hiyo hela yao wanaipata. Naomba maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Unauliza kwenye mapato, maana hii ni mapato.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mheshimiwa nimejaribu kuangalia sana katika vifungu vyote, Kamisheni ya Utalii sikuiyona nimeona hapa na pia imenibabaisha, kwa sababu ipo fungu 31 badala ya 21. Kwa vile hata kifungu hiki yape kingenipa maelezo kwa sababu naona kama jambo jipya.

Mhe. Mwenyekiti: Utakwenda kwenye Mipango na Sera ndio anayoongoza mambo yote. Sawa.

Kifungu 02 Utawala Unguja	805,800,000
Jumla ya Fungu	**805,800,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 21 WIZARA YA UTALII BIASHARA NA UWEKEZAJI

Kifungu 03 Afisi Kuu Pemba 163,407,000
Kifungu 04 Mipango na Sera

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa mipango na sera ili kupata yale maelezo ya awali ambayo nimemwambia Mhe. Waziri anisaidie ili niwe na *hope* ya kuona nikifika kule nionekane kama hiyo kazi nimeifanya na matumaini yapo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwanza ningemuomba Mheshimiwa Mwakilishi angeanza kuwasaidia hawa watu mapema mno na asingesubiri ndani ya Baraza la Wawakilishi, kwa sababu hawa watu wametokea jimboni kwake na yeye ndiyo mwenye jimbo ana wajibu wa kuyashuhulikia hayo.

Kwa upande wa Wizara yangu kama nilivyosema kwamba mwanasheria wa Kampuni na mwanashiria wangu wa ZIPA wanalifanyia kazi suala hili. Sisi kama Wazanzibari na waliodhulumiwa ni Wazanzibari hatutokubali kuacha watu hawa wakose haki yao kwa hivyo tutajitahidi kulifanyia kazi.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa mlaini sana lakini inavyoonekana kwamba Mhe. Waziri ananambia sijalishuhulikia. Lakini nimeitwa nimelishuhulikia na nilitegemea sana kwamba Afisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa itajitahidi mapema sana, lakini inaonekana kwa mbali wako watu hawapende liwe.

Kwa hivyo sasa namuomba Mheshimiwa yeye ndiye mwenye uwezo Kamisheni ya Utalii ndio yenye uwezo wa kutoa na kufuta leseni. Hivyo katika Mkoa wa Kaskazini hili suala sio hawa tu karibu ukanda mzima ina maana halijui. Na kama halijui wafanyakazi wake wanafanya kazi gani kwa sababu wapo maafisa ya Wilaya, Mkoa na hata Kamisheni yenyewe. Naomba bado Mheshimiwa alisaidie hili kwa sababu Wazanzibari hawajawa mafundi kwa kuweka mikataba hata hiyo ya *supplier* naomba atusaidie sote sio Matemwe tupu.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe.Mwenyekiti, sikukataa kusaidia. Nimesema Wizara yangu kupitia wanasheria tunalisaidia na wala sio Kamisheni ya Utalii kwa sababu hili ni suala la ZIPA. Nimesema tuko tayari

tutasaidia na wananchi wake wananisikia. Lakini mengine yalipaswa kufanyiwa kazi kabla leo. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mheshimiwa nimemsikia Mhe. Waziri na Ishallah tutalifanyia kazi pamoja lakini tunahitaji nguvuzao wao sana kwa sababu wao ndio wanaotoa leseni na wao ndio wenye uwezo wa kufuta leseni na halijaanza hapa. Naomba Mhe. Waziri alijue, hili ni uzembe wa watu ambao wananafasi hii lakini wanafanya ndivyo sivyo ili utalii wenyewe uchafuke. Naomba tuendelee na tutajitahidi kuwa pamoja ili kuona tunafika wapi.

Kifungu 04 Mipango na Sera	1,531,160,000
Kifungu 05 Idara ya Viwanda	72,196,000
Kifungu 06 Idara ya Biashara	172,237,000
Jumla ya Fungu	**1,939,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU - 31 KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 02 Utawala Unguja	603,531,000
Kifungu 03 Afisi Kuu Pemba	133,469,000
Jumla ya Fungu	**737,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU - 21 WIZARA YA UTALII BIASHARA NA UWEKEZAJI

Kifungu 04	Mipango na Sera	1,413,548,000
Kifungu 06	Idara ya Biashara	1,136,000,000
Jumla ya Fungu		**2,549,548,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirejea)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya

Utalii Biashara na Uwekezaji bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Naafiki.
Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na Makadirio hayo wanyanyue Mikono, Wanaokataa, waliokutali wameshinda.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunakushukuruni kuimaliza shughuli hii mapema hivi asubuhi na tulipanga ratiba yetu kutokana na hoja ambayo alitoa Mhe. Waziri hapa kwamba shughuli zetu ziendelee mpaka tarehe 7/7/2010, lakini kwa muelekeo huu inaonekana siku ile itakuwa mapumziko kama yalivyo. Kwa hivyo nilimuomba na amekubali Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi kwamba yeye aseme hotuba yake leo jioni, amenambia yupo tayari, nimetizama na Waziri Kivuli na yeye pia kanambia yupo tayari. Nilikuwa namtafuta Mhe. Nyonje yeye sijamuona lakini nimepeleka habari na yeye inaonekana yupo tayari.

Kwa hivyo jioni tutafanya marekebisho ya *Order paper* ya leo ili tuweze kuendelea na shughuli hiyo ili ituwezeshe kumaliza shughuli ya Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi kesho jioni. Hiyo itafanya kwamba wajumbe tuwape wasaa wa kuitumia saba saba yenu vizuri na pengine itakuwa imefidia nilivyosema jana tupumzike na wale wanaotaka kwenda Dodoma watakwenda kwa wasaa mzuri.

Baada ya hayo machache naahirisha Kikao hichi mpaka saa 11 jioni leo.

(Saa 6:15 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na

Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Zakiya Omar Juma (Kny: Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri Kivuli naomab kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetuwezesha kukutana hapa leo hii tukiwa wazima na wenye afya njema. Kadhalika napenda kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Amani Abeid Karume kwa juhudi zake alizozichukua za kuiongoza sekta ya mawasiliano na uchukuzi tokea wakati alipokuwa waziri wa wizara hii miaka ya 1995 – 2000. Chini ya uongozi wake wakati huo, mbali na hali ngumu ya fedha iliyoikabili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini akitumia juhudi na uhodari wake alihakikisha kuwa wizara inatekeleza majukumu yake katika sekta za barabara, anga, mawasiliano na bandari kwa ufanisi zaidi. Kwa kujua umuhimu wa sekta ya usafiri na mawasiliano Mhe. Amani mara tu baada ya kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar mwaka 2000 aliweka kipaumbele cha kwanza kuiendeleza sekta ya usafiri na mawasiliano.

Matokeo ya juhudi zake zilitusaidia sana kwa kuhakikisha kuwa wizara inapatiwa nyenzo na fedha za kutosha katika kutekeleza majukumu yake. Juhudi zake hizo zimezaa matunda kwa kuifanya sekta ya usafiri na mawasiliano ni moja kati ya sekta iliyopata maendeleo ya haraka zaidi hapa Zanzibar. Mhe. Dr. Amani amekuwa akitupatia ushauri na muongozo uliotusaidia sana katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa maendeleo ya sekta ya usafiri na mawasiliano. Bajeti ya mwaka huu wa 2010/2011 kwa upande wa wizara yangu ni maalum katika kuenzi juhudi za Mhe.Rais za kuleta maendeleo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka 10 ya uongozi wa Mhe. Dr. Amani Abeid Karume, wizara imeweza kutekeleza na kukamilisha ujenzi wa barabara 34 na jumla ya barabara 18 ujenzi wake unaendelea kwa Unguja na Pemba kama zinavyoonekana katika **kiambatanisho namba 1.** Kadhalika wizara imeweza kukamilisha miradi ya miundombinu ya Bandari ya Malindi, upanuzi wa bandari ya Wete, ujenzi wa bandari ya Wesha, matengenezo makubwa na utanuzi wa njia ya kurukia na kutulia ndege, kuimarisha huduma za usafiri wa barabarani, angani na baharini.

Kutokana na kupenda kwake maendeleo ya nchi yetu Mhe. Rais Dr Karume pia amewezesha kupatikana fedha za ujenzi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar. Ni katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Amani ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Mfuko wa Barabara kwa lengo la kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu. Naomba nikiri kwamba mfuko huo umekuwa na manufaa makubwa katika kuimarisha barabara zetu.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Dr Amani Abeid Karume kwa uongozi wake wa busara na hekima ambao umemuwezesha kuongoza nchi yetu ya Zanzibar kwa kipindi cha miaka kumi kwa amani na utulivu. Namshukuru sana Mhe. Rais kwa ujasiri wake wa kuleta muafaka wa kuwaunganisha Wazanzibari wote kuwa kitu kimoja. Utulivu na mshikamano unaoendelea katika nchi yetu wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu ni matokeo ya juhudi zake zenye lengo la kuwafungulia watu wa nchi hii ukurasa mpya wa maendeleo katika karne hii ya ishirini na moja.

Napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wafanyakazi wote wa wizara yangu kumpongeza na kumshukuru Mhe. Rais kwa utumishi wake uliotukuka kwa kipindi chote cha uongozi wake. Vile vile napenda nimpongeze Waziri Kiongozi wa Zanzibar Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na Naibu Waziri Kiongozi Mhe. Ali Juma Shamhuna kwa mashirikiano wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu ya kazi katika wizara yangu. Kadhalika naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuitekeleza kwa asilimia kubwa sana ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 hadi 2010 katika sekta ya Usafiri na Mawasiliano. Pia nachukuwa nafasi hii kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa kuliongoza Baraza lako tukufu kwa busara, hekima na uadilifu.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Anayeshughulikia Fedha na Uchumi D. Mwinyihaji Makame Mwadini ambaye hotuba yake imetoa mwelekeo wa kuimarisha miundombinu, maelezo ya hali ya uchumi, mipango ya maendeleo ya nchi yetu na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha wa 2010/2011. Kadhalika naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa maelekezo na ushauri uliosaidia kufanikisha shughuli za

wizara yangu. Naomba uniruhusu pia nimshukuru Waziri Kivuli wa wizara yangu Mhe. Omar Ali Shehe Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwa mashirikiano makubwa anayonipatia

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kuwa hiki ni kikao cha mwisho cha bajeti kabla ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2010. Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza hili kwa michango yao waliyokuwa wakiitoa kwa wizara yangu kwa muda wa miaka mitano iliyopita. Pia namshukuru Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Mzee Ali Ussi, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani kwa mashirikiano mazuri ya utekelezaji wa kazi za kila siku. Vile vile namshukuru Katibu Mkuu na Wakuu wa Taasisi na watendaji wote wa wizara yangu kwa kutekeleza vyema majukumu yao na hivyo kuifanya kazi yangu ya kusimamia na kuongoza sekta ya usafiri na mawasiliano kuwa nyepesi zaidi.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu niishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono na kunipa moyo katika utekelezaji wa kazi zangu. Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi na viongozi wenzangu wa Jimbo la Chumbuni kwa imani yao kwangu kunichagua kwa kishindo katika uchaguzi wa mwaka 2005. Ni matarajio yangu kuwa wataendelea kuniamini na kuwekeza kwangu kwa kunichagua tena kwa kipindi cha 2010 hadi 2015 ili niweze kuendelea kuwaletea maendeleo katika jimbo nami ninawaahidi sitowaangusha.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 wizara yangu ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 3,744,000,000 kwa kazi za kawaida na kupanga kukusanya jumla ya shilingi 1,500,000,000. Aidha, wizara ilipangiwa kutumia jumla ya shillingi 5,750,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi Machi 2010 jumla ya shilingi 2,543,847,930 zilipatikana sawa na asilimia 68 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,221,498,584.02 zimekusanywa sawa na asilimia 81 ya makadirio na vile vile jumla ya shilingi 5,176,264,620 sawa na asilimia 90 zilipatikana kwa kazi za maendeleo **(kiambatisho namba 2.)**

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO KWAMWAKA 2009 / 2010 NA MALENGO YA MWAKA 2010 / 2011.

Mhe. Spika, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inaundwa na Afisi Kuu Pemba, Idara ya Mipango na Sera, Idara ya Anga, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, Idara ya Usafiri na Leseni, Shirika la Meli na Shirika la Bandari.

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba inaratibu shughuli zote za sekta za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa upande wa Pemba. Katika kipindi cha 2009/2010 Afisi Kuu Pemba imetekeleza kazi mbali mbali za wizara kama inavyooneshwa kaitika uk 3

wa hotuba hii. Utekelezaji wa majukumu mengine yameelezwa katika maelezo ya sekta husika.

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ilitengewa jumla ya shilingi 1,024,673,000 kwa kazi za kawaida. Hadi Machi, 2010 fedha halisi zilizoingizwa ni Tsh 746,856,640 zikiwa ni sawa na asilimia 73. Afisi Kuu Pemba ilipangiwa kukusanya Jumla ya Tsh 82,300,000 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia Machi, 2010 Jumla ya Tsh 68,757,750.10 sawa na asilimia 84 ya mapato zilikuwa zimekusanywa.

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba kwa mwaka 2010/2011 inatarajia kutekeleza majukumu mbali mbali ya kazi za kawaida, kuajiri wataalamu wa fani mbali mbali, kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake na kuendelea kuzifanyia matengenezo nyumba zake Gombani na Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba.

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba kwa mwaka 2010/2011 inatarajia kukusanya jumla ya Tsh 90,500,000 na inaombewa jumla ya Tsh 1,100,418,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera ina jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera na mipango ya sekta ndogo za usafiri wa baharini, nchi kavu na anga.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 wizara ilikamilisha utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri wa Zanzibar (*Zanzibar Transport Master Plan*). Wizara imeanzisha kitengo maalum ambacho kitafanya shughuli zake kama zilvyoelezwa katika uk wa **8** wa hotuba hii. Aidha, wizara imo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kugeuza Afisi ya Mrajis wa Meli kuwa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (*Zanzibar Maritime Authority*) kama sheria inavyoelekeza.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi, 2010 wizara ilikamilisha kazi za utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Kiwanja cha Ndege (*Airport Master Plan*) na uchambuzi yakinifu wa jengo jipya la abiria (*feasibility study for terminal building*) katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar.

Mhe. Spika, wizara imeendelea kutekeleza masuala ya kiutumishi na uendeshaji kama inavyoelezwa katika ukurasa wa 9 wa hotuba hii. Kadhalika, wizara iliunda Kamati ya Kusimamia Shughuli za Udhibiti wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano zikiwemo simu, radio na kadhalika, kama inavyoelezwa katika uk **wa 9.**

Mhe. Spika, hali ya jengo la wizara hivi sasa ni chakavu na linahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa kwani linapunguza ari ya kazi miongoni mwa wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, ili kurekebisha hali hiyo na kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi wa Idara ya Mipango na sera, wizara imelazimika kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara. Hivi sasa wizara inasubiri kukabidhiwa kiwanja na mamlaka zinazohusika ili hatua za ujenzi ziweze kuanza. Kwa mwaka wa 2010/2011 wizara imepanga kutumia shs. 100 milioni kwa kazi hiyo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Idara ya Mipango na Sera ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi 642,749,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Fedha halisi zilizotolewa katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 ni shilingi 509,381,870 sawa na asilimia 79. Kwa upande wa mapato Idara ya Mipango ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 77,700,000 kupitia Afisi ya Mrajisi wa Meli. Hadi Machi, 2010 jumla ya shilingi 57,107,772.52 sawa na asilimia 73 ya mapato yalikusanywa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2010/2011, wizara kupitia Idara ya Mipango na Sera itaendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usafiri, na Mpango Mkuu wa Usafiri wa Zanzibar (*Zanzibar Transport Masterplan*) na kuendelea na utekelezaji wa kazi nyengine kama imnavyoelezwa katika uk wa **11.**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Idara ya Mipango na Sera inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 82,000,000 kwa kupitia Afisi ya Mrajisi wa Meli na inaombewa jumla ya shilingi 748,118,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara

Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ina jukumu la kuzijenga na kuzitunza barabara zote za Unguja na Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imezifanyia matengenezo barabara kadhaa za Mijini na Vijijini kwa kutumia fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara. Matengenezo hayo kama yanavyoonekana katika **Kiambatisho Nam.4**. Aidha, idara kupitia Mfuko wa Barabara imeweza kununua lami tani 1000 ambazo zitasaidia sana kuziweka barabara zetu katika hali nzuri.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo, wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kipindi cha mwaka 2009 / 2010 ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 10 ya ujenzi wa barabara. Kwa mwaka 2010 / 2011 wizara inakusudia kuiendeleza miradi hiyo na kutekeleza miradi 2 mipya. Kwa kuzingatia

kuwa Zanzibar ni visiwa viwili vikubwa hivyo kwa mwaka huu wa 2010/2011 miradi hiyo iliyopangwa ya ujenzi wa barabara ina jumla ya km 232 kati ya hizo km 181 sawa na asilimia 78 zitatekelezwa Pemba na km 51 sawa na asilimia 22 zitajengwa Unguja. Hivyo, kwa mwaka wa pili mfululizo wizara yangu imeelekeza nguvu na nyenzo zaidi katika uimarishaji wa miundombinu ya ujenzi wa barabara Kisiwani Pemba.

(i) Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu za Zanzibar.

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Kwa mwaka 2009/2010 mradi huu ulikusudia kukamilisha kazi za ujenzi wa barabara zilizosalia za Mazizini-Fumba, Amani-Dunga, na Mfenesini-Bumbwini. Hatua za utekelezaji ni kwamba barabara ya Mazizini-Fumba imekamilika na kuzinduliwa katika sherehe za kuadhimisha miaka 45 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kuhusu barabara ya Amani –Dunga mkandarasi anaendelea na kazi na hadi sasa jumla ya km 3 zimeshajengwa kwa kifusi pamoja na *"culvert" 6 na "box culvert"* moja. Aidha, kwa barabara ya Mfenesini – Bumbwini kazi za matayarisho ya ujenzi wa barabara hiyo yanaendelea vizuri.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa barabara zilizosalia katika mradi huu na jumla ya shilingi billioni 1.8 zinaombwa kutoka Serikalini.

(ii) Mradi wa Barabara za vijijini Kusini Pemba
(South Pemba Rural Roads).

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Norway ambao unajumuisha ujenzi wa barabara za Mtambile – Kengeja – Mwambe (9.4 km), Kenya – Chambani (3.2 km), Mizingani – Wambaa (10 km), Chanjamjawiri – Tundaua (10 km), Chanjaani – Pujini (5 km) na Mtambile – Kangani (6.2 km). Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia mfumo ambao umeelezwa katika uk **wa** 14 wa hotuba yangu.

Mhe. Spika, mradi huu umeanza kwa ujenzi wa barabara 2 za Mtambile – Kengeja- Mwambe ambapo tayari kazi za ujenzi wa kifusi kwa barabara hiyo zimekamilika pamoja na *"culverts" 9 na "drift" 4.* Kazi za uwekaji "base" inaendelea na jumla ya km 3.0 zimekamilika kati ya hizo km 1.3 zimeshawekwa lami. Kwa upande wa barabara ya Mtambile – Kangani kazi za usafishaji zimekamilika na jumla ya km 2 zimeshajengwa kwa kifusi. Ujenzi wa barabara zilizosalia utafuata mara baada ya ujenzi wa barabara hizi kufikia hatua nzuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 wizara itaendelea kutekeleza mradi huu na jumla ya shilingi milioni 300 zinaombwa kutoka Serikalini.

(iii) Mradi wa Barabara 3 za Pemba

Mhe. Spika, mradi huu unaogharimiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (*Saud Fund*) na unazihusisha barabara za Chake – Wete (24 km), Wete – Konde (15.1 km) na Wete – Gando (13.6 km). Mradi huu kwa awamu ya kwanza unatekelezwa kwa kujenga barabara ya Wete - Konde na Wete – Gando ambapo hatua iliyofikiwa ni kuwa Mkandarasi Kampuni ya Mecco ameshaanza kazi na jumla ya km 14 za barabara ya Wete – Konde zimeshasafishwa na kati ya hizo km 6 zimeshajengwa kwa kifusi. Aidha, kwa upande wa barabara ya Wete – Gando kazi za upimaji zimekamilika na kazi za usafishaji zimeanza. Kuhusu barabara ya Wete – Chake imepangwa kutekelezwa katika awamu ya pili.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara hizo na jumla ya Shilingi Milioni 900 zinaombwa kutoka Serikalini.

(v) Mradi wa Barabara ya Ole-Kengeja

Mhe. Spika, huu ni mradi unaogharimiwa na Jumuiya ya Nchi Zinazosafirisha Mafuta kwa Wingi Duniani (*OPEC*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao una lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Ole hadi Kengeja yenye urefu wa kilomita 35. Tathmini za zabuni za ujenzi kwa barabara hiyo na usimamizi zimeshakamilika na ripoti zake zimeshatumwa *OPEC* kwa uamuzi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wizara inakusudia kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo na jumla ya shilingi milioni 100 zinaombwa kutoka Serikalini.

(vi) Mradi wa barabara za Vijijini Kaskazini Pemba (*North Pemba Rural Roads*)

Mhe. Spika, mradi huu unagharimiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Marekani kwa kupitia mfuko wake wa Akaunti ya Changamoto ya Millenia una lengo la kuzijenga kwa lami barabara za Kaskazini Pemba zenye jumla ya urefu wa kilomita 35. Barabara hizo ni Mzambarauni – Pandani – Finya (8.3km), Bahanasa – Daya – Mtambwe (13.1km), Mzambarauni – Mapofu (8.3km), Chwale – Kojani(2km) na Kipangani – Kangagani (3km).

Mhe. Spika, hatua zilizofikiwa ni kuwa kazi za kufanya uchambuzi yakinifu na usanifu *"feasibility study and detailed design"* zimekamilika na tathmini ya nyumba na mimea itakayoathirika zimekamilika. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea na matumaini yetu ni kuwa kazi za ujenzi zitaanza ifikapo mwezi wa Septemba 2010.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wizara inakusudia kutekeleza ujenzi wa barabara hizo na gharama zote za ujenzi zitagharamiwa na Mfuko wa Akaunti ya Changamoto wa Milenia (*MCC*)

(vii) Mradi wa Barabara ya Mgagadu – Kiwani

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na una lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mgagadu hadi Kiwani yenye urefu wa kilomita 7.6 kwa kiwango cha lami. Hatua ya utekelezaji wa mradi huu ni kuwa kazi za usafishaji zimeshakamilika na km 3 zimeshajengwa kwa kifusi ikiwemo kurekebisha sehemu zenye milima na mabonde.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wizara inakusudia kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo na jumla ya Shilingi milioni 350 zinaombwa kutoka Serikalini.

(viii) Barabara ya Pale – Kiongele

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ulikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Pale - Kiongele hadi Mkwajuni yenye urefu wa kilomita 11**.** Hatua za utekelezaji ni kwamba wizara imetiliana saini mkataba na Mkandarasi kwa ajili ya kujenga *culvart* katika barabara hiyo kazi ambayo tayari imeshaanza.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na jumla ya Tshs millioni 100 zinaombwa kutoka Serikalini kwa ujenzi wake. Katika kuweka nguvu za ujenzi wa barabara hii jumla ya shilingi milioni 100 pia zimeombwa kutoka Mfuko wa Barabara hivyo jumla ya shilingi milioni 200 zinatarajiwa kutumika kwa mwaka huu wa fedha kwa barabara hiyo.

(ix) Barabara ya Mkanyageni – Kangani

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ulikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Kangani hadi Mkanyageni yenye urefu wa kilomita 6.5 kwa kiwango cha lami. Hakuna hatua za utekelezaji kwa kipindi kilichopita kwani ujenzi wake unatarajiwa kuanzwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mgagadu – Kiwani.

Kwa mwaka wa fedha 2010/2011wizara inakusudia kuanza ujenzi wa barabara hii na jumla ya Shilingi milioni 50 zinaombwa kutoka Serikalini.

(x) Barabara ya Mpendae - Nyumbambili

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ulikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mpendae hadi Nyumba mbili yenye urefu wa kilomita 1.5 kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hiyo umeshaanza na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mradi huu utatekelezwa kwa kutumia fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa barabara kwa ajili ya kuweka lami.

(xi) Mradi wa Barabara ya Benjamini W.Mkapa (Amani /Mtoni).

Mhe. Spika, huu ni mradi mpya, wenye lengo la kujenga sehemu ya pili ya barabara ya Amani - Mtoni ambayo kukamilika kwake kutawezesha gari kutoka Mtoni kwenda Amani na zile zinazotoka Amani Kwenda Mtoni kutumia barabara mbili tofauti (*double carriage way*). Mradi huo unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutokana na ahadi iliyotolewa na Rais Mstaafu wa awamu ya tatu Mhe. Benjamini William Mkapa wakati wa ufunguzi wa awamu ya kwanza ya Barabara hiyo.

(xii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Maeneo huru Fumba (*Fumba ring road).*

Mhe. Spika, mradi huu ni mpya ambao unakusudia kuijenga kwa lami barabara inayopita sehemu za Ukanda wa Maeneo Huru Fumba kwa urefu wa km 10.4. jumla ya shilingi bilioni 2 zinaombwa kutoka Serikalini kwa ajili ya Ujenzi huo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi, 2010, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ilitengewa jumla ya shilingi 961,094,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Fedha halisi zilizotolewa kwa kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 ni shilingi 636,419,540 sawa na asilimia 66 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara inakusudia kutekeleza na kusimamia miradi mbali mbali ya ujenzi wa barabara pamoja na kuzifanyia matengenezo barabara kadhaa za mijini na vijijini Unguja na Pemba kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kama zinavyoonekana katika **kiambatisho namba 4** Sehemu B. .

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara inaombewa jumla ya shilingi 1,070,683,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Idara ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia usalama kwa watumiaji wote wa barabara kwa kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji madereva na walimu wa skuli za udereva. Aidha, idara hudhibiti utoaji huduma za usafirishaji abiria, mizigo kwa njia ya barabara, kuendesha na kusimamia Karakana Kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010 Idara ya usafiri na leseni imendelea na shughuli zake za kawaida za ukaguzi wa vyombo, upashajaji wa madereva, matengenezo ya magari na utoaji ruhusa njia. Utekelezaji wake imeelezwa katika ukurasa wa 11.

Mhe. Spika, idara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 310,000,000 na hadi Machi 2010 ilikusanya jumla ya shilingi 228,725,500 sawa na asilimia 74. Kwa upande wa matumizi, idara ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi 406,440,000 na hadi Mach,i 2009 fedha iliyopatikana ni shilingi 177,381,900 sawa na asilimia 44 ya makadirio.

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Idara ya Usafiri na Leseni ilitekeleza na kukamilisha mradi mmoja wa maendeleo wa ujenzi wa uzio unaozunguka eneo la Karakana kuu ya Serikali ili kuimarisha ulinzi na usalama katika sehemu hiyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Idara ya Usafiri na Leseni inatarajia kusimamia vizuri kazi zake hasa katika kuimarisha usafiri wa barabarani. Kwa kupitia Bodi ya Usafiri Barabarani idara itawapatia elimu watumiaji wa barabara, kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya moto, kuimarisha Karakana Kuu pamoja na kuipatia vifaa, kuhakikisha kwamba Bodi ya Usafiri barabarani inafanya kazi zake kama inavyotakiwa na sheria pamoja na kuendeleza matengenezo ya Afisi kuu ya Idara.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Idara ya Usafiri na Leseni inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 345,000,000 na inaombewa jumla ya shilingi 384,363,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika, sekta binafsi inamchango mkubwa katika usafiri wa nchi kavu hasa kwenye utoaji wa huduma za usafiri wa barabarani. Hata hivyo, licha ya sekta binafsi kutoa mchango mkubwa katika sekta ya usafiri wa barabarani maumbile yake na hali ya uendeshaji wake hapa Zanzibar imekuwa chanzo cha changamoto nyingi zinazoikabili sekta hiyo hivi sasa. Wizara yangu inaandaa mbinu za kukabiliana na changamoto hizo kwa kushirikiana na taasisi nyengine za usimamizi ili kuongeza usimamizi na utekelezaji wa sheria na kutoa mafunzo kwa madereva na makondakta na elimu ya usalama kwa umma.

Mhe. Spika, naomba nikiri kuwa kwa upande wa ujenzi na utunzaji wa barabara bado kumekuwa na mchango mdogo wa sekta binafsi hasa kwa Wazanzibari. Kazi nyingi zinazofanyika zinahusisha wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara au makampuni kutoka nje ya Zanzibar. Hivi karibuni wizara yangu imetiliana saini na Kampuni ya Sogea Satom ya Ufaransa mkataba wa kuzifanyia matengenezo barabara za mjini Unguja ambazo ni Miembeni – Kidongo chekundu, Kilimani – Kariakoo, Maisara – Bwawani, Uwanja Ndege wa Zamani – Kiembesamaki na Barabara za ndani za jengo jipya la Baraza la Wawakilishi liliopo Chukwani. Matengenezo hayo yanategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Julai 2010.

Idara ya Anga

Mhe. Spika, Idara ya Anga imepewa jukumu la kusimamia maendeleo ya usafiri wa Anga Zanzibar pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: (anaendelea**)** Zanzibar pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/10 Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Idara ya Anga imetekeleza kazi mbali mbali za kawaida za kuhudumia ndege, abiria na mizigo. Viwanja vya Unguja na Pemba vimehudumia jumla ya ndege 33,392 ikilinganishwa na ndege 33,203 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha 2008 - 2009. Kati ya ndege hizo, ndege 29,964 zilihudumiwa katika kiwanja cha Kimataifa cha Zanzibar na ndege 3,428 zilihudumiwa katika kiwanja cha Karume Pemba. (**kiambatisho namba 8** Sehemu A.**)**

Mhe. Spika, **i**dadi ya abiria waliohudumiwa katika viwanja vya ndege vya Zanzibar kuanzia mwezi Julai 2009 hadi Machi 2010 ilikuwa ni 479,142 ikilinganishwa na abiria 454,133 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2008 /2009. Kati ya abiria hao, abiria 451,878 walihudumiwa katika Kiwanja cha Kimataifa cha Zanzibar na abiria 27,864 walihudumiwa katika Kiwanja cha Karume Pemba. Aidha, abiria waliopita (*transit*) katika viwanja vyetu wamefikia 60,611. Takwimu hizo zinaonyesha kwamba kumekuwepo na ongezeko la idadi ya abiria waliohudumiwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2008/09. (**kiambatisho namba 8** Sehemu B**.)**

Mhe. Spika, Kwa upande wa mizigo (*freight*) ikijumuishwa na vifurushi vya posta, jumla ya kilogramu 624,140 zilihudumiwa katika viwanja vyetu vya ndege vya Unguja na Pemba ikilinganishwa na kilogramu 557,557 zilizohudumiwa kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, kuanzia Julai, 2009 hadi Machi, 2010, idara imekusanya mapato halisi ya jumla ya shilingi 866,907,561.42 sawa na asilimia 84 ya makadirio. Mapato hayo yamekusanywa kutokana na ada za utuaji ndege kiwanjani (*landing fees*), kodi za ofisi (*rents*), makusanyo ya madeni ya nyuma na mapato mengineyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 Idara ya Anga ilitengewa jumla ya shilingi 709,044,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Fedha halisi zilizotolewa kwa kipindi cha Julai 2009, hadi Machi 2010 ni shilingi 473,807,980 sawa na asilimia 67 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo sekta ya anga ilipangiwa miradi 3 kwa mwaka wa 2009/2010. Kwa mwaka 2010/2011 idara inatarajia kuendeleza miradi hiyo na kuongeza mmoja mpya.

i) Mradi wa barabara ya kurukia na kutulia ndege

Mhe. Spika, mradi huu unagharimiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Dunia una lengo la kuijenga barabara ya kutulia na kurukia ndege ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar pamoja na kuongeza urefu kutoka mita 2,462 ziliopo hivi sasa hadi kufikia mita 3,022. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 utekelezaji wa mradi huu ni kuwa Mkandarasi Kampuni ya *SOGEA SATOM* amekamilisha kazi za ujenzi wa sehemu ya uwanja iliyotanuliwa yenye urefu wa mita 560. Aidha, kazi ya matengenezo makubwa ya uwanja wenye urefu wa mita 2462 nayo imekamilika, kwa kuwekewa lami na kuufanya uwanja wa ndege wa Zanzibar kuwa na urefu wa mita 3022. Kadhalika nguvu (*strength*) ya kiwanja imeongezeka kutoka nambari 41 hadi kufikia nambari 61. Kazi zilizobakia ni pamoja na kazi za mitaro na kukamilisha kazi za uwekaji umeme katika njia hiyo ya kurukia na kutulia ndege. Kazi hizi zinategemewa kukamilika mwezi Julai 2010 na hivyo kuufanya mradi huu kukamilika mapema kabla ya muda uliopangwa yaani tarehe 15 Agosti 2010.

Mhe. Spika, mradihuu unatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 4 Agosti, 2010 na Mhe. Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, serikali ilikubaliana na Benki ya Dunia kuwa, Benki igharamie mradi wa huu utanuzi na matengenezo ya uwanja wa ndege kwa asilimia 100 na serikali igharamie kazi za ujenzi wa uzio. Serikali kupitia wizara yangu, inaendelea na kazi za ujenzi wa uzio huo kwa kutumia fedha zake wenyewe na kwa mwaka 2010/2011 wizara itaendelea na kazi hiyo ambayo inaombewa jumla ya Shilingi Bilioni 3 kutoka serikalini.

ii) Kuimarisha huduma za viwanja vya ndege

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kulifanyia matengenezo makubwa jengo la makao makuu ya Idara ya Anga, uwekaji taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege kiwanja cha ndege cha Karume - Pemba na kujenga uzio katika kiwanja hicho.

Mhe. Spika, hatua za utekelezaji ni kwamba kazi ya kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Makao Makuu ya Idara ya Anga kwa awamu ya mwanzo imekamilika. Kazi za ujenzi wa uzio katika kiwanja cha Karume kwa urefu wa kilomita 1 zinaendelea na malipo ya fidia za nyumba za wananchi na mimea katika eneo la kiwanja hicho yameshafanyika.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za uwekaji wa taa kwa kiwanja cha ndege cha Karume Pemba, Wizara kwa kupitia idara tayari imeshafanya mazungumzo na Kampuni ya *Siemens* kufanya utafiti wa kujuwa gharama za uwekaji taa na mahitaji halisi ya kazi hiyo. Kazi hiyo ya uwekaji wa taa inatarajiwa kufanyika kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) baada ya kukamilika kwa taratibu za kupata fedha katika benki hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 20010/2011 wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi huo wa uzio ambapo jumla ya shilingi milioni 70 zinaombwa kutoka serikalini.

iii) Ununuzi wa Vifaa Kupitia Fedha za Msamaha wa Madeni kwa Tanzania (*MDRI*).

Mhe. Spika, mradi ulikuwa na lengo la ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya uimarishaji huduma katika viwanja vya ndege kwa kutumia fedha za msamaha wa madeni (*MDRI*). Taratibu za zabuni za manunuzi ya vifaa hivyo zimekamilika na ripoti imewasilishwa Wizara ya Fedha kwa hatua za manunuzi ya trekta na jenereta la akiba.

iv) Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria

Mhe. Spika, huu ni mradi mpya wenye lengo la kujenga jengo jipya la abiria pamoja na kuweka huduma na vifaa mbali mbali katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Zanzibar. Kwa sasa serikali imeshakamilisha taratibu za kupata mkopo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia *Exim Benk*. Aidha mkataba wa Ujenzi umeshasainiwa kati ya Serikali na Kampuni ya *"Beijing Construction Engineering Group"* kutoka China. Kazi zinategemewa kuanza ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 yaani tunategemea mwisho

wa mwezi wa Julai kati hiyo itaanza. Serikali ya Zanzibar itagharamia shughuli za usimamizi wa ujenzi huo.

Mhe. Spika, wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa jengo hilo na jumla ya Shilingi milioni 300 zimeombwa kutoka serikalini kwa ajili ya kumlipa msimamizi wa ujenzi huo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, wizara yangu kupitia Idara ya Anga inakusudia kuimarisha huduma mbali mbali za viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba ili ziweze kukidhi mahitaji ya wateja wa ndani na nje. Aidha, idara itaendelea kuongeza mashirikiano mazuri na wadau wa sekta ya usafiri wa Anga kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 idara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 1,130,000,000. Ili kutekeleza shughuli zake kama ilivyopangiwa idara inaombewa jumla ya shilingi 763,418,000 kwa ajili ya kazi za kawaida kwa mwaka 2010/2011.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Mhe. Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu ya Serikali ya Muungano ya Tanzania ambayo ina tawi lake hapa Zanzibar. Taasisi hii ina jukumu la kutoa taarifa za utabiri wa hali ya hewa kwa kila siku. Kadhalika mamlaka hutoa tahadhari na matukio ya hali ya hewa hapa nchini.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2009/2010 Mamlaka iliendelea kutoa taarifa za utabiri wa hali ya Hewa za kila siku kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar, *Zenj FM* na TVZ na tabiri za msimu (*Seasonal wheather forecasts*) kwa maandishi kupitia taasisi mbali mbali za vyombo vya habari vinavyohusika. Aidha Mamlaka iliendelea kutoa huduma zake katika sekta mbali mbali zikiwemo sekta ndogo za usafiri wa anga, bahari, kilimo, taasisi nyengine za Serikali na watu binafsi.

Mhe. Spika, Mamlaka bado haikuweza kutekeleza ahadi zake za kufungua kituo cha hali ya hewa bandarini Zanzibar na kujenga Afisi za Mamlaka huko Pemba kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo ukosefu wa fedha. Hata hivyo Mamlaka iliweza kuwasomesha masomo ya juu wataalamu wake 5 katika vyuo vikuu vya Nairobi, Dar es Salam, Chukwani na Chuo cha hali ya hewa Kigoma.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Mamlaka itaendelea na huduma zake za kawaida na kuziboresha kwa kuongeza nyenzo za mawasiliano zinazotumia teknolojia ya kisasa na vitendea kazi. Aidha, mamlaka bado ina azma ya kutaka

kuanza kutoa huduma kwa vyombo vya Baharini kutoka kwenye Afisi yake inayotarajiwa kujengwa bandarini Unguja na pia kulifanyia ukarabati mdogo jengo lake hapo Uwanja wa Ndege Zanzibar.

Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga

Mhe. Spika, Mamlaka ya usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Miundo mbinu ya Serikali ya Muungano wa Tanzania ambayo inatoa mchango mkubwa katika sekta ya Usafiri wa Anga hapa Zanzibar. Taasisi hii ina jukumu la kusimamia mambo yote yanahusu taratibu za usalama wa usafiri wa anga Tanzania. Taratibu hizo zinafuata mfumo uliowekwa na kukubalika na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia na kuratibu safari za Anga Duniani (*ICAO*).

Mhe. Spika, *k*atika kipindi cha 2009/2010 Mamlaka imeendelea kusimamia usalama katika safari za anga kwa kutumia taratibu zilizowekwa na kwa uharaka. Sekta za safari za anga zimeboreshwa na usalama wake umeendelea kuimarishwa.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha 2010/2011 mamlaka inakusudia kuifanyia vipimo vya angani (*flight checks*) mitambo muhimu ya kuongozea ndege (*CVOR/DME*) iliyopo kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Zanzibar kwa ajili ya kuziwezesha ndege zinazotumia mitambo hiyo kutua na kuruka katika kiwanja chetu kwa uhakika na usalama zaidi. Aidha, mamlaka inatarajia kuweka meza ya kisasa ya kuwekea vyombo vya kuongozea ndege (*ATC Console*) kwenye chumba cha kuongozea ndege (*Control Tower*) katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Zanzibar.

MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

Mhe. Spika, sekta binafsi inatoa mchango mkubwa katika kusadia juhudi za serkali za kuendeleza na kuimarisha usafiri wa anga hapa Zanzibar. Sekta hii inachangia katika usafirishaji abiria na mizigo, utoaji huduma za upakizi na upakuwaji wa mizigo katika ndege, utoaji wa huduma za mafuta kwa ndege na huduma nyengine ndogo ndogo za chakula na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 kampuni mbali mbali za ndani na nje ya nchi ziliendelea kutumia viwanja vyetu vya ndege. Kampuni hizo ni kama zinavyoonekana katika **kiambatanisho namba 9.** Wizara itaendelea kuongeza ushirikiano na makampuni hayo ili kuimarisha na kurahisisha huduma za usafiri wa anga.

V. SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI

Mhe. Spika, katika sekta ya usafiri wa Baharini Wizara yangu ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya usafiri wa baharini katika Zanzibar kwa kuweka miundo mbinu ya bandari, kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na kusimamia usalama wa watu na mali zao pamoja na mazingira ya baharini yasichafuliwe. Majukumu haya yanatekelezwa na Afisi ya Mrajis wa Meli, Shirika la Bandari, Shirika la Meli, pamoja na kampuni za watu binafsi ambazo zimewekeza na kutoa huduma katika sekta hii.

Afisi ya Mrajis wa Meli

Mhe. Spika, Afisi ya Mrajis wa Meli ni kitengo kilichoazishwa kwa ajili ya kushughulikia na kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri wa baharini na masuala ya mabaharia kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Baharini ya mwaka 2006.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010, Afisi ya Mrajis ilishasajili jumla ya meli 7 zenye uzito wa *GRT* 4,474 na hivyo kufikisha jumla ya meli 71 katika usajili wa meli za ndani zenye uzito wa *GRT* 36,902. Aidha jumla ya vyombo vidogo vidogo 45 vilikaguliwa na kupewa leseni. Katika usajili wa meli kubwa chini ya mradi wa usajili wa wazi (*Open Registry*) jumla ya meli 47 zenye uzito wa *GRT* 217,399 zimesajiliwa. Afisi ya Mrajisi wa Meli iliendelea na kazi za utungaji wa kanuni za uendeshaji wa meli (*manning*) ambazo tayari zimeshakamilika katika hatua ya rasimu ya mwanzo.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho kitengo kiliendelea na shughuli za kuwafanyia mitihani manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo ambapo jumla ya watahiniwa 14 wamepatiwa vyeti. Aidha, kitengo kilitoa vitabu vya ubaharia (*discharge book*) 88 na vitambulisho vya kimataifa vya Ubaharia '*Sea farer's Identity*" 37.

Shirika la Bandari

Mhe. Spika, Shirika la Bandari linatoa mchango mkubwa katika kuimaarisha Sekta hii ya Usafiri wa Baharini. Shirika hili lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usalama wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na usimamizi wa usalama wa usafiri ndani ya maeneo ya bandari hizo. Shirika pia linawajibu wa kuhifadhi mizigo na utunzaji wake katika Bandari pamoja na kuvifanyia

matengenezo madogo madogo vyombo mbali mbali vya usafiri wa Baharini kwa kutumia Karakana yake kuu ya Malindi.

Mhe. Spika, shirika liliendelea na kazi zake za kutoa huduma mbali mbali zikiwemo kuhudumia vyombo vya baharini, mizigo na abiria pamoja na vyombo vya usalama baharini. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, Shirika liliweza kutoa huduma kama ifuatavyo:-

Vyombo vya Kigeni:

Mhe. Spika, jumla ya meli za kigeni zilizoingia katika Bandari ya Zanzibar ni 124 ikiwa ni upungufu wa meli 15 sawa na asilimia 11 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kilichopita. Meli hizo zina uzito wa ujazo (*GRT*) wa Tani 1,300,356.22 ikiwa ni ongezeko la *GRT* 577,746 sawa na asilimia 80. Kati ya meli hizo, meli za mizigo mchanganyiko 20, meli za makontena 64, za Kitalii ni 5, Meli nyenginezo ndogo ndogo 10 na meli 25 za mafuta (*tankers*). Aidha kati ya meli za mafuta, 6 zenye ujazo wa (*GRT*) wa tani 6,275 zilipokelewa Pemba.

Meli za Ndani (nchini)

Mhe. Spika, meli za ndani (zilizosajiliwa nchini) zilifanya safari mara 3,892 ambapo safari 2,884 zilihudumiwa katika Bandari ya Malindi Unguja na safari 1008 zilihudumiwa katika Bandari za Pemba (Wesha, Wete, na Mkoani).
vyombo vya kienyeji (Majahazi na Maboti) vilifanya safari 2,231 ambapo vyombo 1,287 vilihudumiwa katika Bandari za Unguja na 944 katika Bandari za Pemba. Idadi hiyo ya vyombo vya kienyeji ni sawa na asilimia 93.43 ya vyombo vilivyohudumiwa katika kipindi kilichopita cha Julai, 2008 hadi Machi, 2009. **Kiambatanisho namba 10 S**ehemu A.

Mizigo Mchanganyiko

Mhe. Spika, Bandari ya Unguja ilihudumia bidhaa mbali mbali (*General Cargo*) zenye uzito wa tani 72,765.90. Mbali na hizo tani 64,741 za aina mbali mbali za mafuta ziliteremshwa katika Bandari ya Mtoni. Idadi hiyo ya mizigo (T. 72,766) ni upungufu wa asilimia 57 ya mizigo ya aina hiyo iliohudumiwa katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009 kutokana na mabadiliko ya mfumo wa usafirishaji. Aidha, bandari za Pemba zimehudumia jumla ya tani 20,869.03 za mizigo aina mbali mbali pamoja na tani 7,493.56 za mafuta ya kuwasha yalioteremshwa katika Bandari ya Wesha.

Makontena

Mhe. Spika, Bandari ya Unguja imehudumia makontena 19,652 (sawa na *Teus* 24,572) yaliyowasili na kusafirishwa kwenda nje ya Zanzibar. Idadi hiyo ni ongezeko la makontena 5,955 sawa na asilimia 44 ikilinganishwa na kipindi kilichopita (Julai, 2008 – Machi, 2009) ambapo makontena 13,674 (sawa na *Teus* 17,857) yalihudumiwa. Aidha, makontena 11 sawa na Teus 11 yalihudumiwa katika Bandari ya Pemba.

Mzigo wa majahazi

Mhe. Spika, jumla ya tani 63,201.46 za mizigo mbali mbali (chakula, vifaa vya ujenzi, vinywaji n.k) zilihudumiwa katika gati za majahazi ikiwa ni ongezeko la tani 3,181.03 (5%) ikilinganishwa na kipindi kilichopita (Julai, 2008 hadi Machi, 2009). Tani 10,794.57 zilihudumiwa katika Bandari za Pemba. **Kiambatanisho namba 10** Sehemu B.

Huduma za Abiria

Mhe. Spika, Kwa upande wa abiria, Shirika lilihudumia jumla ya abiria 1,360,279 waliosafiri kwa vyombo vilivyosajiliwa nchini, ambapo kati yao abiria 1,058,054 walitumia Bandari ya Malindi (Unguja) na 302,225 walitumia Bandari za Pemba (Mkoani na Wete). Aidha Shirika lilihudumia wageni (watalii) wapatao 3,633 waliowasili na kusafiri kwa meli za Kitalii (Cruise Ships).

Kazi za kiufundi:

Mhe. Spika, Shirika limefanikiwa kufanya kazi mbali mbali za kiufundi zikiwemo matengenezo ya vyombo vya baharini vinavyomilikiwa na Shirika lenyewe, pamoja na vyombo vyengine vilivyohitaji huduma za Shirika (Chelezo). Kadhalika kazi kadhaa za uchongaji wa vipuri kwa vitendea kazi vya bandarini zimefanyika katika karakana hizo za Shirika.

Mhe. Spika, Shirika kupitia Kitengo chake cha Maboya, limeweza kuyafanyia matengenezo maboya pamoja na minyororo yake, yakiwemo maboya ya "*solar*" na maboya yasiyokuwa na taa (bubu) **Kiambatisho namba 10** Sehemu C. kinahusika. Katika kipindi hicho Shirika limeweza kulifanyia matengenezo jengo la abiria katika Bandari ya Wete baada ya kuporomokewa na tope zilizopelekea uharibifu kwa baadhi ya sehemu za Jengo hilo. Vile vile shirika limeufanyia matengenezo Mnara wa Nungwi pamoja na nyumba ya walinzi.

Mhe. Spika, Shirika kupitia Kiwanda chake cha Mvuke (*Gas Station*) kiliweza kuzalisha chupa 46 za gesi kwa kutumia mali ghafi ya *"culcium carbide"* yenye uzito wa kilogram 1500. Jumla ya minara 10 iliwashwa kwa kutumia gesi hiyo.

Uzalishaji wa gesi kwa kipindi hichi umekuwa mdogo kutokana na tatizo la kukosekana umeme kwa miezi mitatu.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009, hadi Machi, 2010, shirika lilipanga kutekeleza jumla ya miradi saba ya maendeleo pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma zake. Mhe. Spika, miradi yenyewe ni kama ifuatayo:-

Ujenzi wa Jengo la Abiria katika Bandari ya Malindi

Mhe. Spika, lengo la Mradi huu ni kujenga jengo la abiria ikiwa ni hatua za uimarishaji wa huduma za abiria katika Bandari ya Malindi. Shirika limefanikiwa kubomoa banda lililokuwa likitumiwa na Idara ya Usafiri na Leseni na Shirika la Meli. Shirika linakusudia kulitumia eneo hilo kwa maegesho ya magari. Hivi sasa eneo hilo inaendelea kutengenezwa na kazi ya uwekaji wa lami imekamilika. Kazi za ujenzi wa jengo la abiria zitafanywa mara tu hali ya kifedha ya Shirika itakaporuhusu.

Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kuiimarisha miundo mbinu ya Bandari ya Mkoani kwa kurekebisha eneo lililodidimia katikati ya gati hiyo. Shirika limekamilisha maandalizi ya kazi hiyo na matengenezo ya eneo hilo yanategemewa kuanza mwezi wa julai, 2010.

Mradi wa Uimarishaji wa Gati ya Mkokotoni

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kujenga gati katika Bandari ya Mkokotoni pamoja na Tumbatu. Shirika limeshindwa kuutekeleza Mradi huu kutokana na uhaba wa fedha. Hata hivyo Shirika linajiandaa kuanza ujenzi wa gati hiyo katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011.

Uimarishaji wa Zana Nzito

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kuvifanyia matengenezo makubwa vifaa vya kufanyia kazi Bandarini pamoja na kununua vifaa vipya vya kisasa. Shirika limeendelea kulipa deni la mkopo lililochukua kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar kwa ajili ya vifaa vipya katika mwaka uliopita, ambapo Shirika tayari limelipa T.Shs. 1,414,754,134.19 kati ya T.Shs. 2,269, 627,800 zilizokopwa. Aidha vifaa vikuukuu navyo vinaendelea kufanyiwa matengenezo.

Matengenezo ya Meli ya *L.C.T Jitihada*

Mhe. Spika, lengo la Mradi huu ni kuifanyia matengenezo makubwa Meli ya L.C.T Jitihada ambayo tayari imekabidhiwa Shirika la Bandari kutoka Serikalini na Shirika limekamilisha matengenezo ya umbo (*Hull*) la Meli hiyo. Aidha kazi za ufungaji wa mashine mbili mpya pamoja na mitambo yake mengine zitafanyika kabla ya kumalizika mwaka 2010 kwani mashine hizo tayari zimeshanunuliwa.

Matengenezo ya Sakafu ya Bandari ya Malindi

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kuyafanyia matengenezo maeneo yaliyovunjwa mabanda ya kuwekea mizigo na maeneo mengine yaliyoathirika ya Bandari ya Malindi kwa kuyashindilia na kujenga sakafu mpya ili yatumike kuwekea makontena. Eneo la zamani la kuhifadhia makontena bandarini limeshafanyiwa matengenezo tayari linatumika. Shirika linaendelea na matengenezo ya sakafu zilizobakia awamu kwa awamu.

Ujenzi wa Sehemu ya Kuegesha Vyombo vya Mizigo aina ya *"Landing Craft"*

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kujenga ″Ramp″ kwa ajili ya kuegesha vyombo vya aina ya *"Landing Craft"* ambavyo vilikuwa vinahudumiwa eneo la Forodha Mchanga. Kazi zilizofanywa ni pamoja na kuvunja sehemu ya banda lililokuwa na karakana ya maboya pamoja na kujenga ″*ramp*″ yenyewe. Mradi huu unategemewa kukamilika kabla ya Disemba 2010.

Mapato na Matumizi

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi, 2010 Shirika lilikukusanya Jumla ya shilingi 5,543,498,051 kati ya hizo, shilingi 5,383,876,576 zilizokadiriwa kutokana na mauzo ya huduma zake mbali mbali, ikiwa ni sawa na asilimia 103 ya makadirio. Aidha, jumla ya shilingi 3,492,206,721 zilitumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilima 85 ya makadirio ya matumizi ya shilingi 4,128,715,249. Katika kipindi hicho jumla ya shilingi 1,686,492,374.60 zilitumika kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Malengo kwa mwaka 2010 / 2011

Mhe. Spika, Shirika la Bandari linatarajia kutekeleza malengo mbali mbali katika utoaji wake wa huduma. Malengo hayo ni kupokea meli 192 za kigeni zenye uzito wa ujazo (*GRT*) wa tani 1,500,000.00 pamoja na safari za meli za ndani zipatazo 3,500 na majahazi 1,600; kutoa huduma za minara na maboya,

huduma za rubani kwa vyombo vinavyoingia na kutoka bandarini, uuzaji wa vibali mbali mbali vya kuingilia bandarini na huduma nyenginezo za mizigo. Kadhalika Shirika linategemea kuteremsha na kupakia jumla ya tani 121,850 za mzigo mchanganyiko pamoja na makontena 20,360.

Mhe. Spika, shirika limekadiria kukusanya jumla ya shilingi 7,751,025,396.00. Aidha, katika kutekeleza malengo hayo Shirika limepanga kutumia jumla ya shilingi 5,936,955,705 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo Shirika linatarajia kuendelea na uimarishaji wa huduma na rasilimali zake kwa kuikamilisha miradi iliyoanzishwa mwaka wa fedha unaomalizika. Aidha, Shirika linatarajia kununua taa za solar, kuimarisha njia za mawasiliano kwa kuweka *Radio Base* (2) *GMDSS* (*Global Maritime Distress Safety System*) na matengenezo ya Mnara wa Mwana wa Mwana. Kadhalika Shirika linategemea kumaliza matengenezo ya Meli ya M.V. Jitihada, ununuzi wa tishali dogo la kuhudumia vyombo vya kasi vya abiria, pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa (zana nzito) vya kuhudumia mizigo bandarini.

Shirika la Meli

Mhe. Spika, Shirika la Meli lina jukumu la kuendesha meli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kutoa huduma za Uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar. Kwa sasa Shirika linaendesha meli mbili za MT Ukombozi na MV Maendeleo baada ya serikali kuiuza Meli ya MV Mapinduzi kwa kampuni ya *BADR EAST AFRICAN ENTRPRISE LTD* ya Dar es salaam .

Mhe. Spika, Shirika la Meli limezifanyia matengenezo makubwa meli zake ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi kama ipasavyo. Meli ya MV. Maendeleo imesharudi kutoka Mombasa mnamo mwishoni mwa mwezi wa Mei mwaka huu. Meli hiyo ilipelekwa kwa matengenezo mnamo mwezi Julai mwaka 2009 baada ya kupata maharibiko wakati ikitokea Pemba. Matengenezo ya meli hii yalichelewa sana kutokana na kutopatikana kwa vipuri vya kuifanyia matengenezo kutoka nje na kufungwa kwa Chelezo cha African Marine kwa muda mrefu hadi Februari 2010 kilipofunguliwa na kuanza kufanya kazi tena. Hivi sasa meli hiyo tayari imeanza safari zake.

Mhe. Spika, Meli ya MT. Ukombozi nayo ilikuwa chelezoni Mombasa Kenya kwa ajili ya matengenezo ya mitambo ya umeme (*generator*). Meli hii baada ya kupata maharibiko ya mashine mnamo mwezi wa Disemba 2009 ilisita kuendelea na kazi zake hadi kukamilika matengenezo tarehe 25 Mei, 2010.

Mhe. Spika, Kitengo cha Uwakala kimeendelea kutoa huduma za uwakala kwa meli mbali mbali zinazoingia katika bandari za Zanzibar na kuingiza Jumla ya shilingi 456,376,470. Kitengo hichi kimepata ufanisi mkubwa baada ya wafanyakazi wake kupatiwa mafunzo kwenye vyuo mbali mbali nje na ndani ya nchi. Kitengo hiki kimechangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Shirika hasa katika kipindi hiki kigumu tulichonacho kwa kulinganisha na gharama za uendeshaji wa Kitengo hiki na mapato yake.

Mhe. Spika, shirika limekuwa na matatizo mengi ambayo yanachangia kukwamisha jitihada za Shirika kujikwamua ki-uchumi. Matatizo hayo yanajumuisha uchakavu wa meli ambao unachangiwa na umri mkubwa na hivyo kupelekea kuharibika kwa meli zetu mara kwa mara na kuongezeka kwa gharama za matengenezo na uagiziaji vipuri.

Mhe. Spika, kutokana na matatizo hayo ni dhahiri hali ya uchumi ya shirika si nzuri. Hivyo shirika litafanya maamuzi ya kubadili meli tulizonazo ambazo zimepitwa na wakati kwa kuziuza na kununua meli nyengine zitazoweza kuhimili ushindani ndani ya soko. Shirika pia limepanga kutayarisha Sheria itakayotoa mamlaka kwa Shirika kumiliki vyombo (meli) ili umiliki huu uweze kutumika kukuza biashara za shirika kwa kutumia fursa za mikopo ya benki na shughuli nyengine.

Mapato na Matumizi ya Shirika

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 Shirika lilikukusanya Jumla ya shilingi 1,651,840,466 kati ya shilingi 2,709,009,500 zilizokadiriwa, ikiwa ni sawa na asilimia 73 ya makadirio. Aidha, jumla ya shilingi 1, 820,294,973 zilitumika sawa na asilima 85 ya makadirio ya matumizi ya shilingi 2,569,300,802.

Malengo ya Shirika kwa mwaka 2010/2011

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Shirika linategemea kuendeleza harakati zake za kuanzisha shughuli za uwakala wa meli za kigeni katika bandari ya Dar es Salaam. Shirika linategemea kukusanya jumla ya shilingi 2,790,015,900 kutokana na vianzio vyake vya mapato na linategemea kutumia jumla ya shilingi 2,511,954,812.

MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA USAFIRI BAHARINI

Mhe. Spika, kampuni za watu binafsi zinaendelea kutoa mchango mkubwa katika nyanja ya usafirishaji kwa njia ya bahari kwa kutumia vyombo vyao

mbali mbali vilivyosajiliwa hapa nchini. Kampuni zinazotoa huduma ni *Azam Marine, Sea Star Services, Africa Shipping, Fast Ferries Limited, Mkunazini Shipping Enterprises, Panda Shipping Enterprises, Mega Speed Liners, Al Ghubra Shipping Limited, Seagull Transport* na *Visiwani Shipping.*

Mhe. Spika, kampuni hizi zinatoa ushirikiano mzuri kwa Wizara yangu katika masuala mbali mbali yanayotokea katika sekta ya usafiri wa baharini. Kwa kuzingatia umuhimu wa kampuni binafsi katika sekta hii, Wizara yangu itaendelea na juhudi zake za kushirikiana na kampuni hizo ili kuboresha huduma za usafiri wa baharini kwa kusimamia vyema taratibu za usalama, kuwapa ushauri wa kuendesha kampuni zao kitaalamu, na kuwataka wabadilike kulingana na mabadiliko yanayotokea ulimwenguni katika teknolojia ya usafiri baharini.

SEKTA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Sekta ya Mawasiliano inatoa mchango mkubwa katika kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii, sekta hii hapa nchini inajumuisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa njia za posta, simu na *internet*. Huduma hizi zinasimamiwa na taasisi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliyo chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya SMT.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*Tanzania Communications Regulatory Authority* (*TCRA*) ni mamlaka iliyopewa jukumu la kusimamia shughuli za udhibiti wa huduma na watoa huduma za mawasiliano.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2009/2010 Mamlaka imeendelea na shuguli za kusimamia na kudhibiti watoa huduma na watumiaji masafa wasio na leseni, kupunguza muda wa utoaji leseni mbalimbali za mawasiliano, kutoa elimu kwa jamii juu ya wajibu na haki za watumiaji wa huduma za mawasiliano, kushughulikia kwa karibu malalamiko ya wateja juu ya watoa huduma, kutatua matatizo ya muingiliano wa mitandao itumiayo masafa, kutoa '*call sign'* na *MMSI* (*maritime mobile service identity*) kwa meli zinazosajiliwa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009, hadi Machi 2010, Mamlaka imetoa jumla ya shilingi milioni 17 katika kuchangia huduma mbalimbali za kijamii, ikiwemo vifaa vya ujenzi na komputa vyenye thamani ya shilingi. Milioni sita (6,000,000/=) kwa ajili ya skuli ya Kidoti, Ujenzi wa kituo cha Afya Bwagamoyo Mtambwe shilingi 2,000,000/=, Msaada wa shilingi 7,500,000/= kwa ajili ya kununulia komputa pamoja na *printers* kwa ajili ya Skuli ya

Sekondari ya Chwaka, mchango wa shilingi 1,500,000/= kwa vikundi vya ushirika wa kinamama *Saccos Sharifumsa*.

Shirika la Posta Tanzanaia

Mhe. Spika, Shirika la Posta la Tanzania linaendesha shughuli za huduma za posta Unguja na Pemba kama sehemu ya mtandao wa posta hapa nchini. Kazi zake ni kupokea, kusambaza na kusafirisha barua na vifurushi ndani na nje ya nchi, kutuma fedha kwa hati za fedha, hundi na hawala za posta, kuchapisha na kuuza stempu na kutoa huduma za kibiashara na uwakala. Huduma zilizotolewa katika kipindi cha 2009/2010 zinaonekana katika **Kiambatatisho Nam 11.**

Mawasiliano ya Simu na *Internet*

Mhe. Spika, kwa kiasi kikubwa huduma za mawasiliano ya simu na Internet zinatolewa na sekta binafsi, kwa sasa huduma za simu hapa Zanzibar zinatolewa na kampuni tano za *Zantel, Tigo , TTCL, Zein* na *Vodacom*. Kampuni hizo zinakisiwa kuwa na jumla ya wateja 850,000 kwa hapa Zanzibar na hivyo kupelekea kufikia "*Tele Density"* inayozidi asilimia 40 kulingana na makisio yaliyofanywa hasa ukilinganisha maeneo yenye huduma za simu Unguja na Pemba ni takribani asilimia 95. Aidha mawasiliano ya Internet kwa hapa Zanzibar yanatolewa na kampuni nne za *Zantel, Zanlink, TTCL* na *Zanzibar Data Com.* Kampuni hizo zimeshasajili wateja zaidi ya 100,000 ambao wanapata huduma za haraka na kwa urahisi.

Kampuni ya *Zantel*

Mhe. Spika, Kampuni ya *Zantel* ni kampuni pekee ya simu ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamiliki sehemu ya hisa. Kampuni hiyo imekuwa ikitoa huduma za simu za mkononi na Internet kwa wakaazi wa Zanzibar na Tanzania Bara. Tokea kuanzishwa kwake hapa Zanzibar, *Zantel* imepata mafanikio makubwa yakiwemo kuongezeka kwa eneo la mtandao wake (*network coverage*) kwa aslimia 80 na asilimia 25 kwa Tanzania Bara. Aidha, huduma za kasi ya *data* na *internet* zinawafikia asilimia 18 ya watu wa Zanzibar kwa kupitia teknolojia ya *CDMA/3G network* na vituo vya huduma kufikia 645 kwa Tanzania yote.

Mhe. Spika, mtandao wa teknolojia ya *CDMA* unaotoa huduma za kasi za *internet* umekamilika ukiwa na vituo 74 kwa nchi nzima. Aidha, kampuni imejiunga kwa mfumo wa kutumia mkonga wa baharini (*submarine fibre optic system*) ili kutoa huduma za kasi nje na ndani ya Tanzania. Mtandao huo unajulikana kwa jina la *EASSY (East African Submarine System)* na *Zantel* ni

mmiliki mwenza. Mkonga huu uliwasili nchini mwezi Aprili mwaka 2010 na unategemewa kuanza kazi mwezi Julai 2010.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Kampuni ya Zantel imechangia Serikalini jumla ya shilingi 16.810 Billioni ikiwa ni kodi mbali mbali kwa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, kampuni ya simu ya Zantel imechangia jumla ya shilingi Milioni 91.1 katika shughuli mbali mbali za kijamii hapa Zanzibar. Shughuli hizo ni utayarishaji wa mabango ya maelezo katika vianzio vya maji shilingi Milioni 18.2, uandaaji wa maadhimisho ya Sauti ya Busara Sshilingi Milioni 58.8, matengenezo ya Wodi ya Akinamama katika hospitali ya wagonjwa wa akili shilingi Milioni 6.4 na matayarisho ya mkutano wa Baraza la Biashara Zanzibar shilingi Milioni 7.7.

Mhe. Spika, Kampuni ya Zantel inakusudia kutekeleza mipango mbali mbali ili kuboresha huduma zake kwa wateja. Miongoni mwa mipango hiyo ni kuanzisha huduma za teknolojia ya *3G* ili kuwapatia wakazi wa Zanzibar huduma bora na za kasi za data na internet na kutekeleza mradi mpya wa upanuzi wa hudumma ya *Internet* ambao utaongeza vituo 600 katika mtandao pamoja na kubadilisha teknolojia ya simu za mkononi ya "broadband" na kuongeza vituo 156. Kampuni inakusudia kuingia katika mpango wa kujenga mwamko wa mazingira.

Kampuni ya *TTCL*

Mhe. Spika, Kampuni ya simu Tanzania (*TTCL*) ina jukumu la kutoa huduma bora za mawasiliano kwa njia ya simu katika mazingira ya ushindani wa kibiashara na kujenga Mtandao wa simu nchi nzima, ili kuwawezesha Watanzania popote walipo nchini kuwasiliana vizuri kwa njia ya simu ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha 2009/2010 *TTCL* ilikusudia kujenga na kukamilisha "*Base Station*" 5 kwa Unguja na Pemba lakini ujenzi huo haukuweza kutekelezwa kutokana na ukosefu wa pesa ya kugharamia ujenzi huo mkubwa.

Mhe. Spika, kampuni iliweza kuunganisha laini mpya za mezani 574 ikiwa ni asilimia 96 ya lengo.(Unguja laini 524 sawa na asilimia 96 na Pemba laini 52 ikiwa ni asilimia 100 ya lengo). Gharama nafuu ya uunganishaji laini za simu za mezani pamoja na matumizi yake ndio siri ya mafanikio.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Kampuni imelipa kodi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zenye jumla ya shilingi 413,279,803.58. Aidha, kampuni hiyo ilitoa michango mbali mbali katika taasisi za jamii na vikundi vya maendeleo yenye thamani ya shilingi 13,965,000.

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha 2010/2011 Kampuni inatarajia kukamilisha mradi wa simu za Mikononi kwa kutumia teknolojia ya *CDMA* kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba lengo ni kuwa na usikivu mzuri wa sauti na mawasiliano bora ya *Internet*. Kampuni itaendeleza Ujenzi wa *Base Terminal Station* (*BTS*) 5 (Pwani Mchangani, Bwejuu, Fuoni, Tunguu na Konde). Kupanua uwezo wa *ADSL Broadband* kutoka viunganishi 580 hadi kufikia viunganishi 1,000. Kufunga simu mpya za mezani 600, huduma ya *internet* (*ADSL BB*) 230 na simu za *Mobile* 1,000.

HITIMISHO

Makadirio ya Bajeti ya Wizara

Mhe. Spika, ili wizara yangu iweze kufanikisha kazi zake kwa ufanisi naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 13,167,000,000 kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kati ya fedha hizo shilingi 4,067,000,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 9,100,000,000 kwa kazi za maendeleo. Vile vile naliomba Baraza lako tukufu liruhusu wizara yangu kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 1,653,500,000 yanayotokana na vianzio mbali mbali vilivyomo katika wizara yangu.

Shukrani

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokuwa nikitoa maelezo ya wizara yangu. Ni matumaini yangu kwamba, Baraza lako tukufu litatoa mchango ambao utaisaidia wizara yangu kutatua matatizo ambayo ilikumbana nayo katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kwanza kuwashukuru waheshimiwa wajumbe wote kwa ushirikiano wao kwa Wizara yangu na pia kuwatakia ushindi mkubwa wale wajumbe watakaogombea ili warudi kulitumkia Taifa kwa kipindi chengine cha miaka mitano. Aidha kwa kuwa nami nitashiriki katika mchakato huo wa uchaguzi naomba pia mniombee nishinde ili tuje tushirikiane katika kazi za ujenzi wa Taifa hili ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mafanikio ya wizara yangu ambayo nimeyaeleza katika hotuba yangu hii ni matokeo ya ushirikianno mkubwa wa wadau mbali mbali wa ndani na nje, na hivyo sina budi kuwashukuru. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi marafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo kwa muda wote

huo wamekuwa wakiisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Nchi hizo ni Uholanzi, Ireland, Jamhuri ya Watu wa China, Libya, Japan, Saudi Arabia, India, Misri, Marekani, Ujerumani, pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya Benki ya Dunia (World Bank), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Umoja wa Maendeleo ya Kimataifa wa Nchi zinazosafirisha mafuta kwa wingi ulimwenguni (*OPEC FUND), SAUDI FUND, NORAD*, Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP*, *IMO*, *ICAO*. Pamoja na nchi na mashirika mengine ambayo kwa njia moja au nyengine yanatuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo ya sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji kwa misaada yao ya fedha, utaalamu na vifaa.

Mhe. Spika, napenda nimalizie kwa kumshukuru Mhe. Brigedia Jenerali Mstaafu Adam C. Mwakanjuki Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha shughuli za wizara katika kipindi chake ambacho amekuwa akitumikia Wizara hii kama Waziri. Ushauri, mwongozo na ujasiri wake umesaidia sana kutekeleza shughuli za sekta ya Mawasiliano na Usafiri. Aidha, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali zinazowakabili, zikiwemo uchache wa nyenzo za kutendea kazi, maslahi yasiyokidhi haja, na mengineyo. Kadhalika napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya. Nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao.

Mhe. Spika, shukurani za pekee zimwendee Mpiga Chapa Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Upigaji Chapa kwa kufanikisha uchapaji wa vitabu mbali mbali pamoja na uchapaji wa hotuba hii, na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Mwisho naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa taasisi za Serikali na watu binafsi pamoja na wananchi kwa jumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu. Aidha napenda kuwashukuru Wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kufanya kazi kwa uaminifu, nidhamu na moyo wa kuipenda Nchi yao.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukuwe nafasi hii uliyonipa nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Subhana Wataalla, mwenye wingi wa Rehma, Muumba Mbingu na Ardhi na kila kitu kilichomo ndani yake na akakitengeneza, na akakikadiria kila kimoja jambo lake na akakiongoza kufanya jambo hilo.

Mwenyezi Mungu Mtukufu nakuomba *Inshaallah* katika mchakato huu wa kutafuta mgombea Urais wa Zanzibar, rais ambae atakuwa na jukumu la kuongoza nchi yetu na kuwatumikia watu wake wote kwa ustawi wa Zanzibar na kwa manufaa ya Wazanzibari, lakini kwa kuwa jambo hili ni kubwa, linalotaka uadilifu mkubwa na siri sana, tunakuomba sisi waja wako umuweke madarakani rais ambaye ana nia nzuri na watu ataowaongoza na ana malengo mazuri kwa nchi yetu. Mwenyenzi Mungu wewe ndiye unaejua yaliyo dhahiri na yaliyofichikana na wewe ndiye unaejua nani au yupi atayefaa kuwa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakushukuru na wewe mwenyewe binafsi kwa kuniweka mchangiaji wa mwanzo katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka huu wa fedha wa 2010/2011. Aidha, napenda nitumie fursa hii uliyonipa kuwashukuru wajumbe wangu wote wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mashirikiano makubwa waliyonipa wakati wote wa utendaji wa kazi zetu. Mashirikiano yao yamewezesha na kufanikisha kamati yetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa sana. Nakupongezeni nyote Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, namalizia shukrani zangu kwa kuupongeza uongozi mzima wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi chini ya usimamizi wa Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni Waziri wa Wizara hii, Mhe. Mzee Ali Ussi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani Naibu Waziri wa Wizara hii, Katiu Mkuu Ndugu Dr. Vuai Lilla, Mkurugenzi Mipango na Sera Ndugu Msanif Haji na Wakurugenzi wote waliobakia, Mameneja Shirika la Meli na Bandari pamoja na Watendaji wote wa Wizara na wafanyakazi wote kwa jumla. Tunakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa tuliyoyapata kwenu hasa tulipokuwa tukifanya ziara za mara kwa mara za kikazi katika taasisi zenu.

Shukrani za pekee si za upendeleo bali ni kwa umuhimu, naomba azipokee Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (*UUB*) Ndugu Ali Tahir Fattawi kwa msaada wake mkuwa kwa kamati yangu na mimi binafsi, lakini pia takriban kwa Waheshimiwa wote wenye Majimbo hususan Mkoa wa Mjini Magharibi, na hasa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. Msaada wake wa gari za vifuzi, *grader* na matengenezo ya dharura ya kuziba mashimo kwenye barabara na kadhalika umewaweka pahala pazuri

Waheshimiwa na sasa kuwa na matumaini mazuri ya kushinda uchaguzi kwani hizo zilikuwa sehemu ya baadhi ya kero za wananchi.

Mhe. Spika, kwa kuwa kamati yangu inamaliza muda wake wa uhai wa kamati katika kipindi cha muda mfupi ujao, natoa shukrani kwa niaba ya wajumbe wanzagu, kwako wewe Mhe. Spika, kwanza kwa kutuchaguwa sisi tukaunda Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na tukaifanyia kazi kwa muda wote wa uhai wa kamati tena kwa mafanikio makubwa sana.

Pili, kwa kutuelekeza na kutuongoza katika shughuli zetu za kikazi na kutushauri vizuri pale tunapopata jambo zito ambalo huhitajia mwongozo wako.

Mhe. Spika, nawashukuru Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu na Wajumbe wako wote wa Baraza lako hili la Saba la mwaka 2010 kwa mashirikiano mazuri waliyoonesha ndani ya Baraza tangu wakiwa kwenye Kazi za Kamati mpaka wakiwa kwenye Baraza zima. Hali hiyo ya mashirikiano imejenga imani na kuleta matumaini mema ya huko tunakoelekea kwenda.

MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imeundwa kwa mujibu wa kanuni ya 109 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi na kwa mujibu wa Kanuni ya 104(c) kamati imeundwa kutokana na wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamad Masoud Hamad - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Kamal Basha Pandu - Mjumbe
4. Mhe. Ame Ussi Juma - Mjumbe
5. Mhe. Subeti Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Zakiya Omar Juma - Mjumbe
7. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Omar Ali Jadi - Mjumbe
9. Mhe. Ali Denge Makame - Mjumbe
10. Mhe. Asha Moh'd Hilal - Mjumbe
11. Ndg. Othman Ali Othman - Katibu Kamati
12. Ndg. Rabia Juma Shaaba - Katibu Kamati

Mhe. Spika, sasa naomba uniruhusu niende katika kuichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ilitarajiwa kutumia shilingi 3,744,000,000.00 kwa kazi za kawaida na kupanga

kukusanyanya jumla ya shilingi 1,500,000,000, hadi kufikia mwezi Machi, 2009 fedha zilizoingizwa hadi Machi, 2010 kwa kazi za kawaida zilikuwa ni shilingi 2,543,847,930 sawa na asilimia 68 ya makadirio.

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA 2009/2010 NA MALENGOKWA MWAKA WA 2010/2011

Afisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, Afisi kuu Pemba katika mwaka 2009/2010 ilikuwa na majukumu ya kuratibu na kuunganisha idara na mashirika yote ya wizara hii, kusimamia kazi za utawala na utumishi, kupokea makampuni mbali mbali ambayo yako tayari kwa ujenzi wa barabara/Anga katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kupokea vikao vya mkutano wa mashirikiano kati ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Pemba, kusimamia na kuratibu majengo yote ya wizara, kukusanya na kusimamia mapato yote ya wizara Pemba na ziara za viongozi wa wizara zinazofanyika Pemba.

Mhe. Spika, malengo ya Afisi kuu Pemba kwa mwaka 2010/2011 kupitia Idara ya Mipango na Sera ni kuwa na mwanasheria wake, kujenga nyumba za wageni zilizoko Gombani, kufundisha wafanyakazi na kuwaendeleza katika fani mbali mbali.

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inapongeza jitahada zinazofanywa na afsi hii katika kuendeleza kazi na miradi mbali mbali iliyoko Pemba, kama miradi ya barabara ya Wete - Konde na Wete - Gando inayojengwa na kampuni ya *MECCO* ambapo tayari nyumba zilizoathirika na ujenzi huo zimeshalipwa fidia na kiasi cha kilomita 14 za barabara ya Wete-Konde zimeshasafishwa na kilomita kadhaa zimeshajengwa kwa kifusi. Aidha, barabara ya Wete - Gando kazi za upimaji zimekamilika na kazi za usafishaji tayari zimeanza.

Mhe. Spika, kamati inashauri Kitengo cha Mipango na Sera Pemba kipewe nyenzo ili kazi za kitengo hiki ziweze kuendelea zaidi, kutokana na umuhimu wake na kuongezwa wafanyakazi ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, matatizo yanayokabili utendaji kazi Pemba ambayo yanataka kufanyiwa kazi ni pamoja na uchakuvu wa mitambo katika karakana, tatizo la kutokupelekwa gari za serikali katika karakana, kuharibika kwa zana zinazotumika katika kazi za barabara, ukosefu wa taa za Uwanja wa Ndege Pemba, uchakavu wa *tractor* uwanja wa ndege, upungufu wa wafanyakazi na kutofika fedha za utendaji wa kazi kwa wakati ni mambo ambayo kamati inashauri kutafutiwa ufumbuzi.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera katika mwaka 2009/2010 ilijipangia malengo ya kukamilisha Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri wa Zanzibar, kuanzisha kitengo cha kusimamia mpango huo, kukamilisha kazi za utayarishaji wa mpango mkuu wa kiwanja cha ndege pamoja na uchambuzi yakinifu wa ujenzi wa jengo jipya la abiria katika kiwanja cha ndege cha Zanzibar na kukamilisha taratibu za kugeuza Afisi ya Mrajis wa Meli kuwa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kama sheria inavyoelekeza.

Mhe. Spika, kamati inazipongeza jitahada za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Idara ya Mipango na Sera kwa shughuli mbali mbali zilizotajwa katika maelezo ya idara hii. Suala la ujenzi wa jengo jipya la abiria utasaidia sana katika kuendeleza mbele maendeleo ya nchi yetu kwa kuinua uchumi ikiwa pamoja kuongezeka kwa utalii. Kwani uwanja wa ndege ni kioo cha nchi.

Mhe. Spika, suala la kuimarishwa kwa kitengo cha urajis kuwa mamlaka kamili ni la kupongezwa sana kutokana na umuhimu wa kitengo hiki. Kamati inaziunga mkono jitihada hizi kutokana na nchi yetu kuzungukwa na bahari na kuongeza nguvu mamlaka hii kwa kuipa uwezo kufanya mambo yote yaliyotajwa katika sheria iliyoanzisha mamlaka hii, ili kuondosha matatizo yaliyokuwepo kabla ya kupitishwa sheria hii.

IDARA YA USAFIRI NA LESENI

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2009/2010 idara imetekeleza jukumu lake la ukaguzi wa magari ambapo jumla ya vyombo 25,632 vimekaguliwa vikiwemo 120 kwa ukaguzi maalum, jumla ya madereva 3,015 walipasishwa kati ya waombaji 4,506.

Mhe. Spika, Idara ya Usafiri na Leseni ilitoa ruhusa za njia kwa magari Unguja na Pemba zilikuwa 1,755, magari ya shamba yalikuwa 398, daladala 432, *private hire* 336, *taxi* 183, magari ya wanafunzi 211, magari ya wafanyakazi 21, magari ya mizigo 364 na idadi ya bendera za SMZ zilizouzwa ni 135.

Mhe. Spika, kazi zinazofanywa na idara hii ni kubwa na zinahitaji fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji kazi. Kamati inashauri kuongezewa fedha ilizoziomba katika bajeti hii ili iweze kufanya kazi zake kama ilivyojipangia.

Mhe. Spika, kamati imepokea malalamiko ya wamiliki wa magari ya abiria yenye magurudumu/maringi mawili ambayo yamepigwa marufuku kutembea

barabarani pamoja na sababu ambazo serikali inazitambua za kukataza gari hizo aina ya daladala zisitembee.

Mhe. Spika, kamati inashauri kuwa gari hizo ziruhusiwe lakini kwa masharti maalum na kwa muda maalum hasa kwa kuwa tangu kuondoshwa kwa gari hizo usafiri umekuwa wa tabu sana.

IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI BARABARA

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2009/2010 idara ilifanya kazi za kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kamati inazipongeza jitihada zinazochukuliwa na Wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kwa kuweza kuzishughulikia barabara za mjini zile zenye matatizo makubwa kwa kushirikiana na Kampuni ya *SOGEA* na mafanikio yameanza kuonekana na wananchi wamelifurahia sana kwani mawasiliano ni maendeleo.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Wizara kupitia Idara ya UUB bado kamati inakumbushia na kutaka kujua lini ahadi za Mhe. Rais za matengenezo na ujenzi wa barabara za Kwamtipura-Amani zitajengwa ahadi ambazo ameitoa kati ya 2007/2008 na barabara ya Boshoa-Utambi-Tazari ahadi ya Rais aliyoitoa tarehe 8 Disemba, 2005.

IDARA YA ANGA

Mhe. Spika, Idara ya Anga katika mwaka 2009/2010 ilihudumia ndege 33,392 na abiria 454,133 walihudumiwa katika viwanja vya ndege vya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 idara inakusudia kuimarisha huduma mbali mbali za ndege, abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kamati inaridhishwa na jitihadi zilizochukuliwa na Wizara kupitia Idara ya Anga kwa hatua ilizozichukua katika matengenezo ya njia ya kurukia na kutulia ndege. Hii itapelekea kuongezeka kwa huduma za ndege pindi kazi hii ikimalizika na kuongeza uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, kamati inasisitiza suala la idara hii kufanywa mamlaka ili kuweza kuipa uwezo kuweza kujiendeleza zaidi na kutoa huduma bora zaidi, hasa ukizingatia malengo ya idara hii ni makubwa na ipo haja ya kupewa uwezo kuweza kuwa katika mazingira mazuri ya utendaji wa kazi.

MASHIRIKA YALIYO CHINI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI ZANZIBAR

SHIRIKA LA BANDARI

A. SHIRIKA LA BANDARI

Mhe. Spika, Shirika la Bandari kwa kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 limeweza kuhudumia meli za kigeni 124, meli za ndani zilizofanya safari 2,892, majahazi na maboti yalifanya safari 2,231, jumla ya abiria 1,360,279 walisafiri kwa vyombo ndani, abiria waliowasili kwa meli za kitalii 3,633 na matengenezo ya maboya, minara na vyombo mbali mbali vinavyohitaji huduma ya chelezo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 shirika litaendelea kutekeleza miradi ya Ujenzi wa Jengo la Abiria katika Bandari ya Malindi, uimarishaji wa Bandari ya Mkoani, mradi wa Uimarishaji wa Gati ya Mkokotoni, uimarishaji wa zana nzito, matengenezo ya meli ya *L.T.C* Jitihada, matengenezo ya sakafu Bandari ya Malindi na uenzi wa sehemu ya kuegesha vyombo vya mizigo aina ya *landing craft.*

Mhe. Spika, kamati inapongeza Shirika la Bandari kutokana na kazi nzuri inazozifanya hususan matengenezo ya minara iliyoko sehemu mbali mbali katika nchi yetu na kutuletea maendeleo katika kuendeleza mbele shirika, matengenezo ya meli ya *L.C.T* Jitihada na baada ya kumalizika itasaidia sana shirika katika kazi zake.

Mhe. Spika, kamati ilielezwa kwamba kuna matatizo katika mnara wa Nungwi, kutokana na urefu wake na kuna Hoteli ya Zalu ambayo imejenga jeti refu sana ambayo inasababisha meli kutokuuona vyema mnara inapokuwa katika eneo hilo. Katika hali hiyo, kamati inashauri jeti hiyo iondoshwe au ifupishwe kwa usalama wa meli zinazopita katika katika eneo hilo yasije yakatokea maafa, vyenginevyo serikali mkae tayari kujibu na kulipa fidia kwa lolote litakalotokea endapo meli yoyote ile itakapopata ajali ya kugonga jeti hiyo.

Mhe. Spika, kamati yangu jana tarehe 04/07/2010 imepokea barua mbili moja kutoka kwa Kampuni ya *AL-GHUBRA MARINE SERVICES LTD.* REF: AMS/BQ/08/01/09 ya tarehe 25 April, 2010 inayohusu OMBI LA RUHUSA YA KUINGIZA *CRANE* BANDARINI lakini kwa bahati mbaya barua hiyo haikujibiwa. Tarehe 15/5/2010 Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi alimuandikia Mkurugenzi Mkuu Shirika la Bandari Zanzibar kuhusu kuruhusiwa kuingiza *crane* kwa ajili ya meli za *AL-GHUBRA MARINE*

SERVICES LTD., lakini bado barua hiyo haijapata jibu na agizo halijatekelezwa.

Mhe. Spika, kamati yangu inataka kupata jibu kutoka serikalini kwa nini na kwa sababu gani Kampuni ya *AL-GHUBRA MARINE SERVICES LTD.* imezuiliwa na haijaruhusiwa kuleta *crane* hiyo, ambayo licha ya kuwa itamilikiwa na kampuni, bali pia itasaidia sana upakizi na upakuzi wa mizigo mizito bandarini jambo ambalo kwa sasa kwa sababu ya uhaba na ubovu wa *crane* iliyokuwepo unakwamisha shughuli hizo bandarini, lakini pia serikali itapata mapato kutokana na huduma zinazohusu bandarini hapo.

B. SHIRIKA LA MELI

Katika mwaka 2009/2010 Shirika la Meli limeweza kuhudumia meli za kigeni kitengo cha uwakala jumla ya meli 94 na kuingiza jumla ya shilingi 456,376,470. Shirika lilikusanya jumla ya shilingi 1,651,840,466 kati ya shilingi 2,709,009,500.

Mhe. Spika, Shirika la Meli na Wakala linategemea kuendeleza shughuli za Uwakala wa Meli Bandari ya Dar-es-Salaam na linategemea kukusanya jumla ya shilingi 2,790,015,900 katika vianzio vyake vya mapato.

Mhe. Spika, kamati inatoa pongezi kwa wizara kwa kuwezesha kupatikana mteja kuweza kuinunua meli ya MV Mapinduzi kutokana na hali iliyonayo na ushauri wa kitaalamu iliyokuwa inapewa kamati kuhusu meli hiyo na hivi sasa kamati imeridhika na suala hilo.

SEKTA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Sekta ya Mawasiliano ina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya nchi kutokana na mchango wake mkubwa kwa maendeleo. Kamati katika kutembelea taasisi hizi inazipongeza kwa juhudi zake za kubuni mbinu mpya za kuleta maendeleo katika nchi yetu na kuyafanya mawasiliano yawe bora zaidi na jukumu hilo limepewa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

SHIRIKA LA POSTA

Mhe. Spika, kamati ilipotembelea Shirika la Posta imepongeza mpango wa kuanzisha mfumo wa anuani mpya za kitaifa kwa kutumia *symbol* za posta ambazo ni kitambulisho kwenye anuani na kinapotumika humtambulisha mwananchi kwa usahihi zaidi. *Symbol* za posta zinarahisisha eneo au pahala anapoishi mwananchi ifahamike kwa usahihi mkubwa bila kuchanganyikiwa na

kwa kazi za posta inarahisisha sana uchambuaji na ufikishaji wa vitu vya posta kwa waliotumiwa kwa ufanisi.

KAMPUNI YA *TTCL*

Mhe. Spika, Kampuni ya Simu ya *TTCL* ina jukumu la kutoa huduma ya mawasiliano kwa njia ya simu na iko mbioni katika kukabiliana na ushindani wa kibiashara baada ya kuondoka wawekezaji wageni waliokuwa wanalitia hasara Shirika na kuwaweka wazawa katika madaraka ya uongozi wa juu. Kamati inazipongeza jitihada hizi za shirika kwa kuweza kujiendeleza na kurudisha hadhi yake iliyokuwanayo ya kutoa huduma bora za mawasiliano.

KAMPUNI YA *ZANTEL*

Mhe. Spika, Kampuni ya Simu ya *Zantel* ni kampuni iliyoanzishwa hapa Zanzibar na serikali ina hisa katika kampuni hii na kwa hivi sasa haina wateja wengi hapa Zanzibar.

Kamati inazipongeza jitihada za kampuni hii kuongeza huduma zake zikiwemo za *Internet* na kuongezeka kwa eneo la mtandao wake na kujiunga na mfumo wa kutumia mkonga wa baharini na kuwa mchangiaji mkubwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa kuhitimisha malengo ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi naomba Baraza kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 13,167,000,000 na kuidhinishwa makusanyo ya shilingi 1,653,500,000 kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na kuipitisha Bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba yangu binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Muyuni naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Ali Shehe (Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi): Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya iliyotuwezesha kuhudhuria kikao hichi. Aidha, naomba nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii ya

kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naomba pia uniruhusu kuwashukuru sana wananchi na hasa wanachama wenzangu wa CUF wa Jimbo la Chake Chake kwa mashirikiano na imani zao zilizothibitika kwangu kwa kipindi chote cha utumishi wangu jimboni na kwa kupitia kura za maoni zilizofanyika hivi karibuni matawini mwetu. Wingi wa kura walizonipa zinadhihirisha imani zao kwangu. Nami kwa mara nyengine tena naahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kuendelea kushirikiana nao na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote hadi pale maendeleo kamili yatakapopatikana jimboni hapo. Siku zote imani huzaa imani.

Mhe. Spika, kwa umuhimu wa kikao hichi naomba niitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary Kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika Baraza la Wawakilishi kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kwa kuniteua kushika nafasi hii ya Uwaziri Kivuli tangu pale kwa mara ya kwanza nilipokanyaga ukumbi huu. Nakiri kwamba Mhe. Abubakar kama kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani mimi na wenzangu ambao tulikuwa wapya mwaka 2005 ametusaidia sana kutujengea uwezo wa kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi wetu majimboni. Mhe. Abubakar tunakushukuru sana.

UMUHIMU WA SEKTA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Mhe. Spika, Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi ina umuhimu mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yoyote ile ulimwenguni. Hakuna nchi yoyote iliyoendelea au iliyopiga hatua kuelekea kwenye maendeleo kama haikutilia maanani umuhimu wa kuimarisha miundo mbinu katika sekta hii.

Zanzibar yetu ina historia ndefu sana katika kuanzishwa kwa Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi kama vile ujenzi wa muundo mbinu katika usafiri wa baharini, anga na nchi kavu. Kadhalika haikubaki nyuma katika historia ya uanzishwaji wa Sekta ya Mawasiliano ya Simu kwa miaka mingi sana. Laitani kama tungelikuwa makini katika kuendeleza yale tuliyoyakuta na kuanzisha mapya na yaliyo endelevu, hapana shaka Zanzibar ya leo ingekuwa ni ya kupigiwa mfano katika Bara letu la Afrika.

Mhe. Spika, sina budi kwa niaba ya Kambi yangu ya Upinzani kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Alhajj Dk. Amani Abeid Karume kwa jinsi alivyoanza kuchukua hatua za kuanzisha na kuimarisha Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi nchini, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa MKUZA, Dira ya Maendeleo ya 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Millenia

(Millenium Development Goal) sera na mipango ambayo lengo lake ni kukuza uchumi wetu pamoja na kupunguza umaskini kwa wananchi wa Zanzibar.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2009/10 NA 2010/2011

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka 2009/2010 ilibeba kauli mbiu ya kuwa ni BAJETI YA KUIMARISHA MIUNDO MBINU ambapo kwa upande wa makusanyo wizara ilikisia kukusanya jumla ya shilingi 1,500 milioni kwa mapato ya ndani. Kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi. 3,744 millioni. Kwa kazi za maendeleo wizara ilipangiwa kutumia shilingi 64,584,350,000.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011 bajeti iliyobeba kauli mbiu ya BAJETI YA MAENDELEO NA DEMOKRASIA, wizara imeazimia kukusanya jumla ya shilingi 1,653,500,000 wastani wa ongezeko la asilimia 9 ukilinganisha na makisio ya mwaka jana. Kwa upande wa makisio ya matumizi ya kazi za kawaida wizara imekisia kutumia jumla ya shilingi 4,067 milioni sawa na ongezeko la asilimia 8. Kwa upande wa makisio ya matumizi ya kazi za maendeleo wizara imekisia kutumia jumla ya shilingi 52,721,230,000 sawa na upungufu wa asilimia 18 ikilinganishwa na makisio ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka 2009/2010 miradi ya maendeleo kwa Afisi Kuu Pemba ilikusudia kufanya matengenezo ya barabara zifuatazo:

1. Barabara ya Mkanyageni – Kangani
2. Ujenzi wa barabara ya Mgagadu – Kiwani
3. Ujenzi wa barabara tatu za Pemba
4. Ujenzi wa barabara za Kusini Pemba
5. Ujenzi wa barabara Ole – Kengeja
6. Kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Karume

Idara ya Mipango na Sera nayo kwa upande wake ilikusudia:

1. Kufanya matengenezo ya ofisi ya *Maritime* – Malindi.
2. Matengenezo ya ofisi ya leseni na ujenzi wa ukuta wa karakana.

Idara ya Anga nayo ilipanga kufanya:

1. Matengenezo ya barabara ya kuruka na kutulia ndege.

2. Kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar.

Kwa upande wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara ilikusudia:

1. Kufanya matengenezo ya barabara ya Mpendae/Nyumba mbili.
2. Ujenzi wa barabara ya Pale – Kiongele.
3. Ujenzi wa barabara kuu za Unguja.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika bajeti ya 2009/2010 kwa upande wa Afisi Kuu Pemba, wizara imeanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya:

1. Mtambile – Kengeja – Mwambe (fungu la barabara 6 za Kusini Pemba)
2. Mtambile – Kangani (fungu la barabara 6 za Pemba)
3. Wete - Konde (fungu la barabara 3 za Pemba)
4. Mgagadu – Kiwani (fungu la barabara zinazogharamiwa na SMZ)
5. Mchakato wa ujenzi wa barabara za vijiji vya Kaskazini Pemba zinazogharamiwa na SMZ pamoja na Serikali ya Marekani kwa kupitia mfuko wake wa akaunti ya changamoto ya millenia ambao tayari wameshaanza kufanya tathmini ya mali za watu kwa ajili ya ulipaji fidia pamoja na *designing*.

Idara ya Mipango na Sera imekamilisha ujenzi wa ukuta wa karakana na matengenezo ya ofisi ya leseni.

Mhe. Spika, Idara ya Anga nayo kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia imekamilisha kazi ya urefushaji wa njia ya kuruka na kutulia ndege katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar pamoja na kuanza kazi ya ujenzi wa uzio wa uwanja huo chini ya wakati uliopangwa. Kambi yangu ya upinzani inatoa pongezi za dhati kwa Benki ya Dunia kwa kazi hiyo nzuri ya kukamilisha kazi chini ya wakati.

Mhe. Spika, ukiacha mbali miradi ambayo imeanza kutekelezwa, miradi mingine yote iliyoainishwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka jana imeainishwa tena kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha pamoja na ongezeko la miradi mipya mitatu kama vile:

1. Ujenzi wa Ofisi Kuu ya Wizara
2. Ujenzi wa barabara ya Amani – Mtoni

3. Ujenzi wa barabara katika maeneo huru

Mambo muhimu yaliyojitokeza katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2009/2010 na mtazamo wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu 2010/2011 ni dhahiri utagundua mambo yafuatayo:

1. Kuna ongezeko dogo la makisio ya makusanyo ya ndani kwa mwaka huu ya asilimia 9 ukilinganisha na mwaka jana.
2. Kuna ongezeko la makisio ya matumizi ya kazi za kawaida ya asilimia 8.
3. Kuna upunguaji wa makisio ya matumizi ya kazi za maendeleo ya asilimia 18.
4. Kuna kasi ndogo ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo iliyochangiwa sana na kutopatikana kabisa ama upatikanaji mdogo wa fedha zilizoidhinishwa na Baraza hili katika miradi inayofadhiliwa na SMZ, pia kuna kukosekana kwa mchango wa fedha za SMZ katika miradi ambayo kwa asilimia kubwa inafadhiliwa na washirika wetu wa maendeleo.

Mhe. Spika, Kambi yetu ya Upinzani ilitegemea kuwa kwa kuimarika shughuli za bandari ya Malindi, kumalizika kwa utanuzi wa njia ya kurukia na kutulia ndege ambayo matumizi yake yataendana na mwaka huu wa fedha, mapato ya fedha kwa mwaka huu yataongezeka zaidi ya kiwango kilichokisiwa mwaka 2009/2010 katika kodi ya kiwanja cha ndege, malipo ya usajili wa meli pamoja na makisio ya ada ya usalama *(Airport Safety Fee)*, ni bahati mbaya kwamba makisio yaliyoainishwa kwa mwaka jana ni yale yale yaliyoainishwa kwa mwaka huu.

HALI YA UTEKELEZAJI WA IDARA NA MASHIRIKA

Mhe. Spika, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hufanywa kupitia Idara na Mashirika yaliyo ndani ya Wizara hii kama ifuatavyo:

1. Idara ya Mipango na Sera
2. Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara
3. Idara ya Usafiri na Leseni
4. Idara ya Anga
5. Shirika la Meli na Uwakala
6. Shirika la Bandari

Mhe. Spika, kwa ujumla nimeshaeleza mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka uliopita na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka huu 2010/2011 kwa kila idara. Ni muhimu kwa sasa kuainisha muhtasari wa changamoto zinazoikabili kila idara katika utekelezaji wa bajeti ili kufikia lengo la msingi la Taifa letu la kuimarisha uchumi na kupunguza umasikini wa wananchi kupitia sekta hii.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, changamoto kubwa inayoikabili idara hii ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usafiri *(National Transport Policy)* ya mwaka 2008 pamoja na utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri *(National Transport Master Plan).*

Katika Sera na ndani ya Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri kuna mambo kadhaa na ya muhimu yameainishwa kwa lengo la kufanyiwa kazi HARAKA na serikali kama ni uwekaji wa msingi wa uimarishaji wa Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa mfano:

Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri umeagiza kuanzishwa kwa HARAKA mpango unaozishirikisha Sekta Binafsi *(Public Private Partnership)* katika ujenzi wa miundo mbinu kama vile bandari, madaraja, barabara, viwanja vya ndege na kadhalika. Kambi yangu inahoji je, serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa agizo hili la Sera na Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri?

IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA

Mhe. Spika, moja kati ya idara inayokabiliwa na changamoto kubwa ni Idara hii ya Ujenzi na Utunzaji Barabara. Pamoja na juhudi inayochukuliwa na serikali katika kutafuta washirika na kutiliana saini, bado barabara nyingi za vijijini *(feeder roads)* zinazounganishwa na barabara kuu hazijaguswa na hivyo kusababisha kushuka kwa uzalishaji wa shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji na kuathiri sana biashara ya utalii na uwekezaji

Mhe. Spika, mapungufu ya kibajeti na usimamizi yamepelekea ukosefu mkubwa wa vifaa kazi, zana nzito na utaalamu kitu kinachopelekea kudorora kwa utekelezaji wa ujenzi wa barabara zetu.

IDARA YA LESENI NA USAFIRI

Mhe. Spika, changamoto kubwa zinazokabili utekelezaji wa idara hii ni:_

1. Upandaji wa nauli kiholela katika vyombo vya usafiri.

2. Ongezeko la ajali za barabarani.

Pamoja na biashara ya usafiri kuwa huru, serikali inapaswa kusimamia na kuratibu suala zima la upangwaji wa nauli kwa usafiri wa nchi kavu. Pamoja na hili Kambi yetu ya Upinzani inaiomba serikali ifanye zaidi utafiti juu ya kuongezeka kwa ajali za barabarani. Tunavyohisi, ongezeko la ajali za barabarani zinachangiwa na mambo mengi kama vile:

- Ubovu na hali ya barabara zetu
- Ubovu wa magari
- Nidhamu mbovu za madereva
- Elimu duni kwa watumiaji wa barabara na kadhalika.

Mhe. Spika, hatudhani kuwa kupiga marufuku matumizi ya vyombo vya abiria (dungu) kuwa kutakuwa ndio suluhisho la kutokea kwa ajali za barabarani. Karibuni katika barabara ya KOANI gari la maji la Kampuni ya *MECCO* lilivamia gari ya abiria ya Machui na wananchi wenzetu wapatao 6 walifariki dunia papo hapo (namuomba Mwenyezi Mungu awalaze pahala pema peponi). Amin.

IDARA YA ANGA

Mhe. Spika, Idara ya Anga nayo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazodhoofisha maendeleo ya viwanja vya ndege hususan kiwanja cha Karume Pemba. Tatizo ni lile lile la idara kutokuingiziwa fedha kwa miradi iliyoainishwa kwa miaka mitatu iliyopita, kama vile ujenzi wa uzio, uwekaji wa taa, uwekaji wa genereta, marekebisho ya jengo la abiria na kadhalika.

Kambi yetu inarudia kuipongeza Benki ya Dunia na inarudia kusikitishwa sana na tabia ya serikali ya kutokuchangia sehemu ya fedha inayoahidi kwa miradi hiyo.

SHIRIKA LA BANDARI NA SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA

Mhe. Spika, mashirika haya ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta ya usafiri na usafirishaji wa majini kati ya visiwa na nje ya visiwa vyetu.

Shirika la Meli linakabiliwa na hali mbaya kiuwezo unaopelekea tatizo katika uendeshaji. Shirika linakabiliwa na madeni mengi, lina idadi kubwa ya wafanyakazi wasio na kazi ya kufanya, lina tatizo la mtaji na kadhalika.

Kambi yetu ya Upinzani kwa kutambua na kufahamu umuhimu wa shirika hili tunaishauri serikali kuchukua hatua za dharura kulinusuru shirika hili muhimu kwa kufanya mambo yafuatayo:-

1. Serikali itafute namna ya kufuta madeni ya shirika.
2. Serikali itafute namna ya kulisaidia shirika katika kuwapunguza wafanyakazi ambao hawahitajiki kwa sasa.
3. Serikali itafute namna ya kulisaidia shirika kupata mtaji, sambamba na kupata meli zitakazotoa huduma ndani na nje ya visiwa vyetu.
4. Serikali ilifanyie mageuzi ya kimuundo utakaokidhi shirika kujiendesha zaidi kibiashara.

Mhe. Spika, kwa upande wa Shirika la Bandari linaendelea vizuri, ingawa linakabiliwa na changamoto nyingi zinazokwamisha maendeleo ya shirika hilo.

1. Shirika linakabiliwa na wingi wa wafanyakazi pamoja na mishahara duni.
2. Shirika linakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya upakuzi na upakiaji zana nzito, eneo la kuhifadhia makontena pamoja na vyombo vya uokoaji.
3. Bandari yetu ya Malindi inakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa maji (hususan wakati wa maji kupwa) hali inayopelekea shida na hofu kubwa ya kuganda kwa meli wakati zinapofunga gati.
4. Bandari yetu ya Mkoani inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vifaa na zana nzito, pia tatizo la kudidimia kwa bandari inaonekana kuwa ni kidonda ndugu.

Mhe. Spika, Katika kukabiliana na ukosefu ama upungufu wa vifaa kazi katika bandari zetu, kampuni ya Al-Ghubra Marine Services Ltd, inayomiliki meli tatu (3) zinazotoa hudma kati ya bandari za Unguja, Pemba, Dar-es-Salam na Tanga ilikuomba kuiruhusu kuagiza *crane,* kwa ajili ya kusaidia kazi za ushushaji wa bidhaa katika bandari ya Malindi, kwa ajili ya meli zao na shughuli nyengine bandarini hapo. Ombi hilo lilifanywa tangu mwezi wa April 2010. Kwa bahati mbaya hadi leo ufumbuzi wa ombi hilo haujapatikana. Kambi yangu imefadhaishwa na kusikitishwa sana na tokeo hilo, linalokwenda kinyume kabisa na dhamira ya Serikali la kuwavutia na kuwashajiisha wawekezaji kuwekeza nchini mwetu. Kwa msingi huo tunakuomba Mhe. Waziri ulieleze Baraza hili ni sababu zipi zilizopelekea kulikataa ombi la mwekezaji huyo, na kama hukumkatalia, ni sababu zipi nyengine zilizopelekea ukwamishaji wa utekelezaji wa ruhusa yako?.

Mhe. Spika, Zanzibar yetu inafursa nzuri sana kijiographia katika uwekezaji wa miundo mbinu ya bandari. Tunahitaji kuimarisha bandari zetu kama ile ya Wete, Wesha na Mkokotoni kwa ajili ya kukuza usafirishaji kati yetu na mwambao wa Tanzania Bara na Kenya; tunahitaji kuimarisha bandari ya Mkoani na kujenga bandari nyengine ya Nungwi, kwa nia ya kuimarisha usafiri wa ndani. Kadhalika tunahitaji kuwekeza katika ujenzi wa bandari ya Mkumbuu na Mpigaduri kwa lengo la uhudumiaji wa meli za Kimataifa.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa maendeleo ya haraka ya kujenga uchumi wetu sambamba na kunyanyua hali ya kipato kwa wananchi wetu, serikali haina budi itilie maanani sana ujenzi wa miundo mbinu bora na ya kisasa ya Mawasiliano na Uchukuzi. Ni kwa kufanya hivyo tu ndipo uwekezaji katika sekta ya viwanda utaimarika, hali ya biashara ya uuzaji na uagiziaji itaimarika, kadhalika biashara ya utalii. Shughuli za uzalishaji kwa wananchi wetu nazo pia zitaimarika. Tunaamini na ndivyo ilivyo kwamba kwa serikali pekee kujipiga kifua kujenga na kukamilisha ujenzi wa mabarabara yote mijini na vijijini, kujenga viwanja vya ndege vyenye sifa, kujenga mabandari yanayoweza kutoa ushindani wa kibiashara katika ukanda wa mwambao wa Afrika ya Mashariki, kama ilivyokuwa ikitawala biashara katika mwaka wa 1892 katika eneo lote kuanzia Somalia hadi Sofala nchini Msumbiji. Hilo kwa Serikali pekee haliwezekani, iwapo haikuihusishwa kikamilifu sekta binafsi katika uwekezaji ndani ya sekta hii. Kambi yetu inatangulia kuishauri serikali ijayo iitilie maanani sana hoja hii.

Mhe. Spika, kwa kumaliza naomba niitumie fursa hii kwa kuwashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuanzia Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi wote wa Idara na Mashirika, Afisa Mdhamini Pemba na watendaji wake, kwa mashirikiano yao walionipa katika kipindi ambacho naifanyia kazi wizara hii kama Waziri Kivuli. Nawashukuru sana wawakilishi wenzangu kwa mashirikiano yao kwa kipindi chote, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamjaalia kila anaetaka kurudi katika Baraza hili atarudi na hii ni Magharibi, dua hii inakuja wakati wa Magharibi.

Mhe. Spika, nitakuwa sijafanya haki ya kutokushukuru wewe Mhe. Spika, si kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa, bali kwa jinsi ulivyoliongoza vyema Baraza hili. Sote tunakiri kuwa hali tuliyoanza nayo mwishoni mwa 2005 ni tofauti na tunayomalizia nayo. Wewe umekuwa ni muhimili muhimu sana uliotumika kujengea mazingira haya. Tumuombe Mwenyezi Mungu atupeleke mbele na kamwe asiturudishe nyuma tena. ‘Mcheza kwao hutunzwa’, kwa msingi huo na kwa kuepusha kisa cha muomba jamvi, nakuomba Mhe. Spika, utangaze nia. Nakushukuruni kwa kunivumilia na kunisikiliza kwa makini.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi kwa bajeti yake ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mameneja na wafanyakazi wote wa taasisi mbali mbali wa wizara hii, kwa kuhakikisha kwamba mawasiliano ni nyenzo muhimu kwa harakati zetu za maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nazipongeza taasisi zote za wizara hii kwa kazi nzuri walizozifanya kwa kipindi cha miaka mitano hii tuliyokuwanayo, hasa tukiangalia kwamba katika Baraza hili hakuna hata mwakilishi wa jimbo moja ambaye hakufaidika. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya na nitatangazia kwa upande wangu mengine nitasema baadae.

Mhe. Spika, naipongeza Idara ya UUB, ujenzi na utunzaji wa barabara kwa kazi nzuri waliyoifanya katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Maana Mhe. Spika, kama tutasimama kuzitaja hizo barabara kwenye ukurasa wa 58 na 59 basi ni kielelezo tosha kwamba kila mmoja kafaidika katika nchi yetu hii.

Mhe. Spika, lakini mimi napongeza kwa upande wa Jimbo langu la Kwahani. Barabara ya kutoka kwa Biziredi Mikunguni mpaka Amani, barabara ya kutoka *taxi stand* Mwembeladu mpaka Posta, barabara ya kutoka Miembeni ambayo sasa hivi inakwenda Changamoto imekaza nguvu na Mhe. Waziri nampongeza kwa dhati kabisa yeye mwenyewe na watendaji wake Mkurugenzi na watendaji wote wa UUB kwa kutuwekea miundombinu mizuri ya barabara hii na kuhakikisha kwamba ile adha ya kero ya miaka yote imeondoka.

Namshukuru Mhe. Waziri kila nilipomuomba na nilipomweleza alinifahamu. Kwa hivyo, jimbo la Kwahani, kuanzia Kwa Biziredi Amani, yaani Mikunguni Amani, ukija Magomeni mpaka Kwa Boko, ukitoka Kwa Boko na ukielekea Kidongo Chekundu Kwa Chimbeni kule mpaka Kwa Moh'd Ali mpaka Polisi na kuelekea Miembeni, hapa Kijangwani ndio sikuambii tena Mhe. Spika. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote. Lakini pia niipongeze serikali nzima kwa kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara na mambo mengineyo ndio uhai wa nchi.

Mhe. Spika, naamini usimamizi mzuri wa Mhe. Rais kwa shughuli mbali mbali za miundombinu hii, akisaidiwa na Mhe. Waziri Kiongozi, Waziri wa Nchi

Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi. Hii inaonesha wazi kwamba harakati zinaweza kutekelezeka zikisimamiwa vizuri. Nampongeza sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi nzuri ya kufuatilia na kuhakikisha kila alilolipanga linafanikiwa. Hongera Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitalizungumza kwa ufupi kabisa, kwa sababu naangalia muda nao unakwenda haraka. Mhe. Spika, Mhe. Machano Othman Said ni rafiki yangu sana katika Baraza hili, na urafiki huu haukuanza kwenye Baraza la Wawakilishi, lakini toka tunakotoka, lakini zaidi ni hapa Barazani na kwenye kamati moja tumekaa wote, akapata U-Naibu Waziri akaondoka, akaja akapata tena Uwaziri nikampongeza kamasikosei katika kamati yangu tulikuwa wote.

Mhe. Spika, lakini kubwa zaidi hasa katika mambo yetu ya michezo kwenye timu ya *Simba Sports Club*. Mimi na yeye mara nyingi tunakuwa pamoja hata kwenye uwanja wa uhuru Dar es Salaam tunakutana, ili kuhakikisha tunamwangalia mnyama akipambana na Yanga. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhihirisha wazi kwamba sina kinyongo katika nafsi yangu, wala sina chuki na mtu. Lakini cha kuelezana tuelezane kwa maslahi ya wananchi wetu na taifa letu.

Mhe. Spika, Wizara ya Mawasiliano na Uchukizi ina nafasi kubwa sana ya kutoa ajira kwa wananchi wetu, kuanzia vyombo vya baharini, vyombo vya usafiri wa angani, vyombo vya usafiri wa daladala na abiria na gari za mizigo pamoja na *taxi*. Lakini ukichukua hivi vyombo vya nchi kavu vya abiria na mali zao, basi unaweza kupata vijana wasiopungua 4,000 au zaidi kwa daladala zilizokuwepo katika nchi yetu. Namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na kwamba juzi katika maswali na majibu tulijibiwa kwamba labda kuna zogo au kuna mambo ambayo yanajitokeza mpaka daladala zikafika kuwekewa kikomo kuwa mwisho ni mwezi wa April mwaka 2011.

Kwa hivyo, Mhe Spika, namuomba kwa dhati Mhe. Waziri, vijana wanaopata ajira hapa kwenye daladala basi wanatusaidia sana kwenye majimbo yetu na sehemu mbali mbali. Pia baada ya kujisaidia wao na wanazisaidia na familia zao. Kwa hivyo, naomba daladala zisiondoshwe Mhe. Spika. Nasema hili sina daladala ninayoitegemea katika maisha yangu, lakini majimboni kuna vijana wetu ambao kwa asilimia kubwa wametuleta katika Baraza hili. Halafu kesho hao hao vijana tunawaomba tena kwa serikali iliyoko madarakani pamoja na Chama cha Mapinduzi wairudishe hapa.

Kwa hivyo, namuomba kwa moyo safi, namuomba kwa imani za wananchi wetu na namuomba kwa walionituma kwa asilimia mia moja, kila mwenye daladala yake anaamini kuwa ndio maisha ya pato lake na kila mwenye

daladala yake amepata wafanyakazi wawili ambao ndio ajira yeye mwenyewe anapata na wale vijana wanapata na wanazisaidia familia zao. Namuomba sana Mhe. Waziri kanuni inatungwa, lakini kanuni hiyo pia huwekwa kando ili maendeleo ya nchi yetu yaendelee.

Mhe. Spika, leo kanuni imebadilishwa hapa. Tulivyoingia asubuhi ilikuwa hakuna kusoma hotuba ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini kanuni iliwekwa kando, jioni tukaletewa *order paper* mpya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, inawezekana hakuna lisilowezekana. Naamini katika kitabu hiki kaeleza vizuri Mhe. Waziri. Kama kuna matatizo kwa madereva basi waelekezwe, kama kuna matatizo mengine waelekezwe, kama kuna magari mabovu yaondoshwe. Lakini mimi namuomba sana Mhe. Waziri tuangalie jamii inayowategemea hawa wanaofanyakazi miaka 30 au 40.

Mhe. Spika, kuna watu wetu wengi wako nje na tunasema ukikaa nje basi saidia kwenu. Kuna wengine wameleta kidaladala kimsaidie mzee wake na familia yake. kwa bahati mbaya leo ukimuambia hiki hatukitaki tena tunataka maringi sita, hana uwezo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ikiwa tutaleta mfumo wa lazima kuanzia madaladala ya maringi sita, basi watu watakaofaidika ni wachache sana. Watu wengine wanapiga kelele wanasema bora ije hiyo.

Mhe. Spika, kwa sababu aliyestaafu jeshini, polisi au sehemu yoyote ya kazi, mfano kama kapata milioni zake 10 au 12 kisha akanunua kidaladala. Halafu leo ukisema kwamba hizi daladala ziondoshwe na ziletwe nyengine za maringi sita basi hana uwezo tena yule wala hana pakuipata. Siku nyengine ile itakufa pale pale ndio mwisho wa safari yake.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri pamoja na uzuri wote tunaosifia wizara yake na uzuri wote wa maendeleo katika nchi yetu na miundombinu mizuri, bado kuna haja ya kuhakikisha kwamba daladala za wanachi wetu katika nchi yetu waachiwe waendelee na biashara zao. Lakini kama kuna mwelekeo wa baadae basi waambiwe, daladala zilizokuwepo katika nchi hizi ndio za mwisho, sasa hivi tunataka mtuletee mwelekeo huu au za aina hii, huo ndio utaratibu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili aliangalie kwa moyo wa imani kabisa.

Mhe. Spika, nakuhakikishia kama utaitoa kauli basi unaweza kufanyiwa maandamano ya furaha na maandamano ya kusherehekea ushindi wako na *Wallah* utashinda, tena utashinda kwa kishindo mheshimiwa. Mimi mmoja nitakupigia debe popote. Mhe. Spika, hii ndio changamoto ya wananchi wetu wanavyotaka, kwa sababu wananchi wetu wamekubali wito wa kuitumikia nchi yao kwa kila sekta. Sekta ya usafiri wa nchi kavu imechukua asilimia kubwa

sana vijana wetu. Kwa hivyo, nadhani hili kalisikia na kama kalisikia atalifanyia kazi na kazi yenyewe kama nilivyotangulia kusema kwamba mimi Mhe. Machano ni rafiki yangu, sina haja ya kuzuwia bajeti, kwa sababu hata nikizuwia bajeti si mshindi yeye nitaishinda serikali yangu na hilo silifanyi hata siku moja.

Mhe. Spika, nipo hapa kwa kipindi cha tatu hiki, sijasema leo nazuia shilingi, hakuna lugha hiyo. Lakini nina utaratibu wa kuhoji au kuelelezwa ili tufanikiwe. Namuomba sana Mhe. Waziri hilo alifikirie na alifanyie kazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitalizungumza kidogo ni kuhusu hali ya maendeleo katika sehemu mbali mbali zimeendelea vizuri, mawasiliano mazuri na mambo mengine yote mazuri. Pia tuwapongeze wenzetu wa Shirika la Bandari sasa hivi kusema kweli tunakotoka ni mbali sana na tulipo. Shirika la Bandari hivi sasa ni shirika ambalo kwa kila hali lina uwezo wa kufanya kazi zake kikamilifu na lina uwezo kwa kuhimili tena mara moja. Kwa hivyo, nimuomba Mkurugenzi na *management* yake, waongeze bidii na wahakikishe kwamba vifaa walivyokuwa navyo vipya vinahifadhiwa na vinalindwa kwa asilimia mia moja.

Kwa sababu Mhe. Spika, ukiwa na gari mpya na aliyekuwa na gari tatu kukuu basi kunatofauti. Kwa hivyo, tofauti ya bandari sasa hivi imejitokeza sana na kazi zinakwenda vizuri. Kwa hivyo, namuomba Mkurugenzi kwa kupitia Mhe. Waziri afanyekazi zake vizuri na aendelee na awatunze wafanyakazi wetu ili waendelee vizuri.

Mhe. Spika, jengine napenda niipongeze Idara ya Anga, kwa sababu tunasema hivi sasa harakati za maendeleo zimekuwa na moja katika kitu ambacho tunakitegemea ni Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, Uwanja wa Ndenge umebadilika kwa asilimia kubwa sasa hivi. Hivi sasa tunategemea kwamba mara baada ya kukamilika kwa uwanja ule harakati nyingi zitaongezeka katika uwanja wetu. Mhe. Spika, mimi naomba kwamba vifaa bora na vya kileo viwepo katika uwanja wetu. Anafika mgeni anachukua mgeni wake anaondoka bila matatizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie, lakini najua madhali tunaweka upya mradi huu mzuri basi na mambo yote yatakuwa salama na yataendelea vizuri.

La mwisho Mhe. Spika, ni kuhusu sekta binafsi. Katika mambo mbali mbali kama usafiri wa baharini, usafiri wa anga kama nilivyosema mapema. Lakini usafiri wa baharini Mhe. Spika, una changamoto kubwa kwa maendeleo ya wananchi wetu. Zanzibar ni sehemu ya visiwa vya Unguja na Pemba na Tanzania Bara ndio inategemea kwa usafiri kwa asilimia kubwa wananchi wetu kutumia usafiri wa baharini.

Namuomba Mhe. Waziri pana kila sababu na haja ya kufuatiliwa vyombo vyetu vya baharini viwe na usalama. Kama juzi tulipokea taarifa moja Mhe. Spika, kwamba *Seagull* iligonga jahazi moja ambayo ilipakia machupa ya bia yanakwenda Dar es Salaam. Lakini kwa bahati mbaya *Seagull* ile baada ya kugonga tu wakasimama kidogo wakatia pozi, kisha wakatia gia pale pale wakenda zao. Wakawaacha wale jamaa wakasumbuka, nasikia sijui, *captain* anatafutwa mpaka leo hajulikani aliko, yaani nafikiri kakimbia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje atupe maelezo kwa sababu tunasema siku zote, wewe una chombo kikubwa umuonee huruma huyu mwenye chombo kidogo. Leo kwa bahati nzuri wako karibu na bandarini pale wamekwenda kuokolewa, lakini kama wako kwenye maji mengi mheshimiwa basi wanakufa na kupoteza maisha yao, hatuna faida kwa mwelekeo kama huo. Namuomba Mhe. Waziri busara itumike kuliko uwezo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kabisa. Mimi leo suala langu kubwa lilikuwa ni daladala tu. Nadhani Mhe. Waziri kalisikia, atalitolea jibu zuri. Ninamuahidi tena akilitolea jibu zuri basi akialikwa maandamano atakayofanyiwa yeye kupongezwa na mimi anialike nimpigie debe katika Jimbo lake apite kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ninawatakia wajumbe wenzangu wote tumsaidie Mhe. Waziri ili kuweka miundombinu kwa manufaa ya nchi yetu, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni ya leo tukawa tuko hai na wenye afya njema, kuweza kuja kujadili mambo yetu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tuyashinde matatizo yetu.

Pili, Mhe Spika, nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa pili baada ya wahusika wakuu Mhe. Waziri, Mwenyekiti na Waziri Kivuli hatima yake na mimi nimefuatia katika kutoa mawazo yangu.

Lakini jambo la tatu, nimshukuru Mhe. Waziri Kivuli. Kwa kweli japokuwa ni swahib yangu, lakini kafanya kazi nzuri na yeye mwenyewe alisema kuwa mcheza kwao hutunzwa na mimi namwambia hongera. Nafasi ya uwaziri anaiweza, sio Waziri Kivuli ni uwaziri kamili anauweza. Kwa hivyo, nina imani kama serikali inayokuja *Inshaallah* itamuona na yeye awe waziri kamili.

La nne Mhe. Spika, ni kumpongeza Mhe. Machano Othman Said ambaye ni Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi, nimpongeze Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Lakini hususan pongezi zimuendee Afisa Mdhamini Pemba. Kwa kweli ni mtu mtaratibu anayekubali ushauri na ni mchapakazi. Naomba waziri isijekumuacha au serikali ijayo basi na yeye ijeimpe uwaziri rasmi sasa, maana aje kuchapa kazi zaidi.

Mhe. Spika, sitofanya haki, kila mmoja anamsifu wake na mimi nataka nimsifu wangu, ili *Inshaallah* atakapokuja kwenda katika Baraza Kuu, ajekuniona na mimi kwamba bado nafaa. Nimpongeze Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa busara hekima zake na akifuatiwa na Mhe. Haji Faki Shaali. Kwa kweli hekima zao na busara zao zinatupasa wawakilishi bado tuishi kwa furaha na tutowe michango yetu bila woga. Mwenyezi Mungu awajaalie kheri viongozi hawa na mafanikio.

Lakini katika shukurani zangu hizo nisimsahau *professor* ni mshauri wangu mkuu, Mhe. Hamad Masoud. Hiki ni kiungo kwa kweli, bila yeye mimi nasema mafanikio yangu yasingepatikana, bila yeye michango yangu nisingefafanua. Lakini kanisaidia vyema na nashukuru *Alhamdulillah* napata kuthubutu kusema kwamba najinata.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa niende kwenye bajeti. Nianze katika ukurasa wa sita, kuhusu sera na utawala. Katika malengo waliyojipangia ni kufanyia matengenezo uwanja wa ndege wa Pemba. Lakini bahati nzuri kama mjumbe wa kamati, kilio chetu kila siku tunasema bado uwanja jinsi na bajeti yake hii kama utafanya matengenezo, lakini kilio cha pale ni taa. Mhe. Spika, bado uwanja hauna taa, uzio uwanja hauna na wananchi kila leo wanavamia maeneo yale, tusije tukawatia kazi wananchi serikali ikajakupata majukumu ya kulipa fedha kwa fidia. Maana mwananchi akishajenga, nina imani na serikali kama kiongozi Karume ni lazima watalipa fidia tu.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Spika, wizara ingejitahidi japokuwa haijawa na nguvu ya kufanya matengenezo hayo yote kwa pamoja, basi wangeweka *block* kabisa kama hapa sio ruhusa mtu yeyote kuingia. Vyenginevyo wananchi tutawalaumu kwa sababu hawana makazi wengine.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 12 kuhusu sekta ya usafirishaji wa nchi kavu. Mhe. Ali Suleiman Ali kazungumza habari ya magari na kwa sababu ni matatizo. Lakini usafirishaji huu nasema bado wanafunzi wanapata matatizo. Wanafunzi wanateswa kwenye madaladala. Baadhi ya daladala haziwafanyii haki wanafunzi. Wanakwenda kituoni basi konda anawaambia hasa wanafunzi kaeni kando mimi natafuta abiria, maana yeye keshamuona hana haki na serikali imeshapitisha utaratibu. Kwa hivyo,

wangethaminiwa wanafunzi, kwa sababu mtoto wa leo ndio mzee wa kesho. Bila ya mtoto na sisi tusingefika hapa leo tulipo. Kwa hivyo, watoto wananyanyaswa na kuteswa katika daladala.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kwa kupitia kwenye vitengo vyake vya kusimamia mambo haya, basi wangepata siku maalum wakatembelea kwenye vituo vya daladala kama wale Manispaa wanaotembelea sehemu zao, basi wakaangalia matatizo, halafu yake atakayebainika na kosa akachukuliwa hatua, ili mwengine asifanye kosa hilo.

Vile vile Mhe. Spika, niungane na mwenzangu Mhe. Ali Suleiman Ali. Ajali ni ajali Mhe. Spika, ikiwa chombo kina miguu minne, miguu sita au miguu 16, ikiwa ajali imeshatokea basi itakwenda tu. Nina imani kama kweli kama mfumo umeshabadilika wa dunia, lakini kila jambo lina taratibu. Kusema kwamba daladala zilizokuwepo katika nchi hivi sasa zisifanye kazi, maana yake ni kuwazuwia waliowengi kukosa safari.

Mhe. Spika, rafiki yangu yeye anatetea kwa sababu ana usafiri, ana vyombo. Lakini mimi natetea jamii ambayo kuwa wana gari zile. Tunapowazuia zisifanye kazi maana yake ni kuwabana kupata maisha. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri suala hili, mwenzangu kasema labda zisiagizwe tena, hapana. Maeneo ya mjini, tufanye utaratibu kweli kipindi kijacho kuwe na gari nyengine kama wenzetu wa Bara. Lakini gari ndogo ndogo yapo maeneo ya vijijini zipangiwe, zisiondoswe moja kwa moja na hivyo ndivyo wenzetu Bara wanavyofanya.

Mhe. Spika, katika maeneo ya mjini kuna sehemu maalum zinapita zile gari za maringi manne, kuna maeneo mengine ni zile gari za ringi sita, lakini vijijini ni gari yoyote. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri hili akalizingatia. Vyenginevyo wengi atatutia umaskini. Haiwi daladala zangu mbili ninazojipatia rizki kusaidia jamii, halafu leo nikaambiwa zimekwama au zimesimamishwa, kwa kutembelea zote sitazimaliza. Nina gari ya kutembelea, nina daladala mbili, sijui nitachukua ipi niache ipi, hatimaye vpuri kwa sababu vimeshaanza kutumika vitakufa na gari iwe haifanyi kazi. Kwa hivyo, nina imani kwamba Mhe. Spika, hili Mhe. Waziri atalisikia na kwa sababu ni kilio cha wengi atalifanyia kazi. Kwa sababu bado ni waziri kijana na ni waziri mahiri anaweza kufanyakazi zake.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa huo huo wa 12 ujengaji na utunzaji wa barabara. Mhe. Spika, mimi niseme idara hii naipongeza na imejitahidi kufanya kazi zake. Hivi karibuni nilivyokuwa nikichangia hapa nilisema hakuna kizuri ambacho hakina upungufu, hiyo ndio sifa ya binadamu, mapungufu madogo madogo yatakuwa yapo. Wanazuoni wanasema ‘jitihada

wajada', unapofanyakazi kwa bidii. Wazee walisema 'juhudi hujenga bahati', unapofanya juhudi sana basi Mwenyezi Mungu hukupa bahati.

Mhe. Karume sio bure leo kuona Wazanzibari tunamsherehekea na kufurahika, kafanya juhudi. Kwa hivyo, naamini na mwengine yeyote atakayefanya juhudi kwa kazi zake kwa ukweli basi Mwenyezi Mungu humpa bahati na hatimaye watu hufahamu anachokifanya ni kipi. Kwa hivyo, ningeshauri Mhe. Spika, katika utunzaji na ujenzi wa barabara na ambazo zimeshajengwa kwa lami, fusi, kuziba viraka mashimo, *culvert* na mambo mengine. Mhe. Spika, angetuambia tuangalie kiambatisho namba 4 kweli zipo barabara zilizojengwa.

Lakini nataka niulize Mhe. Spika, kujengwa ni vipi na kusubiri kujengwa ni vipi, kwa hiyo nataka kufahamu maana hapa sijafahamu vizuri. Kwa kweli zipo barabara ambazo tayari zimeshajengwa na hivi sasa zinaendelea kujengwa kama vile barabara ya Mtambile/Kangani, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi juzi tulipokuwa katika ziara tulikwenda na gari zetu zikashindwa kufika na hivi sasa ndio zinapigwa *grader*. Lakini kwenye kiambatisho hicho anachosema Mhe. Waziri hizi anasema tayari na amedhiorodhesha pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wasi wasi wangu ukaendelea pale aliposema barabara ya Kojani tayari nayo inaanza kujengwa, maana inaanza kujengwa tayari imo katika shughuli hivi sasa. Sasa ile inajengwa au itajengwa baadaye. Kwa hivyo, hapa nataka kupata ufafanuzi wakati atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Vile vile mwaka jana tulizozana sana na Mhe. Waziri kuhusiana na barabara hii tena nilikuwa mkali sana kwenye fungu hili na Mhe. Waziri aliniambia aa! Tayari fedha tumeshapewa, lakini mimi nilimuuliza fedha mumepewa na nani na mimi nilisema Mfuko wa Bush wa Marekani na yeye akaniambia ni MCC na tukapingana hapo. Kwa hivyo, nataka kupata ufafanuzi kuhusu MCC na Mfuko wa Bush yote ni moja, yaani yote ni ya Wamarekani.

Kwa maana hiyo, aliahidi hapa kwamba fedha tayari zimeshaingizwa mwezi wa *April* na mwezi *August* barabara ya Kojani barabara itajengwa. Mhe. Spika, hivi sasa ni mwezi wa *August* 2050 au mwezi wa *August* 2000 na ngapi na hapa nataka ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako, lakini ninayo mengi na ulikuwa umkate mwenzangu unipe mimi na baadaye nikuletee jogoo japo mmoja. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia niende katika Gati ya Mkoani. Kwa kweli hapa naomba kutoa ushauri kwa sababu muda ni mfupi, kama tumeshindwa kuijenga vizuri huku juu, basi itobolewe na maji yawe yanapita chini au tulifanye bwawa la kuogelea na watu wanaposhuka meli kwanza waogelee na baadaye ndio waende majumbani. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli ni aibu leo tunachukua watalii na kwenda kutembea Kisiwa cha Pemba wanashuka meli wanaingia kwenye bahari, sasa wanauliza Pemba wapi, yaani hapa tumeshafika Pemba na tunakwenda nchi nyengine au vipi pale kwenye gati. Kwa hivyo, nashauri kama tumeshindwa kuijenga basi tuitoboe na maji yapite chini au vyenginevyo tulibadilishe liwe bwawa la kuogelea watu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako, lakini nilikuwa na mengi ya kusema. Nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Said Khelef Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi.

Vile vile sina budi kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, kabla sijasahau sina matatizo na Mhe. Waziri wangu, kwa sababu ni mwanangu. Kwa hivyo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli sina budi kumpongeza tena Mhe. Waziri kwa utendaji wake wa kazi. Mhe. Spika, leo nimepita njia ya bububu ambayo inaendelea kutengenezwa na ule ndio utengenezaji ambao tumezoea watu wa Unguja. Wakati walioanza kutengeneza njia ile walitupa matatizo makubwa sana wajengaji wale, yaani njia zilikuwa zinafungwa na kusababisha watu kupitia Mwera wananchi wanapata tabu, nauli zinazidi.

Lakini hivi sasa tumeona wanakata upande mmoja na upande mwengine wanaacha. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri.

Mhe. Spika, nikiendelea na pongezi zangu nimpongeze Mkurugenzi wa Barabara kwa juhudi zake pamoja na mashirikiano mazuri, pia alinisaidia vizuri kwa sababu nilikuwa na njia yangu kuanzia Kidanzini kuelekea pwani, kwa kweli alinipa *grader* na kazi imefanywa na njia imekamilika. Kwa hiyo, namwambia ahsante sana Mkurugenzi wangu wa Barabara. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, hivi kweli njia ya Bumbwini itajengwa. Kwa hivyo, hapa nataka atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri aje anipe majibu, lakini Mhe. Waziri ni mkakamavu kweli kwa kutuliza watu, yaani busara zake na hivyo ndivyo inavyotakiwa.

Mhe. Spika, kwanza ameanza kutanguliza *graders* mbili pamoja na lile la kushindilia moja tunayo kule, lakini yamelala tu na wala hayana kazi yoyote. Sasa nadhani ameleta kwa ajili ya kututuliza roho zetu. Tunakushukuru Mhe. Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

Hata hivyo, watu wa Bumbwini tunayo masikitiko makubwa sana. Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri alijibu kwamba mpaka hivi sasa kazi haitoendelea kwa sababu hazijapatikana shilingi milioni 5. Hivi kweli Mhe. Spika shilingi milioni 5 za kuhamisha mabomba ya maji kupeleka upande mwengine, mpaka hii leo. Sasa je, zikipatikana tukizitafuta na kuzileta Mhe. Waziri ataanza kazi kesho.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kufanya majumuisho atujibu, kwa sababu hali ngumu ya Bumbwini na tumeshachoka, yaani wananchi wa Bumbwini wananiuliza njia itajengwa lini Mhe. Said Khelef Ali na wala jawabu sina, kwani nitasema uongo na mimi kusema uongo siwezi, mimi tayari nimesharudi Makka Mhe. Spika na tulikwenda pamoja. Sasa kusema uongo siwezi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awajibu wananchi wa Bumbwini wakati atakapokuja kufanya majumuisho.

Suala jengine ni kuhusu minara. Mhe. Spika, iko siku hapa niliuliza swali la nyongeza na Mhe. Naibu Waziri alinijibu minara hii ikianza kujengwa wao wanashirikishwa, kwa sababu wao wanalifahamu suala hili. Sasa nilimuuliza swali kwamba kule kwetu kuna mnara umejengwa tena ni muda mrefu sasa haufanyikazi tatizo lake nini, pia pale kuna watu wawili kwa ajili ya kufanyakazi, lakini hivi sasa naweza kusema imeshafika mwezi wa 12 au 20 bado hawajalipwa fedha.

Mhe. Spika, alinijibu kwamba hilo si kweli, nadhani hawa wenzetu hawafuatilii haya masuala, kwa sababu mnara niliomuuliza sio ule ambao amenijibu na yeye amenijibu wa *Zantel* na ule uliopo mimi wala siujui ambao upo chini ya nyumba yangu. Kwa kweli sehemu yenyewe inaingia maji na wakati wowote mnara ule unaweza kung'oka na kutuua. *(Makofi)*

Sasa nilimuuliza, lakini alinijibu sivyo na mpaka leo sijapata jawabu, hivi kweli kuna ufuatiliaji hapa. Mhe. Spika, wakati mwengine husema hapa kwamba

watatujibu kwa maandishi, basi huoni barua na wala kuitwa na kukunong'oneza. Kwa hivyo, tuwaambie nini wananchi wetu kule na suala hili si zuri jamaa.

Mhe. Spika, kwa kweli mchango wangu si mkubwa nimalizie kwa Mfuko wa Barabara. Mhe. Spika, nauomba Mfuko wa Barabara kupitia Mhe. Waziri, ulione tatizo la Zingwezingwe kwa sababu walisema watalitengeneza na iko siku niliambiwa kwamba zipo shilingi milioni 10, lakini hadi leo sijaona utaratibu wowote kwa ajili ya matengenezo ya daraja ile.

Kwa kweli, daraja ile inatumiwa na watu wengi kwa ajili ya kwenda kwenye mashamba yao na kuendeleza shughuli za kilimo na hivi sasa haipitiki. Mhe. Spika, nauomba Mfuko wa Barabara ulishughulikie daraja lile.

Mhe. Spika, mimi sina mengi na wala ilikuwa nisichangie suala hili lakini sina jawabu la kuwajibu watu wa Bumbwini. Kwa hivyo, hapa naomba kumalizia. *(Makofi)*

Ahsante sana na ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, napenda kukushukuru na mimi kuniorodhesha kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi. Nampongeza kwa namna alivyowasilisha hotuba yake kwa ufupi sana na kuweza kufahamika, lakini mimi haijanitosheleza.

Pamoja na hayo, nawapongeza watendaji wake wote kwa taarifa ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2009/2010 ambazo zimeelezwa humu, nazipongeza kazi hizo. Kwa kweli kazi hizo tumeziona au tumezishuhudia kama zilivyoelezwa. Kwa hivyo, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu niwapongeze watendaji wote kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na taasisi mbali mbali za wizara hii.

Mhe. Spika, vile vile sina budi kutoa pole kwa Mhe. Waziri wa Wizara wa Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. *Brigadier* Mstaafu Adam Mwakanjuki, kutokana na maumivu aliyonayo na muda mwingi tumemkosa pamoja na huduma zake. Kwa hivyo, namuomba Mwenyezi Mungu ampe uzima na afya aendelee kujenga taifa hili kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyomuwezesha.

Mhe. Spika, najua wafanyakazi wa wizara hii wengi wao watakuwa na masikitiko, familia yake pamoja na mimi binafsi ninayo masikitiko kumkosa *Brigadier* Mstaafu Adam Mwakanjuki kuendelea na wizara hii. Kwa kweli tulikuwa tumeahidiana mengi kunitekelezea katika jimbo langu, hasa barabara ya Kidimni kwenda mpaka Jeshini na yeye mwenyewe alishawahi kwenda

kutembelea, Jumbi/Koani, lakini naona utenzi humu mwingi tu umo na wala sijatengenezewa mpaka hivi sasa.

Mhe. Spika, naamini kama angekuwa mzima Mhe. *Brigadier* Mstaafu, kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa ameshakwenda basi kazi hii ingekuwa imeshafanywa. Lakini ndio matakwa ya Mwenyezi Mungu hayana makosa. Hata hivyo, namuombea kwa serikali ya awamu ijayo japo kuwa hana uwezo basi hata kuwa mshauri wa wizara hii, yaani uwezo wa kufanyakazi hana, lakini akili yake itakuwa inafanyakazi basi aweze kutoa ushauri wa hapa na pale.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nianzie na mchango wangu kwenye Idara ya Mipango na Sera. Idara hii inahusika na Bohari Kuu pamoja na Karakana Kuu ya Serikali. Mhe. Spika, mwaka jana tulichangia umuhimu wa kuimarishwa Bohari Kuu pamoja na Karakana yake, tulielezwa kuwa serikali inayo nia ya kufanya hivyo, lakini kulikuwa na sijui utata au ukata katika serikali, kwa hivyo jambo hilo limeshindikana.

Lakini kwa bahati nzuri tumepata fursa nzuri Mhe. Spika ya msamaha wa madeni na tulifanya mengi. Kwa mfano, tumenunua magari pamoja na mambo mengine. Sasa kwa nini tumeshindwa angalau ile Bohari Kuu kushindwa kuijaza vifaa kutokana na fedha zile.

Aidha kuimarisha Karakana yetu Kuu kwa fedha zile, kwa sababu tulisema fedha zile tusizitie benki na sisi tunayo mahitaji mengi, kwa nini wizara hii isione kuna haja ya kumega na tulisema sana hapa.

Mhe. Spika, hivi sasa serikali kutumia maduka ya watu binafsi haipendezi hata kidogo. Kwa mfano, Wakoloni walikuwa na mambo mabaya, lakini baadhi ya mambo yao mengine yalikuwa mazuri, kuhakikisha serikali inakuwa na vifaa vyake maalum vya serikali.

Kwa kweli Bohari Kuu ilikuwa na uwezo wa kuhudumia vifaa tofauti vikiwemo vya ujenzi mpaka vya majumbani, yaani hata matofali mtu akitaka basi anapelekana *requisition* anapata matofali, mafuta ya taa, *petrol* pamoja na mambo mengine, lakini hivi sasa hakuna na badala yake kunakuwa na vurugu tu.

Kwa mfano, tunataka *furniture* kwa Mhe. Spika, tunaambiwa tukachukue kwa nani sijui, wakati zamani vyote unapata kutoka Bohari Kuu. Vile vile hivi sasa afisi ikihitaji mapazia basi mtu anakwenda kununua vitambaa kwa SUMA, hivi Nyumba ya Serikali inatiwa mapazia ya SUMA, majembe. Kwa kweli zamani majembe, mapanga yote ya serikali yanakuwa na *quality* maalum na

kununuliwa na kuwekwa kwa utaratibu mzuri pamoja na umadhubuti wake tena yametiwa alama.

Lakini hivi sasa vifaa vyote vinavyonunuliwa Mbuyuni pamoja na Juakali ndivyo vile wanavyonunua wananchi, yaani mtu yeyote anaweza kuvichukua na kwenda navyo nyumbani na wala huwezi kuvigundua. Kwa hivyo, Mhe. Spika athari mmoja ambayo serikali inashindwa kuitumia Bohari Kuu ni kwamba mali inapotea ovyo.

Mhe. Spika, kwa ufupi nasema umuhimu wa kuimarisha Bohari Kuu, ili mahitaji yote ya serikali yapatikane pale upo na tutakuwa tunapata vitu madhubuti. Sasa vitu kama hivi ambavyo mtu hawezi kukichukua nyumbani wakati wowote, kwa sababu atakapokichukua kinajulikana kwani kimeandikwa cha serikali au sahani imetiwa SMZ inajulikana kuwa ya serikali, lakini hivi sasa jambo hilo halipo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika ninasisitiza kuimarishwa kwa Bohari Kuu ya Serikali.

Halikadhalika Karakana Kuu ya Serikali. Kwa kweli magari ya serikali hivi sasa ni mengi na wala haipendezi magari kupelekwa chini ya miembe au *garage* za vichochoroni, kwa sababu wataalamu tunao. Sasa kwa nini tunashindwa kuimarisha Karakana yetu na Gari za Serikali zote zikashughulikiwa huko.

Kwa mfano, siku hizi kuna vifaa ambavyo havina kiwango vingi sana, yaani mtu anaweza kuona au kusema kwamba hiki kitu kizuri, lakini gari ya Mhe. Spika ikatiwa kitu kibovu na siku ya pili Mhe. Spika yumo kwenye msafara anakwama.

Mhe. Spika, vile vile tumesikia hapa kwamba yapo mafuta ya kuchekecha, ikiwa kwenye vituo vya mafuta hakuna mafuta basi mtu anaweza kwenda kuchukua Mikunguni au sehemu nyengine yoyote, kwa sababu hakuna utaratibu.

Kwa hivyo, lazima hivi sasa vyombo vya serikali viwe na mahala pake pa kupata huduma na sio ovyo na huu ni wakati mwengine. Mhe. Spika, nafikiri utaratibu wa kutumiwa taasisi zetu za serikali kwa vyombo vya serikali umuhimu wake upo na vyombo hivi viwili ninavyovitaja viko chini ya wizara hii.

Kwa maana hiyo, lazima Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze namna gani, mtazamo wake na kuna matatizo gani, fedha kama tulikuwa hatuna ndio hizo na kwa nini hakuweza kuimarisha Bohari Kuu

pamoja na Karakana Kuu kushindwa kuweka vifaa, kwa ajili ya gari zote za serikali zikahudumiwa pale, bado wanakwenda pale chini ya mti Miembeni au kwa Buda. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Idara ya Barabara ambayo ni kubwa. Kwa kweli ninamshukuru Mkurugenzi wa idara hii kwa jitihada zake, vile vile naishukuru serikali kwa ujumla kutokana na jitihada za Mradi wa Utanuzi wa Barabara Kuu, hatua waliyofikia ni kubwa. Kwa hivyo, mwelekeo wa kuinua ustawi wa watu pamoja na ukuzaji wa biashara na utalii hivi sasa utafanyika katika hali ya ufanisi.

Lakini bado tunacho kilio kwa barabara ndogo ndogo za vijijini kama nilivyoeleza barabara yangu ya Jumbi, kwa sababu kwenye kitabu hutiwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, kwa nini haiwezi kutengenezwa. Kwa kweli mwaka 2008/2009 nilipangiwa kwenye mfuko shilingi milioni 15, mwaka 2009/2010 niliambiwa shilingi milioni 45 na kama ilikuwa tatizo fedha na hivi sasa fedha zipo, kwa nini tumeshindwa hata kufukia mashimo.

Mhe. Spika, utasikia Mpendae/Mshelishelini na sijui kule kwa watu wanaojua kuvaa viatu na sisi kule tukanyage tope au vipi. Kutokana na hali hii wakati mwengine naweza kusema katika utengenezaji wa barabara ndogo ndogo kunakuwa na upendeleo Mhe. Spika, lazima niseme ukweli, kwa sababu sisi malalamiko yetu ya miaka mingi, tumetaja matatizo ya Jumbi/Koani kabla ya mji wa Mshelishelini haujakuwepo au Nyumba Mbili.

Kwa hivyo, juzi tu baada ya kuwepo hii mitaa ya Mshelishelini na barabara wanatengenezewa, wakati sisi Jumbi tunapiga kelele kwa muda mrefu, kwa sababu Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume amewahi kujenga robo kilomita huku na kule, kutokana na ule umuhimu wake. Lakini leo viongozi wote mpaka awamu hii ya sita bado hamjaona umuhimu wa barabara ile, hivi kweli ndio tunayatunza mazuri ya Marehemu Mzee Karume au alifanya makosa kuanza kujenga ah! Mhe. Spika, inasikitisha sana. *(Kicheko/Makofi)*

Suala jengine ni kuhusu mjenzi wa barabara ya Amani Kampuni ya *MECCO*. Mhe. Spika, ufanyajikazi wake unaleta maudhi pamoja na uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, pale Koani chini kwenye bonde la mpunga anachukua kifusi na mpunga wa watu anaumwagia kifusi pamoja na kuendelea kuharibu bonde lile. Kwa kweli wananchi katika kupunguza umasikini kupitia Idara ya Kilimo pale tunao Mradi wa *PADEP* wa shilingi milioni 50 kwa ajili ya kujenga kisima na kutengeneza *irrigation*.

Mhe. Spika, wakati tulipowauliza wanasema sisi tumeambiwa *open space*, kweli kwenye mabonde ya mpunga ndio *open space*, hivi hawajui wale, yaani mpunga wa wananchi wanyonge ambao wametegemea kupata chakula chao. Kwa bahati mbaya hawa ni wasimamizi wetu tunasema wanapokuja wageni wawepo na wala siwaoni kuzungumza nao. Kwa mfano, leo mchana nimegombana nao, basi angalau kuwaelekeza unatengeneza barabara, lakini na mazingira usiyaharibu.

Kwa kweli siku zote tunasema kwenye miradi pia inazingatia na athari za mazingira kuhusiana na mradi husika, kwa sababu mradi wowote tunaangalia faida zake pamoja na athari za kimazingira na hivyo ndivyo tunavyozungumza. Kwa hivyo, suala hili halikufanywa na wenzetu wa Idara ya Barabara na yule mjenzi anatuharibia mazingira kama vile, kifusi mpaka kwenye migomba anapita na kumwaga tu, basi ni vyema wakapita wakaona. *(Makofi)*

Vile vile kwenye Mto wa Mwera Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri pale patajengwa daraja au vipi naona kunafanywa manyago tu, kunazibwa *culverts* huku na kule hivi majuzi pote palikuwa hapapitiki na kutafuta mitumbwi, kwa sababu lile daraja hivi sasa haliwezi kupitika.

Sasa katika ujenzi wa barabara hii naomba Mhe. Waziri aniambie litajengwa daraja ndio zinatiwa zile *culverts* laa si hivyo pale patakuwa hapana barabara. Nadhani tuweke kivuko kwa ajili ya kuwavusha watu wanaotoka mjini kwenda shamba kutokana na ujenzi ule ninaouona, ikiwa halitojengwa daraja madhubuti, basi tuhakikishe tunaweka kivuko, yaani tunavusha gari zinazokwenda Chwaka, Bambi kutokana na ujenzi ule. Mhe. Spika, mimi si fundi lakini naona anafanya manyago. *(Kicheko/Makofi)*

Pamoja na hayo, mjenzi yule anafanya uharibifu kwa vipando vya wananchi. Kwa hivyo, Mhe. Spika nitawaita watu wa kilimo kwa ajili ya kufanya tathmini na itabidi alipe na nitalishughulikia suala hili kuhakikisha mjenzi anatulipa mpunga wetu ambao alioumwagia kifusi.

Lakini pia kwenye bonde letu ambalo tumesaidia kwa ajili ya kuondosha au kupunguza umasikini kifusi chake kiondoke, kama si hivyo zile konde au ile ardhi yetu ya kilimo itakuwa imeharibika na kama mwekezaji wa kituo cha mafuta basi siku za mvua mafuta yake yataharibika. Vile vile kuna mradi wetu wa skuli nayo itabomoka kwa sababu kwenye eneo la maji ndiko kulikowekwa kifusi, kwa hiyo maji lazima yatakwenda skuli pamoja na kwenye kituo cha mafuta.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akazungumze uzuri na mkandarasi wake laa si hivyo, basi sisi tutampeleka mahakamani kama anamuonea haya. *(Kicheko/Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Idara ya Bandari. Kwa kweli nawashukuru kwa kazi zao nzuri pamoja na mategemeo ya kununua vifaa vipya. Mhe. Spika, sitaki kumjibia Mhe. Waziri lakini kutokana na maelezo ya kitabu cha hotuba labda vifaa vyetu viko njiani, kwa hivyo ndio akaona Al-Ghurba vifaa vyake visije kwa sababu vyetu tumeshaagiza katika mpango huu.

Hata hivyo, nashukuru kwa niaba ya wafanyabiashara wa jimbo langu kwa namna mizigo inavyoshughulikiwa. Kwa mfano, mara moja inapakuliwa kwenye meli na kufikishwa kwenye ghala, tunashukuru kwa shughuli hizo.

Vile vile suala la mpango wa kujenga banda la abiria pale kwenye Gati ya Malindi ni muhimu sana tunashukuru. Lakini kuhusu suala la vifaa vya maboti yetu yanayosafirisha abiria kienyeji kama vile boti na jahazi kwa kweli vifaa vyao bado havipatikani kwa ukamilifu kama vile *life jackets* na mambo mengine. Kutokana na hali hii tunawahimiza mabaharia au manahodha wetu wa vyombo hivi vya kienyeji kutumia vifaa hivi, lakini bado havipatikani.

Kwa mfano, hivi karibuni kulitokea ajali Mkoani na watu wakatumia madumu ya maji kwa bahati nzuri wanayo na kama hawana wangekwenda na maji na yale si mambo ya salamu. Mhe. Spika, tumesikia hapa chombo kilikuwa abiria kumi na tatu na mmoja hakuonekana na kumi wamefika Makoongwe na wengine wamekamata mapira ya maji ya kunywa, lakini kama kungekuwa na *life jackets* ambazo zingewasaidia.

Kwa hivyo, ni vyema kutoa taaluma kwa vyombo vyetu vinavyopakia abiria na hata vyenye kupakia mizigo kwani wanakuwemo watu, vyema wawe na vifaa hivi vya kuokolea maisha wakati mambo haya yanapotokezea.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda unamalizika.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru. Sasa naomba kumalizia kwa kuwashukuwa watoaji huduma wa *Quarry* ya Kibele, kwa kweli wanafanyakazi nzuri sana usiku na mchana. Lakini bado kwa sababu mwaka jana niliwaombea ombi tuwaekee bima watu hawa mazingira ya moshi na vumbi na baadaye mapafu yao yanaharibika na wanaweza kupata maradhi ya *TB* na maradhi mengine ya mapafu na baada ya muda wanaweza kuishiwa na nguvu.

Kwa hivyo, kutokanana na kazi za pale kuna haja ya wafanyakazi hawa waekewe bima. Mhe. Spika, naomba Waziri aje kunieleza amefikia ni hatua gani.

Mhe. Spika, mgeni mnjoo mwenyeji apone hivi sasa tunategemea kuwa na vijiji vya karibu na *quarry* hii itusaidie na hasa vile vijiji vya barabarani kwa kifusi, kama vile Kibele, Bungi, Kikungwi. Kwa kweli tunasikia watu wenye miradi ya utalii husikia kwamba wanawasaidia sehemu za skuli na mambo mengine. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili liwe endelevu, ili na sisi litusaidie na rasilimali ambayo tunayo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nikushukuru wewe pamoja na watendaji wa wizara hii kwa kazi zao, pia ninamuomba Mhe. Waziri aniwekee sawa mambo yangu niliyomuuliza, basi nitamuungana mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunijaalia kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa leo.

Nianze mchango wangu kwa barabara ya Gando. Mhe. Waziri alitegemea kwamba nitaanzia hapa. Mhe. Spika, wananchi wa Gando kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba kutengenezewa barabara yao. Tunashukuru tumepewa matumaini mengi lakini kasi yake kwa kweli ni ndogo sana. Naogopa yaliyomfika somo yangu Mhe. Said Khelef Ali, kuna wakati tama zilimchania nguo kwamba barabara ya Bumbwini tayari, lakini hadi leo analalamika kwamba hali si shwari. Alipenda sana amalize uwakilishi wake barabara iwe tayari, lakini bahati mbaya amesema anastaafu wakati barabara bado anaiacha.

Sasa Mhe. Spika, barabara ya Gando nimepewa matumaini mengi. Ukisoma vitabu hivi vya Mhe. Waziri hata hichi cha mara hii utahisi labda mambo tayari. Kwa kweli bado hali si shwari bado mambo hayajaanza. Pamoja na jitihada kubwa ambayo hapa niisifu ya mtarajiwa Mhe. Waziri Kiongozi amekuwa akifanya jitihada kubwa kuona barabara ya Gando inajengwa lakini wanaomsaidia wanamuangusha. Mhe. Spika, kuangushwa kipindi hichi ni mtihani kidogo. Kwa hivyo, naomba wanaomsaidia Mhe. Waziri Kiongozi waone hii Julai barabara ya Gando imeanza kweli.

Mhe. Spika, nilikuwa na ahadi na Mhe. Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini kwamba kuanzia mwezi wa Disemba angalau wazibezibe watu wapite. Mhe. Spika, wapiga kura walioko jimboni wananambia hiyo kazi ianze hivi sasa. Sasa nina wasi wasi kama kuzibwa zibwa ni hivi sasa yumkini labda kujengwa mwakani, huu ndio mtihani wangu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri

Kiongozi aliponinong'oneza alinambia kwamba Julai hii barabara ya Gando ianzwe na mimi nikawanong'oneza watu wangu wa Gando kwamba Mhe. Waziri Kiongozi anasema wasiwe na hofu.

Lakini kwa ile ladha ladha inayofanywa sasa hivi ipite hofu yangu ni kwamba ujenzi utachelewa sana. Kwa hivyo, naomba jibu la Mhe. Waziri hasa barabara ya Gando nijue vipi ile ahadi ya Mhe. Waziri Kiongozi ndio ile ile au imebadilika. Hilo muhimu.

Mhe. Spika, la pili nilipata habari kadhaa kupitia humu Barazani kwamba upana wa barabara ule ulikuwa uwe karibu mita 18 lakini unaonekana umefinywa kwa sababu nimeona ile Wete/Konde. Sasa kufinywa kule kunanitia wasiwasi mimi sijui ni kwa sababu gani. Nikitazama ile kwa macho yangu ya kifundi fundi karibu mita 5 hazimo. Kwa hivyo, nikaangalia hizi mita 5 atafaidika nani. Kama *contractor* yeye atasema *Alhamdulillah* kwa sababu alikuwa ajenge mita 18 sasa anajenga mita 5 kwake yeye ni nafuu, sasa sisi kama wananchi tutakuwa tume- *lose*. Mhe. Spika, ningependa kujua ile tutafidiwa vipi.

Lakini Mhe. Spika, nilivyosikia eti serikali inafanya vile kwa sababu inaogopa kulipa fidia za majumba. Sasa kama ni hivyo kwa kweli hatuwezi kwenda hivyo kwamba tunaacha usaidizi wa mpana mkubwa kwa sababu tu tunaogopa kulipa fidia ya majumba au vipando hii haikubaliki. Kwa hivyo, nataka kujua hasa kwa mujibu wa mkataba zile barabara ni mita ngapi na mlivyokubaliana hasa kujenga ni mita ngapi.

Mhe. Spika, katika hilo naomba nitoe masikitiko makubwa kwa namna ya fidia za nyumba za wananchi na utaratibu mbovu wa fidia zenyewe. Kwa kweli hapa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi sijui inamkodi nani kufanya ukadiriaji. Mhe. Spika, inaonekana kwanza ule ukadiriaji wenyewe si wa heshima hata kidogo. Mwananchi wenyewe hashirikishwi katika ukadiriaji wenyewe, anakuwa mkadiriaji anaangalia halafu anakwenda, hata sheha, diwani bahati mbaya hawashirikishwi. Sasa mambo haya vipi, hii bwana tumejitawala, haiwezekani kwamba mtu aende katika nyumba ya mtu afanye ukadiriaji, huu utaratibu mbovu sana. Hata mtu haambiwi kwamba bwana eee tunaikagua nyumba yako kwa sababu labda inataka kuvunjwa.

Lakini Mhe. Spika, baya zaidi ni kwamba nyumba inatolewa ukuta mmoja wa mbele halafu analipwa malipo ya ukuta mmoja. Sasa Mhe. Spika, haiwezekani, kama nyumba ukuta mbele umetoa ina maana nyumba umeivunja. Huwezi ukasema kwamba barabara imezidi huko mbele tunatoa ukuta mmoja au vyumba viwili halafu tutakulipa malipo ya vyumba viwili au ukuta mmoja. Mhe. Spika, hiyo ni kumuonea mwananchi na kumrudisha katika umaskini.

Kama umevunja ukuta wa mbele au vyumba maana yake hiyo nyumba haipo tena, huwezi ukafanya ujanja ujanja hivyo katika kumdhulumu mwananchi. Kwa hivyo, huo ni utaratibu mbovu siupendi hata kidogo.

Mhe. Spika, jengine ni lile ambalo alisema Mhe. Haji Mkema Haji tatizo la *siltation* , ile husababisha mchanga katika mashamba na ardhi ya watu, hili ni tatizo jengine. Makampuni haya yanapofanya kazi hizi kwa mfano *MECCO* huchukua mchanga wakaweka katika shamba la mtu rundo la mchanga bila ya *consultations* wa yule mtu na athari ambayo itaifanya kuondoa ile mbolea. Lakini baya zaidi mfano Pemba ina vilima ule mchanga unachukuliwa unakwenda katika mashamba huko bondeni inasababisha athari kubwa sana ya kilimo. Sasa hii serikali sijui tunakwendaje, kwa kweli mambo haya ya kimazingira hatuwezi kuiachia nchi iende hivi. Wananchi wanalalamika kwa mfano kuna jamaa mmoja pale kila siku anagombana nyumbani na mpira kura wangu, bwana namna gani wewe hii ni shamba yangu.

Sasa Mhe. Spika, hatuwezi kuyaachia makampuni liwe namna hii kuwaathiri wananchi wetu na zaidi shughuli zetu za kilimo. Shughuli za kilimo kwa kweli zinaathirika sana katika utaratibu huu mbaya. Wenzetu wanafanya utaratibu kwanza wakaangalia namna gani athari za mazingira zinazovyoingia katika mashamba na vipando vya watu. Mhe. Spika, sisi kwetu tunawaachia makampuni wanafanya wanavyotaka na wakiondoka athari zile zinarudi kwa wakulima wetu. Sasa hili naomba nipate ufafanuzi.

Mhe. Spika, jambo jengine ni Shirika la Bandari kweli linafanya kazi nzuri lakini lina matatizo mawili matatu. Kwanza nimetumwa na wapiga kura wa Gando na Fundo kwamba bado mnara wa Kigomasha hauwaki. Sasa hili nimelisema tangu mwaka 2003 nikaahidiwa sijui kuna tatizo gani, unawaka siku mbili halafu unazima. Mhe. Spika, mnara wa Kigomasha una hadhi ya kimataifa, tutakuja kulipa fidia hapa iwe mtihani mkubwa. Sasa sijui inakuwaje mnara kama ule wa siku nyingi mpaka leo uwe uwakaji wake hauna uhakika hata mdogo. Kwa hivyo, naomba kujua tutafanyaje ili mnara ule uwe unawaka moja kwa moja.

Mhe. Spika, zamani kulikuwa na taa hata ikiwa mbali kiasi gani ulikuwa unaona. Kama hizi walizoziweka sasa haziwaki rudisheni zile lakini ule umuhimu wa mnara uwepo. Hatuwezi kujitia usasa tunaeka mataa ya ajabu ajabu yakawa yanaathiri wavuvi, yanaathiri wasafiri, yanaathiri meli ni bora rudisheni yale mataa ya zamani lakini ilimradi mnara uwe unawake. \

Mhe. Spika, jambo jengine ni suala la Bandari ya Wete. Mhe. Spika, katika kitabu hiki cha Mhe. WAziri ukurasa wa pili kuna sentensi naomba niisome kwamba kadhalika wizara imeweza kukamilisha miradi ya miundombinu ya

Bandari ya Malindi, upanuzi wa Bandari ya Wete. Mhe. Spika, hii sentensi upanuzi wa Bandari ya Wete sijui labda kwa vile sijapita karibu wiki mbili mpaka tatu, lakini Bandari ya Wete ni kwamba haijafanyiwa upanuzi hata kidogo, imefanyiwa marekebisho kidogo ili tuweze kupita kwa hilo tunashukuru. Lakini huwezi kutia sentensi ya upanuzi wa Bandari ya Wete kilichofanywa ni kuifanya ipite tu kidogo angalau kunyanyua zile kuta kidogo. Mhe. Spika, nimewahi kuzungumza sio mara moja wala mara mbili, mara moja tuliita uongozi wa Shirika Wete Kamati ya *PAC* tukawaambia katika vitabu vyenu munaonesha kwamba kumeongezwa mita mbele, lakini uhalisia wa sisi wenyeji wa pale hakuna mita iliyoengezwa *just* mmenyanyua kwa juu lakini kwa mbele hamjanyanyua na tukawashauri ikiwa wanataka kunyanyua waende shimoni kwa sababu kuna bandari ya nguzo imejengwa meli ndogo ndogo zinafunga lakini hali hiyo haikufanyika. Mhe. Spika, sasa kwa hapa hali ilipo naiomba Mhe. Waziri aangalie kama ana nia ya utanuzi wa Bandari ya Wete ufanywe kwani tunahitaji sana sisi watu Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Spika, kuna jambo ambalo na mimi nimelipata hili la *crane* kwa kweli hawa watu binafsi ambao wanataka *crane* naomba nijibu la Mhe. Waziri kwa sababu kauli niliyoipata mimi ni kwamba Mhe. Waziri alikubali. Kwa hivyo kama Mhe. Waziri amekubali katika wizara hii ndiye anayemsaidia Rais na Rais bila shaka ameshakubali Waziri asingeweza kukubali jambo zito kama hili.

Kama Mhe. Waziri ameshakubali na wakubwa wameshakubali sidhani kama kuna mwengine anaweza kuzuia. Kwa hivyo, kama mpaka leo hakuna jambo lolote hilo itakuwa haiwezekani, uwekezaji binafsi katika nchi hii tunauhitaji sana. Kwa hivyo, ikifika pahali kama waziri amekubali lazima asimamie kuona kwamba walio chini yake makubaliano hayo wameyaheshimu.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nalipigia kelele tokea mwaka juzi ni kwamba shughuli za Shirika la Bandari zinaporipotiwa katika Baraza hazielezi zitatumia fedha gani. Mhe. Spika, hatuna maana kwamba tukubali fedha zile, lakini ni vizuri mnapolizungumzia kwamba tutajenga jambo fulani mfano, tutajenga Bandari ya Mkokotoni ni vizuri Baraza liambiwe kwamba shirika litatumia bilioni moja.

Lakini kutaja maelezo tu kama shirika litajenga bila ya kuwa na *monitory quantity* ambayo itatumika kwa kweli huu sio utaratibu mzuri. Imesema mwaka jana na imerudia tena mwaka huu paragraph 107, 108, 109, 111 na 112 ya maelezo ya Shirika la Bandari yametaja nini watafanya, lakini haielezi kiasi gani cha fedha kitatumia. Mhe. Spika, haina maana kwamba sisi tuidhinishe lakini tunaweza kutia baraka tukasema hizo pesa kidogo au nyingi, lakini ya

kuweka *black* kama hakuna kima cha fedha kinachotumika huo sio utaratibu mzuri wa kibajeti.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nataka nizungumze ni ujenzi wa barabara. Mimi nawapongeza sana shughuli ambazo zimefanywa na Idara ya Barabara shughuli zake kwa kweli zimefanya kazi nzuri. Mimi hawa ni wenzangu sana hawa watu wa barabara. Lakini kuna tatizo kidogo kiambatanisho Nam. 1 ukurasa wa 59 mimi ingelikuwa namsaidia Mhe. Waziri basi nisingekiweka. Mhe. Spika, kule juu kuna barabara zilizojengwa katika kipindi cha uongozi wa Mhe. Amani Abeid Karume. Ni sawa lakini kwa vile lilivyo ni sawa sawa na kumpakatisha maiti Rais, bora angetia katika kipindi hiki cha uongozi wa Mhe. Machano kwa sababu mna maajabu maajabu mimi siyapendi kuyataja lakini maradhi mengine huwa nalazimika.

Mhe. Spika, kuna barabara zilizokamika baina ya Unguja na Pemba, ukiangaila za kwanza kukamilika kuna barabara za Pemba na barabara za Unguja. Barabara za Pemba ukipiga mahesabu ni 60 za kipindi hiki, barabara za Unguja ni karibu 200. Mhe. Spika, utekelezaji wa ilani namna hii una mtihani kidogo, hatuwezi kuruhusu hata kidogo ilani ya chama itekeleze kama hivi. Mhe. Spika, nashangaa watu kama Mhe. Dadi Faki Dadi ni watu wa *very active* lakini baadhi ya mambo kama haya yanahitajika Mhe. Spika, haiwezekani hata kidogo kidogo.

Kwa hivyo inanipa mimi kwamba kisiwa kimoja kinaonekana kina *very lion share* lakini kisiwa chengine kimeburuzwa sana *sixty agency two hundred is not good* hata kidogo kidogo, hatuwezi hata kidogo kujisifu kwa ilani kwatika hali kama hiyo. Lakini baya zaidi Mhe. Spika, hata maengenezo ya mfuko wa barabara nilikuwa naangalia kiambatanisho Nam. 5 *page* 66 nacho kinakirihisha kidogo hakipendezi hata kidogo kidogo, nilikuwa naangalia matengenezo makubwa katika kiwango cha lami hapa Unguja pana barabara kumi na mbili, Karakana ukiangalia *page* 66 na 67.

Lakini Pemba kuna matengenezo vibarabara vitatu Kichunjuu, Mtambile, Vichungwani, Machomane na Vitongoji sasa hii haiwezekani Mhe. Spika, hatuwezi kuwacha bajeti kwenda katika mrama namna hii huu si utaratibu mzuri hata kidogo kidogo, mimi naupigia kelele na siwezi kuuruhusu uwende hivi. Sasa mimi naomba majibu ya Mhe. Waziri kwa nini akawaruhusu watendaji wake watekeleze mambo katika utaratibu kama huu, baya zaidi katika ukurasa wa 70 na 71 nayo malengo ya mwaka 2010/2011 yamefuata mpango huo huo kuna barabara kumi na tatu kwa Unguja, halafu kuna vipande vitatu vya Pemba.

Sasa hii Mhe. Spika, mimi nitakuwa mgumu sana mpaka pale Mhe. Waziri atakapotoa majibu lakini sidhani kama anayo kwa utaratibu huu, lakini kama anayo basi naomba. Mwisho naona muda unakwenda zake mbio katika suala hili nilimuomba. Nakushukuru Mhe. Spika, Ahsante.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 6/7/2010 Saa 3.00 Asubuhi)